**Mpadri Georgie Kuyumjoglu**

# KITABU YA KUMUABUDU MUNGU

## YA KILA MWAMINIFU ORTHODOKSE

**Mufasili**
**Mutawa Damaskinos Grigoriatis**
**2005**

**Centre de la Mission Orthodoxe**
**Bujubura-Burundi**
**2005**

# SEHEMU YA KWANZA

## Kuabudu Mungu na uzima katika Kanisa

## 1. Fundisho juu ya Kumuabudu Mungu

Ndani ya roho ya kila mtu ni matakio mengi na anataka ya kumalizwa kwa kuleta furaha kwa mtu. Matakio kabisa kubwa ni ile inanyoloka kwa Mungu. Hii matakio ya mtu ni mapatano yake pamoja na Mungu na hivi tunasema juu ya dini ya mtu, nikusema mapatano kati ya Mungu na mtu. Hii mapatano haiko ni kazi ya akili, lakini ni uzima ya kiroho. Haiko fundisho ya akili, lakini ni uzima ya kiroho. Hii inatuonyesha ya kama mtu anashirika na Mungu katika roho na akili na matakio yake yoyote. Hii onyesho yake unamalizwa kwa namna ya kumuabudu Mungu kwa ajili yake mutu anaungana na Mungu.

Hii kazi ya kuabudu Mungu ni tendo ya kila mtu anayependa Mungu. Kwa hivi dini haiko paka mahasa, lakini ni hekima na mapenzi na yanatumika ma vipande yote ya mutu juu ya kumuabudu Mungu.

### 2. Namna ya kumuabudu Mungu katika Kanisa Orthodokse.

Kazi ya kumuabudu Mungu kwa Waaminifu wa orthodokse inamalizwa katika Kristu na Roho Mtakatifu. Mizizi yake ni mirefu na ya kweli. Ufananisho ya Kanisa ni katika Kristu na kati ya Kanisa Yake.

Ndani ya Agano la Kale tunapata mafundisho ya kama Mungu mumoja anapatia kwa Musa hamuri Yake namna gani mutu ataweza kumuabudu Mungu. Kwa hivi unatengenezwa kundi moja ya ma sheria kwa ajili yake mtu anaweza kuonyesha kuabudu yake mbele ya Mungu. Hii namna ya kuabudu Mungu ilibaki mpaka alikuja duniani Yesu Kristu. Kisha Yake ulijikombola kwa sadaka ya Komonyo Takatifu na namna ya kumuabudu Mungu ilikuwa ya kumushukuru Kwake na kupata Mwili na Damu Yake.

Kuabudu Mungu sasa ndani ya Agano Jipya ni ya kupata mwaminifu Orthodokse Komonyo Takatifu. Maana ya hii Fumbo ni shukrani mbele ya Mungu. Hii kila mwaminifu anamutukuza Mungu, kama anapewa Mwili na Damu yake na hivi anaokolewa na anatimiza kusudi ya uzima yake. Mtu anayeokolewa kwa sadaka ya Yesu Kristu, anamuabudu Kristu katika uzima takatifu yake.

Mtakatifu Bazile anasema ya kama Kumuabudu Mungu ya kweli ni kazi ya kuponyesha mtu ma zoezo mabaya yake katika neema ya Mungu. Vile anasema na Mtume Paulo mu barua yake kwa Waroma: "Kwa sababu ya huruma yake Mungu, ninawasihi mujitoe wenyewe kuwa sadaka iliyo hai, takatifu na ya kumupendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana". (Waroma 12,1). Hii sauti yake inatuonyesha ya kama tunaabudu Mungu na namna ukweli, kama uzima yetu inafanyika sadaka muzima, kama uzima yetu unajitoa na unatumika Mungu, lakini sauti ya mt. Yoane Krisostomo, mtu moja anamuabudu Mungu ya kweli, kama anaishi katika sheria ya hamuri ya Mungu. Kwa hivi, kusudi ya kuabudu Mungu ndani ya kanisa Orthodokse ni unganisho ya mutu pamoja na Mungu, sawa vile waliishi wazazi wa kwanza ndani ya paradizo pamoja na Mungu.

Mtakatifu Maksimos Musimamizi ya imani anasema: „Kuabudu Mungu katika namna ya kweli ni kama mtu anajaribu ya kutakasa nafsi yake“. Tena anasema: „Hasiweze mtu moja kumuabudu Mungu, kama roho yake inaikaa na uchafu ya zambi yoyote“.

Mtakatifu Isaya wa Jangwa anasema: „Kama tunasoma ao tunaimba wimbo ya Mungu kila siku, lakini tunakataa kusafisha roho yetu ya kila zambi, Mungu hasikubali hii sandaka yetu“.

## Uzima ya kiroho

Tunajua ya kama Adamu alifata mapenzi yake na alikataa kufata mapenzi ya Mungu. Ku mwisho alipotesha ushirika yake pamoja na Mungu na alifukuzwa toka Paradizo. Kisha akili ya mutu iliharabika na akili yake inazoea kufata matakio ya hii uzima.

Juu ya kushindi mtu hii zoezo mbaya, inapaswa kusali na kujaribu, kufatana mufano ya Yesu Kristu na Mitume wake. Kwa hii uzima ya kiroho mtu anaweza kusafisha roho yake ya kila zambi na hivi ataweza kuabudu Mungu na namna ukweli.

Uzima ya kiroho anafanya mtu hapana paka ndani ya Kanisa, lakini mbele ya kila dakika ya uzima yake. Tunasali kila asubuyi na magaribi na usiku kanisani, lakini hii saa ya sala itakuwa mwanzo juu roho ya kila mtu kujaribu ya kubadilisha uzima yake yote katika uzima ya sheria ya Mungu.

Uzima ya kiroho haiko paka shukrani mbele ya Mungu kwa zawandi yake, lakini ni matakio moja ya siri yake kwa kumushukuru Mungu kwa sababu alituma Mwana wake wa pekee kwa wokovu wake.

Uzima ya kiroho ni ushirika ya upendo kati ya Mungu na mtu. Mtu anakubali upendo wanadamu na rehema kubwa ya Utatu Mtakatifu na anatoa kwa Mungu roho yake ya kutubu, kushukuru na kutukuza Mungu. Roho yake inaliya kwa upendo ya Kristu na haipumuzika mpaka atatosha kila uchafu mbaya na ataingisha ndani ya roho yake neema ya Mungu.

Kabisa mwaminifu Mungu anamutukuza na anamuabudu Mungu na namna ukweli, kama anasali kwa siri siku na usiku na sala ya Bwana Yesu. Ni hii: Bwana Yesu Kristu, Mwana wa Mungu, unihurumie mimi mwenye zambi“. Kama, hana kazi ya haraka, anakimbilia Kanisani. Kabisa anaenda kila siku ya Mungu na kwa shangilio ya Watakati yetu.

Namna ya kuabudu Mungu ni matoleo ya Mwaminifu ma zawandi yake. Nikusema anaweza kutoa Kanisani Prosforo (mukate ya kutosha mpadri Mwili ya Kristu), vinyo, mafuta, mishumaa na vittu vingine.

Ndani ya kanisa kila mwaminifu anaweza kupandisha akili yake mbinguni juu ya kuunganisha roho yake pamoja na Neema ya Yesu Kristu. Kwa hivi roho yake unapata utulivu na unasikia ndani yake amani.

## Ma uso ya hii uzima ya kuabudu Mungu

Nyuso ya kwanza ndani ya kanisa ni Utatu Mutakatifu: Baba, Mwana na Roho Mtakatifu.

Nyuso ya mbili ni taifa, nikusema wapadri wote na waaminifu wote.

Juu ya kuabudu Taifa  Mungu na namna ukweli inalazimishwa kufanyika mapatano katika upendo kati ya waaminifu na ya Mungu. Juu ya kuendeleshwa hii mapatano inapaswa waaminifu ya kuendelea uzima yao ya kiroho.

Juu ya kumaliza sisi kazi ya kumuabudu Mungu tukona lazima ya wapadri ya kanisa yetu. Hawa weko wafwasi ya Mitume, kwa sababu Mitume walichukua neema ya Roho Mtakatifu na kisha waliipatia hii neema kwa wanafunji wao ya kuweka mikono vyao pa vichwa vyao. Wafwasi ya Mitumi ni wa askofu, wapadri na wa shemasi. Hawa weko watumishi watakatifu wa Mungu.

Sasa kila mpadri inapaswa kuangalia namna gani ataabudu Mungu kila siku, bila ma kosa yake. Mtakatifu askofu Bazile anasema hivi juu ya kila pandiri:

«Ee Mpadri, angalia ya kuwa tayari, ile wakati utasimama mbele ya Altari Takatifu. Haipaswe kusikia haya, wakati utakuwa mbele ya Altari ya Mungu.

Usisimame mbele ya Altari ya Mungu, kama unachunga ndani ya roho yako chuki hata kidogo mbele ya mtu fulani, kwa sababu utakuwa sababu na Roho Mtakatifu atakimbia ku uzima yako.

Ile siku ya Mungu usihukumu mtu hata moja, wala ya kufanya mabishano na mwaminifu moja. Ingia Kanisani ya kusali na kusoma mpaka ile saa utamaliza kazi kimungu yako. Simama mbele ya Altari katika woga ya Mungu, unyenyekevu, roho usafi sawa unasimama mbele ya Mufalme wa mbingu.

Usisome ma sala yako na haraka na bila kusikia maana yao, kwa sababu uko na kazi ingine ya dunia. Paka angalia Mufalme wa mbingu na majeshi ya malaika, wenye wanasimama pempeni yako na wanakuangalia.

Tena fata ma Kanuni ya Kanisa na ya makutano Ikumenike(ya Ulimwengu).

Usifanye Liturgie pamoja na hawa wapadri ma Kanuni yanazibiliya.

Angalia, unasimama mbele ya nani, namna gani unatoa sandaka yako na kwa mwaminifu gani unamupatia Vitu Vitakatifu.

Usisahau hamuri ya Rabi wetu Yesu Kristu: „Musiwape imbwa Kitu Kitakatifu, wala musitupe lulu zenu mbele ya nguruwe, wasije wakazikanyaga, na kisha kuwageukia ninyi na kuwashambulia“ (Matayo 7,6).

Angalia usimutoa Mwana wa Mungu kwa mikono wasiyostahili.

Usiogope watu wakubwa ya hii dunia, wala na huyu anayevaa taji ya utawala wake.

Kwa hawa watu wanakanyanga ma kanuni, haipaswe kuwapatia Komonyo Takatifu.

Angalia juu hapana kuingia kwa ajili ya uzaifu yako, panya ao panjo ao kitu ingine ndani ya Kikombe Kitakatifu. Angalia juu hapana kuharabika Mwili ya Yesu Kristu ao ya kupata simoko ao ya kujitimia kwa watu wasiyostahili.

Kama utachunga mafundisho haya yote, utaweza kuokoa na maugu yako na utasaidia na wale wanakusikia.

## Mwimbaji

Katika fundisho ya Kanisa Orthodokse, bila mwimbaji haimalizwe Liturgia Kitakatifu. Mwimbaji anaimba na anasaidia mpadri kwa jina ya taifa ya waaminifu.

Kila mwimbaji inapaswa kuvaa kanzo meushi yake.

Anasimama pa fasi yake, bila kujitenga ao kuondoka.

Anakataa kuzungumuza ya ma dakika mengi na kama zungumuzo ni ya ovyo. Tena hasicheke, hasiseme sauti ya cheka watu weingine na hasijitenge sana mukono ya kufanya wakati kwa wimbo yake.

Aipaswe kuangalia waaminifu ao kuwafokea juu ya kusimama hawa nzuri bila kuzungumuza.

Anashauria wasaidizi wake, bila kuwafokea, bila udanganyifu na bila tabia mbaya.

Anachunga akili yake na anasali na heshima na woga mbele ya Mungu, mbele ya mpadri na mbele ya watu.

Anafanya alama ya Musalaba na hivi anasaidia waaminifu weingine wakati gani na namna gani wanapaswa kufanya alama ya Musalaba.

Kama anaimba wimbo ya Katavasies, anashuka chini ya kiti zake. Tena, kama mpadri anabariki kusema: Vichwa vyetu tuinamisha kwa Bwana“, na yeye anainamisha kichwa chake.

Anafata uzima ya kiroho, nikusema anaungama na anapewa Mwili na Damu ya Kristu kila wakati.

Anafanya nguvu juu ya kufata na kuchunga mafundisho yote ya Muzike Vizantine. Na anajaribu ya kufundisha na vijana kwa kufata hii muzike ya Kanisa yetu.

Kama anaimba katika roho, anapandisha roho yake mbinguni na anasikia furaha kubwa. Tena inafanyika mufano muzuri mbele ya waaminifu ya Kanisa.

Mwimbaji moja haipaswe kujivuna kwa sauti nguvu na utamu yake. Lakini inapaswa kuuwaza ya kama Mungu alimupatia hii zawadi juu ya kumutukuza.

## FASI YA KUABUDU MUNGU

Kanisa ni fasi pahali tunaweza kumuabudu Mungu. Inaitwa na makao ya Mungu. Ndani ya kanisa (fasi yake juu pia) inaonyesha mbingu na dari ya chini inaonyesha inchi. Maana ya Kanisa ni makusanyo ya wale watu wanaamini Kristu na wanakuja kwa kusali na kumuabudu Utatu Mtakatifu.

Ndani ya kanisa inafanyika Fumbo ya Komonyo Takatifu, iliyefanyika mara ya kwanza mu Karamu Kubwa, mu kazi ine njioni na Yesu Kristu aliwapatia kwa Mitume wake Mwili na Damu Yake.

Mtakatifu Yoane Krisostomo anasema ya kama Kanisa ni obitalo ya kiroho na kila mtu anayepewa mwili na Damu ya Kristu anaponyeshwa katika uzima yake ya kiroho.

Kanisa ya kwanza mujini Yerusalema ilikuwa Hekalu ya Solomono, iliyeitwa nyumba ya sala ao nyumba ya Baba ao Makao Mtakatifu. Kisha inafwata ile Nyumba Bwana Yesu Kristu alifanya Karamu Kubwa pamoja na Mitume wake. Kisha yanafwata ma Kanisa ya nyumba ya waaminifu. Nikusema waaminifu wa kwanza walisanyikwa ndani ya nyumba fulani yao na kule walisali na walifanya Fumbo ya Komonyo Takatifu. Ile wakati ya mafukuzo ya Kanisa ya Kristu, waaminifu walisali na walifanya Liturgia ndani ya ma nyumba chini ya bulongo (Katakombe).

Kisha uhuru, kisha ya mwaka 313, waaminifu walifanya Liturgia juu, pa ile fasi walikufa kwa mateso mengi Mashahidi wa Kristu. Na, tangu wakati ya kujifamia dini ya Kristianisme, (tangu ku mwaka 313 na kisha) waaminifu walijenga kanisa yao makubwa kwa sheria ya utawala ya Konstantinopoli, ile wakati mufalme ya kwanza alikuwa mtakatifu Konstantino Mkubwa.

Kila kanisa ya Kristu iko na vipande tatu : Altari Takatifu ni fasi kabisa ya wapadri. Kipande ya mbili inaitwa Naosu, pahali wanasimama waaminifu wote na kipande ya tatu inaitwa Narthikas pahali wanasimama wa katikumeni.

**Altari Takatifu:**

Hii kipande ni kitakatifu kupita ya vipande ya kanisa ingine. Ni sawa kichwa ya mwili muzima. Inaitwa Altari Takatifu, Mazabahu, Vitu Vitakatifu na ma jina ingine. Ni kidogo juu pia ya ingine kanisa na inajigawanya na kibabashi moja ya mbau, pahali ni ma Picha ya Yesu Kristu, Mzazi mwake na Watakatifu ya mbali mbali. Hii kibabashi ya mbau inaitwa Ikonostasi ao Templo.

Ndani ya Altari Takatifu ni haki ya kuingia paka wapadri yoyote. Watawa wanawake wanaweza kuingia, paka kwa baraka ya askofu yao juu ya kusafisha (Kanuni 15, ya Mt. Nikola, patriarshi ya Konstantinopoli). Wala wanaume, wala wanawake inapaswa kuingia ndani ya Altari Takatifu, katika Kanuni 69 ya Makutano Sita ya Ulimwengu).

Altari Takatifu inaonyesha mbingu, pahali ni Kiti kubwa ya Mungu. Altari ni daima paka pa fasi ya mashariki, pahali inapanda jua, juu ya kusali waaminifu kwa kuangalia pa fasi ya mashariki. Kwa sababu Yesu ni Jua ya Uhaki. Tena sisi wote tunapaswa kutafuta inchi yetu ya zamani kabisa, nikusema Paradiso iliyekuwa pa fasi ya mashariki.

Ndani ya Altari Takatifu tunaweza kuangalia : Meza Takatifu, Prothesi Takatifu, pahali inafanyika matayarisho ya Liturgia Kimungu (Proskomidi). Synthrono, nikusema mu nyuma ya Meza zamani yalikuwa viti kwa kuikaa patriarshi na wa askofu wake. Pa fasi ya kuhume ya Altari ni Skevofylakio, nikusema fasi pahali ndani ya kabachi wa shemasi wanachunga vitu vitakatifu, sawa kikombe, Sahani takatifu na vitu vya Kanisa ingine.. Pa fasi ya kushoto, pempeni ya Prothesi ni fasi ya kusafisha padri mikono yake. Inaitwa Niptiras. Pamoja ni na Honeftirio, pahali maji inatoka inje ndani ya kisima moja.

**Meza Takatifu**

Pa hii Meza inachinjwa Yesu Kristu sawa Mwana Kondoo kwa uzima ya kiroho ya waaminifu wale wanamuamini na wanamufwata. Kama mukristu moja hasikule na hasikunywe Mwili na Damu yake ni mufu katika uzima ya kiroho.

Maana ya Meza Takatifu ni Kiti ya Mungu. Na sawa vile pempeni ya Kiti ya Mungu wanasimama malaika, vile na pempeni ya Meza Takatifu inasimama kundi ya wapadri na kati yao ni mkubwa askofu wao kwani yeye anaonyesha Askofu Mkubwa Bwana Yesu Kristu. Tena Meza inatuonyesha na Kaburi ya Yesu Kristu. Sawa Mungu anaikaa pa Kiti zake halafu sawa mtu anajitoa sawa sandaka kwa uzima na wokovu ya dunia nzima.

Sula ya Meza ni sawa kare ao sawa paralilograme. Inasimama pa nguzo (colone) moja ao pa colone inne. Colone moja inatuonyesha Yesu Kristu na kama Meza inasimama pa colone ine inatuonyesha Waevangelizaji wa Ine. Kwa ile siku ya Ubatizo ya Meza Takatifu, katikati yake askofu anaweka vipande ya Mifupa ya Watakatifu. Kanisa ingine juu ya Meza Takatifu ni dari moja ya mbau ao ya jiwe. Hii inaitwa Kivorio na maana yake inaonyesha mbingu na chini yake ni inchi.

Liturgia Takatifu pa Meza inafanyika paka moja kila ma saa makumi mbili na ine (24), kwa sababu na Yesu Kristu mara moja alijitoa pa Musalaba kwa wokovu ya watu wote ya dunia. Kama inalazimishwa ya kufanyika na Liturgia ya mbili, kwa mufano, usiku, mbele ya Meza takatifu mpadri ataweza meza ingine na juu yake atamaliza Liturgia na usiku atafanya Liturgia pa Meza Takatifu, lakini juu ya Antiminsio ingine. Antiminsio ni Kitambaa Takatifu pahali juu yake ni kati Yesu Kristu ya kularia, kisha ya kumushusha toka Musalaba mwake na pa fasi ya kona ine ni ma picha ya Waevangelizaji. Bila hii Kitambaa, inayeitwa Antiminsio, inakatazwa mpadri afanye Liturgia.

Juu ya Meza na katikati yake ni Evangelio, inayeonyesha Yesu Kristu sawa ya kuikaa kama Mufalme pa Kiti chake. Antiminsio ni chini ya Evangelio. Mbele ya Evangelio ni Artoforio, pahali mpadri anachunga Mwili na Damu ya Yesu Kristu juu ya kukomunyika wale waaminifu weko wagonjwa na wanalazimishwa na haraka Komonyo Takatifu. Pempeni ya kuume ya Evangelio inajiweka Musalaba ya baraka na hii askofu anabariki waaminifu, wakati anafanya Liturgia.

Pa fasi ya kushoto ya Altari Takatifu tunaangalia :

**Prothesi Takatifu**

Pa hii Meza inafanyika matayarisho ya kufanya mpadri Lirturgia Kimungu. Nikusema atasoma ibada moja inayeitwa mu lugha kingiriki Proskomidi. Mpadri anachukua Prosforo (mukate sawa muvirigo). Anaibariki, anatosha Kipande ile ni katikati na inaandika IS. XR. NIKA na ataiweka kati ya Sahani Takatifu. Hii Kipande itafanyika Mwili ya Yesu Kristu. Hii Prothesis, pahali inafanyika Ibada ya Proskomidi inatuonyesha pango ya Bethlehemu. Tena inatuonyesha na Kalvario, ile wakati mpadri anatayarisha Vitu Vitakatifu. Na picha ile ni ndani ya Prothesis iko na pango ya kuzaliwa Kristu ao Bwana Yesu katika unyenyekevu kubwa yake.

**Naosu**

Ni ile fasi ya kanisa pahali wanasimama waaminifu na wanasikia wimbo na Liturgia. Ndani pa fasi ya kuhume ni Kiti ya askofu. Pa hii kiti ni picha ya Bwana Yesu juu ya kumukumbusha kwa kila askofu, ya kama Yesu Kristu ni Bwana na Rabi wa pekee na kila askofu ni pa fasi ya Yesu Kristu na atapatia jibu mbele ya Kristu juu ya matendo yake yoyote.

**Narthikas**

Ni fasi ya kwanza ya kanisa. Leo ma kanisa mengi hawakuwa na Narthikas. Ile wakati ya Mitume Wakatikumeni, wenye walitaka kufata imani ya Kristu, walipata mafundisho pa hii fasi ya kwanza. Toka hii fasi Wakatikumeni walisikia na Liturgia Kimungu.

Ndani ya Narhikas ya kanisa ile ni ndani ya monasteri moja watawa wanasoma Ibada ya Liti, Ibada kati ya Usiku, Saa yote, Apodipno Kidogo na Ibada ya Kiliyo ya wafu. Juu pia ya Narhikas ni fasi ingine, iliyeitwa Ginekonitis, pahali walipanda na walisikia sala yoyote wanawake.

# Vitu vyote ya kumaliza mpadri kazi ya kumuabudu Mungu

## Maguo ya meza Takatifu

Nguo ya kwanza juu yake inaitwa Katasarkio na iko nguo moja meupe. Paka askofu anaiweka pa Meza takatifu ile siku ya kuibatiza Kanisa. Maana yake ni ya kutukumbusha ile sanda walimufunika mwili ya Bwana Yesu Kristu juu ya kumuzika.

Nguo ya pili inaitwa Endyti. Huu ni nguo ya inje, muzuri sana na ragi yake ni ya mbalimbali. Ile wakati ya Kwarezima, mbele ya Pasaka hii Endyti iko na ragi nyekundu, kwa sababu tunamuomboleza Yesu Kristu hapana sawa mtu aliyekufa ya milele, lakini sawa mufalme aliyefufuka kwa utukufu.

Nguo ya tatu inaitwa Ilito. Huu ilijisambaa, kama ilianza Fumbo ya Komonyo Takatifu. Fasi yake ni ya kufungwa chini ya Evangelio na inafunguliwa kama ilianza Fumbo ya Eukaristia.

Nguo ya ine inaitwa Antiminsio. Urefu na mnene yake ni 40x50 cm. Katikati yake ni ya kufatula Kristu kisha lufu yake sawa ya kulala. Kama mpadri moja anafanya Liturgia inje ya Kanisa, inapswa kufanya hii Liturgia paka juu ya Antiminsio. Nikusema hii Kitambaa Takatifu inakombola Meza Takatifu.

# Manguo ya Wapadri yote.

Maana ya Manguo haya ni ya kama mpadri moja hasimalize ma Fumbo yote katika nguvu yake, lakini kwa jina na uwezo ya Kristu na nguvu ya upandirisho yake. Manguo yote ni saba sawa na saba ni ma zawadi ya Roho Mtakatifu.

Kila shemasi anavaa maguo tatu : Stikhario, Orario na Epimanika.

Kila mpadri anavaa maguo tano : Stikhario, Epitrakhilio, Epimanika, Zoni (musipi) na Felonio.

Kila askofu anavaa maguo saba: Stikhario, Epitrakhilio, Epimanika, Zoni (musipi) na pa fasi ya Felonio anavaa Sakkos. Kisha nguo ingine ni Epigonatio na Omoforio. Kisha yaliongezeka na vitu ingine, sawa Musalaba pa kilari yake na Egolpio. Tena askofu anakamata na Bakora, inayeitwa Ravdos Pimantiki na kofya kubwa na nzuri inayeitwa Mitra.

Maana ya kila nguo takatifu ya wapadri:

**Stikhario :** Ni kanzo moja urefu na wanavaa wapadri wote, shemasi, mpadri na askofu. Mikono yake ni mirefu na mnene. Ragi yake ni meupe, maana yake ni onyesho ya uzima safi ya mpadri na alama ya furaha ya kiroho. Tena inaonyesha mavazi ya Malaika na usafi na isiyo uchafu ya uwezo ya upandirisho. Na wakati wanavaa hii nguo wanasema : Roho yangu itashangilia katika Bwana, kwani amenifunika nguo ya wokovu na amenivika kanzu ya furaha. Amenivika taji kama Bwana-arusi, amenipamba kwa mapambo kama bibi-arusi ».

**Orario :**

Ni sawa kitambaa urefu na mwisho yake inaanguka mbele ya shemasi na mwisho yake ingine inaanguka mu nyuma. Inaandikwa pa hii kitambaa : Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu. Maana yake ni ya kama inaonyesha mabawa ya malaika kwa sababu ma shemasi weko wasaidizi ya wapadri wenye wanawatumia ya kusaidia watu weingine.

**Epimanika :**

Ni sawa minyororo na anaweka kila mpadri pa kila mukono yake juu ya kuchunga mikono mirefu ya Stikhario. Yanaonyesha nguvu takatifu ya Mungu na ya Vitu Vitakatifu, yenye yanajitoa ku mikono ya mpadri. Joo hivi, kama mpadri anavaa, anasema : «Mukono wako wa kuume, ee Bwana, umetukuzwa katika uwezo ; mukono wako wa kuuma, ee Bwana, umewavunja ma adui, na kwa sifa kuu ya utukufu wako, umewavunja washindani». Tena Epimanika yanatuonyesha na minyororo yenye walimufunga Yesu na walimupeleka kwa Pilato.

**Epitrakhilio :**

Ni sawa Orario, lakini mwisho yake yote ya bili yanaanguka mbele yake. Hii nguo wanavaa mpadri na askofu. Inaonyesha ile neema ya Roho Mtakatifu iliyeanguka toka juu pia. Kwa hivi, kama wanavaa hii, wanasema: «Mhimidiwa Mungu aliyemimiya neema yake juu ya mapadri, kama mafuta kichwani, iteremukayo nduvuni, ndevu ya Aroni na ishukayo mpaka upindo wa mavazi yake ». Ma nyushi yote ni chini ya kila Epitrakhilio yanatuonyesha ma nafsi ya waaminifu, yenye yanatundikwa toka singo ya mpadri, kwa sababu mpadri atajibu ile siku ya uhukumu mbele ya Kristu juu ya wokovu ya kila nafsi ya waaminifu wake. Bila Epitrakhilio mpadri hasiweze kufanya hata sala ao Ibada moja.

**Zoni (Musipi):**

Zoni anavaa mpadri na askofu juu ya kuchunga mavazi yake yote na inamukumbusha kazi kubwa yake mbele ya Mungu na ya watu. Maana yake ni ya kama kila mpadri inapaswa kukombanisha kila adui ya shetani katika sauti ya Bwana Yesu: «Muwe tayari kwa lolote litakalotokea, mukijifunga mavazi yenu viunoni na mukiwasha taa zenu » (Luka 12,35).

**Felonio:**

Ni nguo ya zamani, bila mikono na inaingia toka kichwa. Inaonyesha ile nguo ya Bwana Yesu Kristu, iliyekuwa bila mushono. Tena Felonio inaonyesha na Knisa ya Kristu pa hii dunia. Sawa nguo ya Kistu ilikuwa bila mushono, bila na kanisa ya kristu inafai kuwa MOJA. Tena felonio,katika sauti ya mt. Germanos, patriarshi ya Konstnaitnopoli, inaonyesha na ile nguo nyekunda walimuvaa Bwana Yesu, mbele ya kumusulubisha juu ya kumuchekelea. Vila na mpadri inapaswa kuangalia ya kama anavaa nguo ya uzarau na ya kuchekelea ya Kistu. Kwa hivi inapaswa kuvumilia kila matukano na uzarau ya watu ya dunia.

**Epigonatio :** Ni nguo nguvu kidogo na mpadri anaifunga ku musipi yake. Pa hii nguo inaonekana picha ya Karamu Kubwa ya Yesu Kristu ao Ufufuo wake. Hii nguo inatelemuka pa muguu ya kuume ya mpadri ao askofu. Anavaa kabisa wa askofu wote na wapadri, lakini hapana wote. Inaonyesha ile kitambaa Bwana Yesu alisafisha miguu ya Mitume mwake, mbele ya Karamu ya Siri. Tena inaonyesha na kisu kitakatifu juu ya kuzimisha mishale yote ya shetani, katika sauti ya Mtume Paulo: «Mushike imani siku zote kama ngao; ndiyo itakayowawezesha kuzima mishale yote yenye moto ya yule Mwovu. Pokeeni wokovu kama vile kofia ya chuma kichwani, na Neno la Mungu ndio upanga wa Roho » (Waefeso 6,16). Katika sauti ya mt. Symeoni, askofu ya Thessaloniki, hii nguo inaonyesha ushindi mbele ya lufu na Ufufuo ya Kristu. Kwa hivi, wakati wanaivaa wapadri, wanasema: Ewe shujaa, weka pajani upanga wako; ndio urembo wako na pambo lako...“ .

**Sakkos Arkieratikos.**

Hii nguo ilikombola Felonio ya wapadri tangu karne 18. Maana yake ni umoja na maana ya Felonio. Kengele kidogo-kidogo pempeni ya hii Sakkos yanatukumbusha kengele kumi na mbili ya Nabii na askofu ya Agano la Kale Aaroni. Na yanatuonyesha uwezo ya kuhubiri askofu.

**Ravdos Pimantiki (Bakora):**

Ni alama ya uwezo na mamlaka kitakatifu ya kila askofu. Juu yake hii bakora iko na musalaba katikati ya ma nyoka mbili. Hawa nyoka yanatuonyesha wa adui ya Kanisa ya Kristu, katika sauti ya Bwana Yesu: «Ninawatuma ninyi kama kondoo katikati ya imbwa wa pori» (Matayo 10,16),

**Omoforio :**

Ni kitambaa urefu na inafanya alama ya musalaba pa kilari ya askofu. Mwisho yake ni ku mbele na ingine ni mu nyuma. Inaonyesha ile kondoo aliyepotea porini na Bwana Yesu alimuletea pa ribeka yake. Mpaka somo ya Matendo ya Mitume askofu anavaa Omoforio kubwa. Kisha somo ya Evangelio anavaa Omoforio Kidogo. Omoforio kidogo iko na miguu (mwisho yake) yote mbili ku mbele pa kilari ya askofu. Maana ya jina hii ni : Nguo iliyewekwa pa mabeka.

**Arkhieratiki Mitra (Kofia) :**

Mwanzo yake inatokea toka Agano la Kale. Inaonyesha ile taji ya miiba walimuvaa Yesu Kristu, mbele ya kumusulubisha. Tena inaonyesha na mamlaka ya mufalme Bwana Yesu, kwani askofu ni mufano na pa fasi ya Kristu ndani ya Kanisa yake, hapa duniani. Ilionekana tangu karne ya 16.

**Arkieratiko Egolpio:**

Inatundikwa na monyororo muzuri toka singo ya askofu na inatelemuka pa kilari yake. Katikati yake ni picha ya Yesu Kristu. Hii Egolpio wanavaa paka wa askofu na iliingia daima, tangu ku mwaka 1856 na sheria ya serkali ya Grece. Inaonyesha chapa na usimamizi ya imani. Inafanana hii egolpio sawa riyayi na ndani yake ni Yesu Kristu ya kubariki na mukono ya kuume na pa mkono ya kushoto anakamata Evangelio.

**Dikirotrikira:**

Ni mishumaa mbili. Moja inaikaa na mishumaa tatu na ingine inaikaa na mishumaa mbili. Kwa hizi mishumaa askofu anabariki taifa ya Waaminifu. Hii mishumaa ya mbili yanaonyesha asili mbili ya Kristu, nikusema kimutu na kimungu. Mishumaa ya tatu yanatuonyesha ma Uso tatu ya Utatu Mtakatifu. Kwa hizi mishumaa tatu anabariki Evangelio kwa wimbo ya Trisagio : Mungu Mtakatifu, Mweza Mtakatifu… ».

## Sahani na vitu vingine ya Vitu Vitakatifu

**Kikombe Kitakatifu.** Ndani yake Padri anachunga Mwili na Damu ya Kristu. Inatuonyesha ile Kikombe aliichukua Bwana Yesu ile siku ya Karamu ya siri na alitoa Fumbo ya Eukaristia kwa Mitume wake (Ona Luka 22,20).

**Sahani Takatifu:** Ni sahani bila kuwa urefu. Juu yake mpadri anaweka, ile wakati anafanya Matayarisho ya Liturgia (Proskomidi), Kipande mtakatifu na kisha ya kushuka Roho Mtakatifu ndani ya Liturgia, hii Kipande ya Mukate inabadilishwa na inafanyika Mwili ya Kristu. Tena mpadri anaweka pa fasi ya kuume kipande ya Mzazi-Mungu na ya kushoto majeshi tisa ya

malaika. Tena Inaonyesha hii Sahani na ile sanduku pahali Mama Maria alimuweka ndani Yesu Kristu, wakati alimuzala.

**Lavida:** Namna ya kukomunika waaminifu tangu wakati ya Mitume ilikuwa ile namna sasa wapadri wote wanakomunyika. Lavida ni jina ya lupau kidogo na hii zoezo juu ya kukomunika waaminifu na lupau iliingia Kanisani ya Kristu tangu karne ya 10. Maana yake ni ukumbusho ya ile lupau malaika Waserafi waliweka kinywani ya Nabii Isaya makala ya moto.

**Asteriskos:** Mu lugha kiswahili inaitwa Nyota. Kisha mwisho ya matayarisho ya Proskomidi mpadri anafunika Sahani Takatifu na hii Nyota. Maana yake ni ukumbusho ya mbingu na ile nyota aliongoza wale wanaume tatu wa Persia, wenye hekima waliyokuja kwa kusujudu Mtoto Yesu Kristu.

**Kalimmata.** Ni vitambaa mbili na alama yao ni sawa musalaba juu ya kufunika mpadri Kikombe Kitakatifu na Sahani Takatifu, ile saa anamaliza matayarisho ya Liturgia (Proskomidi). Yanatuonyesha vitambaa haya manguo ile Mama Maria alifunga mwili ya mtoto mudogo mwake, wakati alimuzala.

**Aeras:** Ni kitambaa ingine na hii mapdri anafunika yote mbili Vitu Vitakatifu. Hii Kitamba mpadri, kama anatoka inje ya Altari Takatifu juu ya kujuguluka kati ya Liturgia pamoja na Vitu Vitakatifu, anaiweka pa ribeka yake. Inatukumbusha manguo ya Mtoto Yesu Kristu, wakati alizaliwa.

**Lokhi:** Ni kisu sawa mishale. Kwa hii kisu mpadri anakata Prosforo na anatosha vipande-vipande ya hii mukate (Prosforo) na anakumbuka ma jina ya Watakatifu na ya wafu. Kabisa na ku mwanzo anatosha Kipande ile ni katikati juu ya kuwa Mwili ya Yesu Kristu. Hii Lokhi inatukumbusha ile mukuki askari moja alimupingilia mbavu ya Yesu Kristu na mara moja ilitoka inje maji na damu ya kuachana.

**Musa:** Ni sifongo sawa muviringo na anaitimia hii mpadri juu ya kusafisha kabisa Antiminsio na Sahani Takatifu. Fasi yake ni ndani ya Antiminsio.

**Spogos**: Ni sifongo na inawekwa ndani ya Kikombe Kitakatifu, kisha ya kumaliza mpadri Liturgia kimungu, juu ya kutosha baridi ile inabaki ndani ya Kikombe. Inatukumbusha ile sifongo wa askari walimupatia siki kwa Yesu Kristu.

**Maktro**: Ni kitambaa na ragi nyekunda na inajitimia juu ya kusafisha na hii waaminifu kinywa yao, kisha ya kupewa Mwili na Damu ya Kristu. Kila mwaminifu inapaswa kuichunga hii chini ya ndevu yake na ataangalia juu hapana ya kuanguka hata kipande kidogo ya Mwili ya Yesu Kristu chini, kwani itakuwa zambi munene.

**Kengele Kidogo** : Ile saa mpadri anaanza Ibada ya Proskomidi, juu ya kukumbuka waaminifu ma jina ya wa ndugu wao wenye uzima na wenye kufa, anapika mpadri hii kengele juu ya kuwaambia ya kusali kwa wa ndugu wao.

**Artoforio**: Ni sanduku moja ya kiuma nzuri sana, pahali mpadri anachunga Takatifu Komonyo, Mwili na Damu ya Kristu. Huu Mwili mpadri anatosha kila mu kazi Ine mkubwa, nikusema ma siku tatu mbele ya Siku Kuu ya Ufufuo ya Bwana Ysu Kristu. Juu ya hapana kuharabika Mwili ya Kristu, mpadri inaikausha pa moto juu ya kuichunga mwaka muzima. Anaitimia mpadri kwa kukomunyika wagonjwa na wale weko karibu ya kifo ao, kama hawaweze kwenda kanisani.

**Musalaba Takatifu.** Ndani ya Kanisa tuko na musalaba ine:

1.Musalaba ile tunajugulusha ku mbele kama tunafanya Litani nikusema ya kujugulusha ma Picha ya Watakatifu.

2.Musalaba ya kutakasa maji ya baraka..

3.Musalaba, ile ni pa Meza Takatifu juu ya kubariki askofu waaminifu ya kanisa.

4.Musalaba mnene ile tunaitosha kila mu kazi Ine Mkubwa, kisha Evangelio ya Tano juu ya kukumbusha usulubisho na mateso ya Bwana wetu Yesu Kristu.

**Epitafios :**

Ni kitambaa nzuri na kubwa pahali ni ya kufatula Maiti takatifu ya Bwana Yesu Kristu, kisha ya kumushusha ku Musalaba wake. Kisha pempeni ya Maiti ya Kristu ni Picha ya Mzazi mwake Maria na wanafunji wake Yosefu, Nikodimo, Yoane na wanawake wabebaji manukato (Myrofori). Tena ni na malaika ya kusimama sawa ya kumuombeleza Kristu.

Hii Epitafio tunaiweka pa meza moja inayeitwa Kuvuklio na kisha tunaisujudu na tunaijugulusha mu Kazi Tano Mkubwa. Hii Kuvuklio, inatukumbusha ile Jiwe inayepokelea Mwili Takatifu ya Bwana Yesu Kristu.

**Chetezo :**

Ni sahani moja sawa muvirigo na inatelemuka ku minyororo ine na ndani mpadri anaweka makala na ubani juu ya kufukiza Meza Takatifu, ma Picha ya Watakatifu na taifa waaminifu. Minyororo hizi ya ine yanatukumbusha Waevangelizaji Ine na kengele yake kumi na mbili yanatuonyesha Mitume kumi na Mbili. Ile fasi chini tunaweka ubani inatukumbusha Mzazi-Mungu na makala ya moto ni sawa Bwana Yesu Kristu.

Ubani inatusaidia, ile saa ya kusali juu ya kupandisha akili yetu mbinguni juu ya kujingaa na neema ya Yesu Kristu. Sawa vile ubani inapanda juu pia na inajaa fasi yote kwa harufu nzuri, vile na roho ya kila mwaminifu kwa imani ya moto yake inapaswa kupanda mbinguni ya kuzarau matakio yote ya hii dunia. Hii harufu inatukumbusha harufu ya neema ya Roho Mtakatifu.

**Eksapteryga:**

Ni sawa muvirigo ya kiuma pahali ni nyuso ya malaika Wa Serafi. Yanatimiwa kwa Kuingia ya Kidogo na ya Kubwa na ya kujuguluka inje na pempeni ya Kanisa. Zamani kazi yao ilikuwa ya kufukuza ma shemasi kilulu yoyote mbali ya Kikombe Kitakatifu. Leo hii kazi inafanyika sawa ukubusho na ile kitambaa inayeitwa Aeras, wakati mpadri anaitenga juu ya Vitu Vitakatifu, ile saa waimbaji wanasoma Fundisho (Symvolo) ya Imani : (Nasadiki Mungu moja…).

**Lavaro:**

Ni pendera ya kanisa. Juu yake ni Picha ya Watakatifu fulani ao alama ya Musalaba ao ma picha ingine ya Siku Kuu ya Kristu na ya Mzazi-Mungu. Wanakamata watoto na wanatembea ku mbele kama ni kujuguluka inje na pempeni ya Kanisa.

**Kiropigia:**

Ni fasi pahali ma shemasi wanaweka mishumaa ya moto. Mbili Kiropigia ni pa Meza Takatifu na moja ni pempeni ya Meza ya Proskomidi (Matayarisho ya Liturgia). Waaminifu wanawaka mishumaa yao pa fasi ingine yanaitwa manualia na fasi yao ni ndani ao inje ya kila kanisa.

**Kengele :**

Kazi ya Kengele ni ya kuita waaminifu wakuje kanisani, ao ya kujuguluka Picha ya Mtakatifu, ao ya kupeleka maiti ya mufu moja kaburini yake. Ndani ya monasteri tunapata na vitu ingine ya kengele kidogo na yanaitwa Simandro, kopanos na talanto.

## Vitabu ya Kanisa

**Evangelio:**

Hii Kitabu inajiweka kati ya Meza Takatifu. Pa fasi moja ni Usulubisho ya Kristu na pa fasi ingine Ufufuo yake. Tangu Ibada ya Magaribi ya Posho mpaka kesho magaribi, ile saa tunasoma Saa ya Tisa mbele ya ibada ya magaribi ya mukazi moja, inaonekana Ufufuo ya Kristu. Ile saa asubui ya siku ya Juma waaminifu wanabusu Evangelio, wanabusu Ufufuo yake. Ma siku ingine ya juma muzima inaonekana pa Meza ile fasi ya Usulubisho Yake.

Evangelio inagawanya kwa vipande mbili. Mu kipande ya kwanza ni Evangelia yote toka Siku Kuu ya Pasaka mpaka Pentikosti tunasoma Evangelia toka Mwevangelizaji Yoane. Kutoka Pentikosti mpaka siku Kuu ya Kupanda Musalaba (14 ya septemba) tunasoma Evangelia katika Matayo. Kutoka hii Siku Kuu ya Musalaba mpaka mwanzo ya Kwarezima, tunasoma Evangelia toka Luka. Ku mwisho ya hii kipande ya kwanza ni Evangelia kumi na mbili, yenye yanaitwa Eothina, kwa sababu yanasomwa kila mu Juma, mu Ibada ya asubui ya siku ya Mungu.

Kipande ya mbili ya Evangelio inakamata Evangelia ya ma shangilio ya Watakatifu wakubwa ya mwaka muzima katika desturi ya kila mwezi kutoka mwanzo ya Septemba mpaka 31 ya mwezi ya Augusti. Ku mwisho ya hii Kipande ya mbili ni Evangelia ya ma Ibada ya mbali-mbali sawa ya Kiliyo, ya ndoa ya Ubatizo ya wafu na ingine ingine.

**Apostolos (Matendo ya Mitume):**

Ni kitabu ya musomaji. Iko na vitabu vitabu ya somo ya Matendo ya Mitume na toka ma barua ya Mitume na yanasomwa kila siku ya mwaka muzima. Desturi ya kila somo ya hii kitabu inafwata kalendari ya kila mwaka muzima mupya.

**Mega Efkologio:**

Hii kitabu wanaitimia wapadri na wa askofu. Iko na ma Ibada ya mafumbo yoyote, desturi ya Upandirisho na ya kila Ibada ya Kanisa ya Kristu.

Mega Orologio (Saa Kubwa) :

Ni Kitabu ya Waaminifu wote na ya wapadri wote. Ndani yake tunapata ma Ibada yote ya siku na usiku, Apolitikia na Kontakia ya kila Mtakaitfu kila siku ya mwaka muzima na kidogo fundisho ya uzima yao. Tena ni Wimbo ya Mzazi-Mungu, Ibada kusoma kila mwaminifu mbele ya Komonyo Takatifu na mafundisho ingine ya muzuri sana.

**Minea:**

Ni vitabu Kumi na mbili, moja-moja ya kila mwezi na weko na ma Ibada ya Watakatifu ya kila siku. Nikusema kila ibada iko na sala ya Magaribi na sala ya Asubuyi. Juu ya Watakatifu wapya tuko na ma Ibada mapya, bila kuwa ndani ya Minea.

**Paraklitiki:**

Hii kitabu iko na ma Ibada ya ma sauti mnane. Tunaimba kila sauti ya kila juma. Pempeni ya ma Ibada ya Minea tunaimba na hizi ma Ibada ya Paraklitiki.Wimbo hizi yanatukuza Ufufuo ya Bwana Yesu, kila siku ya kwanza moja majeshi ya Malaika, kila siku ya mbili wimbo ya Yoane Mtangulizi na Mubatizaji, kila siku ya Tatu wimbo ya Mzazi-Mungu, kila siku ya Ine wimbo ya Mitume kumi na mbili, kila siku ya Tano wimbo ya Usulubisho na Musalaba ya Yesu Kristu na kila mu Posho wimbo ya Mashahidi na ukumbusho ya wafu.

### Triodio:

Hii Kitabu tunaisoma ile wakati iko na jina umoja, ao wakati ya Kwarezima, ma siku makumi saba mbele ya ufufuo wa Kristu. Inaitwa Triodi (Ode tatu) kwa sababu tunaimba ao tunasoma wimbo (Ode) tatu kila siku hile wakati.

**Pentikostari:**

Hii Kitabu iko na wimbo na ma Ibada kila Pasaka mpaka ile siku ya Pentikosti, nikusema ya kushuka Roho Mtakatifu pa vichwa ya Mitume wa Kristu.

**Psaltirio (Kitabu ya zaburi ya Daudi):**

Hii kitabu iko na ma Zaburi 150 na ma zaburi yote ni ndani ya ma sehemu (Kathisma) 20. Lakini Kathisma ya kumi na saba iko na paka Zaburi moja, ya 119.

Kwa monasteri yetu watawa wanasoma hii kitabu mara moja kila juma ndani ya kanisa.

**Synaksaristis:**

Hii ni mustari ya vitabu kumi na tano. Kila Kitabu inaandika uzima ya Watakatifu. Vitabu ingine ni ya Triodi, Juma Takatifu na Pentikostari na yanaandika mahubiri ya kila siku Kuu.

Waaminifu wingi wanasoma hii mustari ya vitabu na furaha kubwa, kwa sababu wanajifunja uzima ya Watakatifu. Pamoja na Evangelio vitabu hizi ni sawa rikalasi ya kila Mukristu.

# SEHEMU YA MBILI
## MA FUMBO NA MA IBADA YA KANISA YETU

### Ufafanusho kidogo ya Liturgia Takatifu

Ndani ya fumbo ya Liturgia kimungu inamalizwa tendo kubwa ya wokovu wetu. Katika neema ya Roho Mtakatifu tunapewa Mwili na Damu ya Bwana Yesu Kristu na kwa kukomunyika Mwili Yake tunapata hivi uzima ya milele, uzima isiyoharabika na uzima takatifu.

Tena mara moja Liturgia ni ukumbusho ya kazi yoyote ya Bwana wetu tangu ile siku alikuja duniani mpaka ile siku alipanda mbinguni. Desturi ya Liturgia ni sawa ya kutuonyesha mbele ya ma macho yetu uzima yote ya Yesu Kristu. Hii tendo inafanyika kwa wimbo na somo, yenye yanaongoza mwaminifu moja mu zima ya kiroho na yanamutayarisha kwa kupewa Vitu

Vitakatifu. Tena vile vitu ya kuonekana na isiyoonekana yanatuongoza mu uzima ya mbingu na vile matendo yasioonekana mbinguni. Nikusema yanaonyeshwa vile vitu visiyoonekana na vitu vilivyoonekana, sawa kwa mufano mu Fumbo ya Ubatizo maji inaonyesha nguvu ya Roho Mtakatifu inayesafisha uzima na roho ya mutu.

Kitu ingine kubwa ni ya kama ndani ya Liturgia kimungu tunasikia ujio ya Bwana wetu Yesu Kristu, sawa vile na Mtume Luka anasema: “Fanyeni hivi kwa kunikumbuka”.(Luka 22,19).

## PROSKOMIDI (Matayarisho)

Proskomidi inaitwa ile Ibada inayefanyika ile saa inajisoma ibada ya asubuyi. Ile saa yanatayarishwa vitu Vitakatifu (Mukate na vinyo) juu ya kutimiza Ibada ya Liturgia Kimungu.

Hii Ibada inafanyika pa fasi ya kushoto ya Altari Takatifu, karibu na mbele ya mulango ya kaskazini. Hii meza pahali inafanyika hii Ibada inaitwa Prothesis. Hii Ibada inaonyesha Uzalio ya Yesu Kristu, mpaka kuondoka kwake kwa kuhubiri na sandaka Yake mpaka mulima ya Kalvario. Kwa hivi ndani ya ile fasi inajifatula picha ya Kuzaliwa kwake ao Uso yake katika unyenyekevu. Hii Meza ya Prothesis inaonyesha pango na sanduku pahali alizaliwa Yesu Kristu, tena inaonyesha na Kalvario, pahali alisulubiwa Kristu. Hii mukate ineyefanyika kisha Mwili ya Kristu inaitwa prosforo, nikusema kitoleo, kwani sisi tunatoa hii mukate na vinyo sawa shukrani yetu na ombi kwa Mungu, aliyetupatia uzima yetu. Kwa hivi Liturgia ni matoleo ya mutu kwa Mungu na matoleo ya Mungu kwa mutu. Hii Prosfora iko na alama sawa muvirigo, kwa sababu inaonyesha ya kama Mungu ni bila mwanzo na mwisho na inatuonyesha Mzazi-Mungu. Inatuonyesjha mwendo ya Mzazi-Mungu mujini Bethlehemu juu ya mandiko.

Kikombe Kitakatifu inatuonyesha sandaka ya Kristu pa Musalaba na kilauri ya lufu Yake, ile aliikunywa Kristu kwa kutuokoa toka zambi. Na huu Kilauri kisha usulubisho ya Kristu ilifanyika kilauri ya baraka na ya wokovu ya mtu.

Sahani takatifu (mu lugha kigreki inaitwa Diskario) ni sawa muvirigo na inatukumbusha sanduku na kitanda pahali alisimama Mtoto Yesu Kristu.

Nyota inatuonyesha usabitisho ya mbingu na ile nyota inayeongoza wale wenye hekima tatu toka Persia ya kumusujudu Yesu Kristu.

Vitambaa yanatuonyesha manguo ya Mtoto Yesu Kristu, kama Diskario inaonyesha Sanduku pahali alilala MtotoYesu na ni sawa ma sanda kama Diskario inaonyesha kitanda ya lufu ya Yesu Kristu.

Ubani ya hii Ibada inatuonyesha ma zawadi ya wale wenye hekima watu tatu wenye walitokea ku Persia ya kumusujudu Yesu.

Tendo ya kwanza ya mpadri kama ataanza kutayarisha hii Proskomidi ni ya kunyanyua Prosfora. Hii kazi yake inatuonyesha ya kupanda Yesu Kristu Musalabani na hii prosforo inatuonyesha upendo ya Kristu kwa sisi wote.

Kisha Padiri anatosha ile mukate itakuwa Mwili ya Kristu na inaitwa Amnos, nikusema Mwana kondoo. Inaikata kwa alama ya musalaba na kisu moja ni sawa mishale mukusema ma sauti ya Wanabii, wenye walisemaka juu ya Mateso ya Kristu. Manabii haya yanatuonyesha ya kama Yesu Kristu alikuja duniani juu ya kusulubiwa. Na Nabii Symeoni, aliyepokelea Yesu alisema: “Na wewe, mwanamuke, uchungu utakuchoma moyo kama upanga”, nikusema Mama mwake atapata huzuni ya roho yake, wakati atamuona mwana mwake pa Musalaba. Yesu Kristu ile saa ya Lufu Yake anapatia Kanisani yake uzima, kwa sababu ilitokea ya mbavu yake damu na maji, na hii jambo ya ajabu inatuonyesha ma Fumbo mbili: Ubatizo na Komonyo Takatifu.

Kisha mpadri anatosha Kipande kimoja kwa jina ya Mzazi-Mungu na anaiweka pa fasi ya kuhume ya ile Kipande (Amnos) ya Kristu na anamuomba juu ya kupokelea sala yake kwa fasi ya sandaka mbinguni. Kisha anatosha vipande Tisa kwa jina ya Majeshi Tisa ya Watakatifu, Malaika, Wanabii, Mitume, Waaskofu, Mashahidi, Watawa, Wa Anargiri, Wababu ya Mzazi Mungu pamoja na huyu Mtakatifu ya hii siku na jina ya mtakatifu ule anasoma Liturgia yake mpadri. Kwa hivi ya kutoa hii sandaka padri yanaunganishwa watu na Watakatifu wote pamoja na Mama Maria na Yesu Kristu, katika sauti ya Kristu anayesema: “Kama mutu akitaka kunitumikia, anapaswa kunifuata, na pahali nilipo mutumishi wangu atakuwa vilevile” (Yoane 12,26).

Kisha mpadri anatosha vipande-vipande ya makombo na anakumbuka ma jina ya wenye uzima sawa anakumbuka askofu yake na ma jina ya wale waaaminifu wanatoa hii Prosfora na vinyo na ma jina ya wakristu weingine. Kisha anakumbuka kusoma ma jina ya wafu na hivi na hawa wafu wanachukua baraka ya Mungu katika mapenzi yake.

Kwa hivi pa Sahani (Diskario) Takatifu ni Kanisa muzima. Kanisa ya mbingu na ya hii dunia na kati yao ni Bwana Yesu. Neema ya Roho Mtakatifu inasaidia kila mutu katika mapenzi na mufano ya roho yake.

Pa hii fasi inatimiza mpadri matayarisho ya Proskomidi. Kisha anafunika na vitambaa Vitu Vitakatifu na mara moja anafuta na chetezo.

Tunatayarishwa sisi ya kuingia ndani ya Liturgia kimungu. Shemasi anasema kwa mpadri: Ni muda ya kutumika Bwana…”. Nikusema wapadri wanamuacha akuje kati yao Bwana Yesu juu ya kupokelea hii prosfora na matayarisho yao juu ya kufanya Liturgia Yake. Liturgia nikusema ni “wakati” ya upendo ya Kristu.

**VIPANDE MBILI YA LITURGIA KIMUNGU**

Kipande ya kwanza inaitwa Liturgia ya neno ao ya Wakatikumeno. Inaitwa hivi kwani tunasoma maombi, masomo na tunaimba wimbo. Ndani ya hii kipande wanaweza kusimama na Wakatikumeni. Kipande ya Mbili ni ile fasi inamalizwa Fumbo Takatifu ya Komonyo na Eukaristia. Inaitwa Eukaristia kwa sababu ni matoleo ya zawadi yetu, utakaso na Ushirika ya Mwili na Damu ya Kristu.

## Liturgia ya neno ao ya Wakatikumeno

Mwanzo: Liturgia inaanza na utukufu ya Utatu Mutakatifu. Ubarikiwa ni Ufalme wa Baba na wa Mwana na wa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote…”.Ile saa mpadri anasema hivi anakamata Evangelio pa mikono yake anafanya na Hii alama ya Musalaba pa Meza Takatifu. Neno ya kwanza ya Liturgia Kimungu ni baraka na utukufu ya Ufalme ya Mungu na tendo ya kwanza ya Liturgia ni alama ya Musalaba.

Basi, Liturgia ni Ufalme ya Mungu na Musalaba na njia na mulango ya paradizo. Ni tangazo ya Ufalme ya mbingu.

Waimbaji wanajibu : Amina, nikusema : kweli, tunatakia ya kutimizwa hivi. Liturgia ni kazi ya taifa yote ya waaminifu. Mpadri na waaminifu wanatumika pamoja na wanapata pamoja ma zawadi ya Ufalme ya mbingu.

**Sinapti (kundi ya maombi) Kubwa:**

Kwa sababu ndani ya Liturgia hatufanye paka ukumbusho ya Sandaka na Karamu ya Bwana, lakini na ombi mbele Yake juu ya kila kitu sisi tunalazimishwa, ao kitu ya kimwili ao ya kiroho. Kwa hivi mpadri anaanza kuomba ku mwanzo amani na anasema : Kwa amani tumwombe Bwana. Ile njia inatuongoza kwa kufata sisi nzuri Liturgia kimungu ni amani ya roho yetu. Amani ya Evangelio ni hali ya roho. Ni hali ya utulivu, kama roho ya mwaminifu iko na urafiki na ushirika na Mungu. Hii amani ilikuja duniani na ilisambaha pa dunia nzima, kisha sikilizano ya inchi na mbingu, iliyefanyika katika Musalaba na kwa unyenyekevu ya Bwana wetu Yesu Kristu. Mwaminifu moja anayefata ma Ibada na ma Fumbo Takatifu ya Kanisa, anapata ndani ya roho yake hii amani ya kiroho. Hii amani inajitoa toka Bwana wetu tangu kuzaliwa kwake. Tangu ile siku ilisikilikwa hii sauti ya utukufu: Utukufu kwa Mungu juu pia na amani pa inchi...“.

Kwa maombi ya tatu tunaona ya kama mtu anaomba amani na upendo. Kisha mpadri anaomba juu ya waaminifu na wapadri ya Kanisa ya Kristu, kisha anaomba juu ya muji na kila mui na inchi na anaomba juu ya kutuma Mungu baraka kubwa ya ma shamba ya watu wote ya dunia. Kisha mpadri anaomba juu ya wa ndugu wetu wagonjwa kwa kuwaponyesha Mungu na kuwapatia baraka ya kimwili na kiroho yoyote, bila kusahau ya kama tunapaswa kupitisha kati ya ma taabu mpaka kufika kwa ufalme ya mbingu. Tena mpadri anaomba juu sisi wote tujitoa maugu yetu na wa ndugu wetu na uzima yetu nzima pa mikono ya Kristu katika saidio ya Malkia wetu Mzazi mwake na ya Watakatifu wote, kwa sababu Kwake inafai utukufu, sifa na usujudu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu sasa na siku zote hata milele na milele. Amina.

**Antifono ya kwanza.**

Kisha maombi ya Sinapti Kubwa, waimbaji wanafanana sawa Wanabii, wenye wanatupeleka mu wakati mbele ya kufika Yesu Kristu duniani na wanaimba ma shairi ao wimbo ya Nabii Daudi, yenye yanatuwaambia ujio ya Bwana Yesu Kristu.

Kisha ma shairi ya hii Antifono inajifwata ombi tatu kwa jina ya Mzazi Mungu, hivi: Kwa maombi ya Muzazi Mungu, ee Mwokozi utuokoe“.

**Antifono ya pili.**

Kisha Antifono ya kwanza inafwata Sinapti kidogo na ombi moja ya mpadri. Kisha waimbaji wanasoma ma shairi tatu toka zaburi 146 na kisha inafwata : « Utuokoe, ee Mwana wa Mungu, aliyefufuka katika wafu, tunaokuimbia. Aliluia ». Lakini ya kila siku, ila tu mu juma, tunasema : Utuokoe…uliye Watakatifu wa ajabu… ».

**Antifono ya tatu.**

Katika Antifono ya kwanza na ya pili mwaminifu anajipeleka toka wakati ya Kristu mu wakati ya Mt. Yoane Mubatizaji, pahali alionekana Bwana Yesu aliyemuonyesha huyu Nabii mt. Yoane. Kwa hii Antifono ya tatu aliisha kuja Kristu na alifanya kuhubiri yake Mulimani. Kwa hivi na waimbaji wanaimba Apolitikio ya Ufufuo ya Kristu ya Mutakatifu ya ile siku kwa sababu ni onyesho moja kubwa ya Ufufuo ya Kristu. Kama tunashangilia Mutakatifu moja, kwa uso yake inaonekana Ufufuo ya Kristu, kwani ni Mutakatifu ya ufufuo, kwa ajili ya neema kimungu yake, katika sauti ile anasema Mtume Paulo: «Si kama mimi ninaishi peke yangu, lakini ni Kristo anayeishi ndani yangu » (Wagalatia 2,20).

**Kuingia Kidogo.**

Ku mwisho ya Antifono ya tatu inafanyika Kuingia Kidogo ao Kuingia pamoja na Evangelio. Hii Kuingia inatukumbusha ujio ya Kristu ndani ya dunia na kuhubiri yake pempeni ya Yerusalema, sawa Huyu alisema: “Imetupasa kwenda katika vivjiji vingine vilivyo karibu, kusudi nihubiri kule vilevile” (Marko 1,38). Huyu mtoto anayetembea na mushumaa moja pa mkono yake ni taa ya Nuru. Huyu Taa ni Mt. Yoane Mutangulizi, anayepaza sauti: «Tazama Kondoo wa Mungu.. » (Yoane 1,30, 36). Kati ya Kanisa mpadri anasema sala ya Kuingia, anabariki Mulango Bora, ananyanyua Evangelio ya kuonyesha hivi ushindi ya imani: “Tunashinda dunia kwa njia ya imani yetu” (Barua ya kwanza ya Yoane 5,4) na anapaza sauti sawa ule malaika aliyetangaza Uzalio ya Kristu kwa wachungaji: “Hekima. Simameni, nikusema Huu ni Evangelio na iko fundisho ukweli wa pekee na hekima ya kweli. Ni sawa kuelejea: “Musiogope, kwa sababu ninawaletea ninyi Habari Njema ya furaha kubwa itakayokuwa kwa watu wote” (Luka 2,10). Kufatana na ile sala ya Kuingia mpadri anaomba kufanyika hii Kuingia ya Wamalaika Watakatifu. Waaminifu wanasimama kwa heshima na ya kuonyesha usujudu na ya kuishi muujiza ya onekano ya malaika, katika sauti ya Luka: “Mara moja kundi kubwa la malaika wa mbingu wakawa pamoja na yule malaika wakimusifu Mungu…” (Luka 2,13). Na sisi wote, waimbaji na waaminifu tunaimba hivi: “Kujeni kumusujudu na kumuangukia Kristu; Utuokoe ee Mwana wa Mungu…”.

**Apolitikia (Wimbo ya Watakatifu).**

Mara moja tunaimba Apolitikia, yenye yanatukuza Matendo mazuri ya Yesu Kristu ao uzima ya Watakatifu ya hii siku. Ku mwanzo tunaimba Apolitikion ya Ufufuo ya Kristu, kisha ya Mtakatifu ya hii siku na ya Mtakatifu ya Kanisa. Kama tunafanya na ukumbusho ya wafu, tunaimba na Kontakio ya Wafu. Ku mwisho tunaimba Kontakio ya Siku Kuu ya ile wakati.

Ile saa waimbaji wanaimba Apolitikia, mpadri ndani anasoma sala ya Mwimbo ya Trisagio (Nikusema hii: Mungu Mtakatifu, Mweza Mtakatifu, musiye kufa Mtakatifu, utuhurumie). Mwisho atasema: Kwa kuwa Wewe ni Mtakatifu… Kwa hii sala mpadri anaomba toka Mungu ya kuhurumia kila zambi katika mapenzi na isiyo na mapenzi yetu na kisha atastahilisha waaminifu wote ya kuimba Mwimbo ya Trisagio;

**Mwimbo ya Trisayo.**

Kisha ya kuimba Apolitikia ya Watakatifu, waaminifu na malaika pamoja wataimba Mwimbo ya Trisagio: “Mungu Mutakatifu, Mweza mutakatifu, musiye kufa Mutakatifu, utuhurumie”. Hii Trisayo ilitokea toka Nabii Isaya, wakati aliangalia malaika ya kumuhimidi Mungu hivi: Mutakatifu, Mutakatifu, Mutakatifu (Isaya 6,3) na toka Kitabu ya Zaburi ya Daudi. Hii Mwimbo inatukuza Utatu Mutakatifu. Kwa hivi inaunganisha Agano la Kale na Agano Jipya. Tena Malaika na Waaminifu ni Kanisa na Kundi moja na wote wanamutukuza Mungu. Mutu mwenye zambi anastahiliwa kuimba Mungu pamoja na majeshi ya Malaika. Mbingu na inchi, viumbe ya kuonekana na visivyoonekana yanasanyikwa ya kufurahi kwa kumutukuza Mungu.

Mpadri, wakati waimbaji wanaimba hii Trisayo, anaenda kwa Prothesis, inayeonyesha Pango ya Betelehemu, anamutukuza sawa na Wamalaika Bwana, anayekuja duniani mukusema: Mubarikiwa anayekuja kwa jina la Bwana. Sisi tunamutoa neno vema ya kumutukuza na Yeye anatupatia Maugu yake.

**Apostolos (Somo ya Matendo ya Mitume)-Evangelio.**

Yesu Krisu anaonekana pole-pole. Kwa Kuingia alionekana Kristu na Evangelio ilikuwa ya kufungwa. Hii inatuonyesha ujio yake ya siri. Hivi aliendа na unyamasha kwa Mt. Yoane Mbatizaji ya kubatizwa. Kisha anaonekana kwa matendo na mahubiri ya Mitume na ku mwisho anaonekana huyu mumoja ndani ya somo ya Evangelio.

Mbele ya kusoma Apostolos mwimbaji, atasoma ma shairi tatu toka Agano la Kale, yenye yanaelejea matendo ya ajabu ya Mungu na yanatutayarisha ya kusikia sisi neno ya Kristu. Kisha ya kusoma Apostolos, waaminifu wanaonyesha furaha yao ya kuimba hii : Alliluya mara tatu, maana yake ni : «Musifuni Mungu».

Mpadri, mbele ya kusoma Evangelio Takatifu, anaomba juu Mungu kumuangazia akili ya waaminifu yote kwa kusikia mafundisho ya Evangelio yake. Vile anasoma : « Ee Rabi Mpenda-wanadamum wangaze mioyoni mwetu na nuru isiyokufa ya kujua umungu wako, tena fungua macho ya akili yetu ili tusikie mahubiri ya Evangelio yako…”. Kisha anafukiza na chetezo Altari takatifu, ma Picha na taifa yote.

Ile wakati mpadri alifanya Kuingia Kidogo, kwa kutembea alifunika nyuso yake juu ya kuonekana Nyuso ua Bwana Yesu Kristu pa Picha yake ya Evangelio. Sasa eko tayari ya kusoma Evangelio Takatifu. Anasimama ya kusoma na anapatia sawa deni kinywa yake kwa Bwana Yesu juu ya kusikia waaminifu sauti ya Yesu Kristu.

Hekima. Simameni. Tusikilize Evangelio Takatifu. Nikusema: Musimame ya kusikia hekima ukweli na ya pekee. Inapaswa ya kusimama neno ya Mungu, kwani akili ya kila mtu inapaswa kuwaza vitu vya mbingu na kupanda juu pia ya vitu vya hii dunia kwa kusikia maana ya sauti ya Mungu. Nikusema haipaswe kutubaba uvivu, lakini tutakuwa ya kusimama kwa kusikia neno Lake na tutajaribu kumufukuza adui ya roho zetu, shetani muovu, anayesimama karibu yetu juu ya kutukamata.

Kwa hivi, tutasimama na katika amani, sawa vile na mpadri anatubariki, tunapaswa kusikia Evangelio juu ya kuchukua neema ya Roho Mtakatifu na baraka ya Kristu. Na kweli, kisha somo ya Evangelio, baraka moja kubwa inaingia ndani ya roho yetu. Akili yetu inaikaa na amani, roho yetu unatulivu na Liturgia Kimungu inatuongoza kwa kusikia Fumbo takatifu ya Upendo kimungu ya wokovu wetu. Nikusema, Mungu alishuka duniani juu ya kuokoa mutu, kila mutu kwa ajili ya upendo yake!

## Maombi Ektenis- sala ya Wakatikumeni.

Kipande ya kwanza ya Liturgia inamaliza kwa hii maombi kubwa na maombi juu ya Wakatikumeni. Mara moja kila somo ya Evengelio, inapaswa kufwata kuhubiri na ufafanusho yake.

Maombi kubwa (Ektenis) ni mustari moja ya maombi, pahali tunaomba rehema ya Kristu, kwa sababu Huyu alikuja kwa inchi yetu juu ya kutuhurumia. Na hii ujio Yake huku duniani inaitwa Huruma, nikusema Yesu Kristu, aliangalia hii hali mbaya sisi wote tulikuwa na

hasikutuzarau. Alisikia ma kosa na magumu ya roho zetu, alikuja kwetu na alitufufua na alitustahilisha kuingia mu Ufalme mwake. Kisha ya kila ombi ya mpadri, waimbaji wanajibu: Bwana hurumia (mara tatu). Kama mukristu moja anaomba hurumia ya Mungu, anaomba nikusema Ufalme Wake, ile Kristu alilaka ya kama ataipatia kwa wale wanaitafuta. Tena alisema ya kama na vitu vyote vya hii uzima Yeye atatupatia, katika sauti yake: „Basi, tafuteni kwanza ufalme wa Mungu na haki yake, naye atawaongezea vitu hivi vyote“ (Matayo 6,33). Yesu Kristu ni bahari, bila mupaka, ya huruma na tunakimbilia kwake katika kitumaini ya kama tutapata huruma na ukombozi.

### Maombi ya Wakatikumeni.

Kanisa sasa inatuma kwa Mungu wetu maombi juu ya Wakatikumeni, wenye watabakia mpaka sasa, kisha sikilizo ya Matendo ya Mitume, Evangelio na kuhubiri. Kisha inaisha sala ya Wakatikumeni na Kanisa inawalejea ya kutoka inje, kwa sababu kisha itaanza sala ya Waaminifu. Wakatikumeni bado kubeba baraka juu ya kupewa Mwili na Damu ya Kristu. Ni sawa watoto wadogo (bebe) ndani ya tumbo ya mama-Kanisa yetu. Wanakomea pole-pole juu ya kuwa stahili siku moja kuingia Kanisani katika Ubatizo Takatifu.

## Liturgia ya Waaminifu

Kisha ondoko ya Wakatikumeni mpadri anaendelea maombi yake juu ya Waaminifu. „Sisi tulio Waaminifu, tena na tena kwa amani tumwombe Bwana“. Ile saa mpadri atafungua Antiminsio pa Meza Takatifu. Sasa Meza pamoja na Antiminsio ni sawa Kaburi ya Bwana Yesu Kristu.

Mpadri anasoma maombi mbili ya Waaminifu. Kwa ombi ya kwanza mpadri anamushukuru Mungu, kwani alimustahilisha kusimama mbele ya Mazababu Yake Takatifu na anamuomba juu ya kumuita katika Jina Lake Takatifu kamili. Juu ya kusali mpadri inapaswa kuwa musafi kabisa. Roho yake inapaswa kuwa kupita safi ya mwangaza ya jua.

Katika sala ya mbili, mpadri anamuita kila mwaminifu juu ya kupifa magoti mbele ya Kristu juu ya kuomba endeleo ya uzima ya kiroho, kuongeza imani na akili ya kujua ma njia ya wokovu. Kwa hii sala tunasikia ya kama, mtu moja anaweza kuchukua neema Yake, kama anaishi ndani ya unyenyekevu, nikusema kama anawaza, anasema, anatembea na anatimiza kila kazi yake katika mawazo ya unyenyekevu. Kwa hivi na sisi tunamuomba Mungu ya kutusafisha toka kila uchafu katika kiroho na mwili yetu...“.

### Mwimbo ya Kheruviko.

Kisha somo ya sala ya mbili, wanaanza waimbaji kuimba mwimbo ya Kheruvikon: „Sisi tunaofanana kwa siri na Wakheruvi na tunaoimbia Utatu Mpaji-Uzima, wimbo watakatifu tatu, tuache sasa shuruli zote za dunia hii“. Hii mwimbo unashauri kila mwaminifu ya kutosha mbali ya akili na roho yake kila shuruli ya hii dunia kwa kumupokelea Huyu anayekuja Mufalme. (sasa mpadri anapeleka paka mukate na vinyo, kwani bado kufanyika Fumbo takatifu ya kubadilisha vile vitu kwa Mwili na Damu ya Kristu). Hii Mwimbo ya Kheruvikon inatukumbusha ya kama sisi tuko kundi moja ya malaika na watu. Hii Mwimbo inatukumbusha Kuingia katika utukufu ya Bwana Yesu ndani ya muji Yerusalema, mbele ya Mateso Yake. Tena inatukumbusha na kupeleka MaitiYake Kaburini juu ya Maziko Takatifu Yake.

Tangu ile dakika waimbaji wataanza kuimba Kheruvikon, mpadri atasoma sala hii: „Mtu hata mmoja wa wale wenye kufungwa kwa tamaa na furaha za mwili anayestahili kuja Kwako, kukujongea na kukuabudu, ee Mufalme wa utukufu...“. Kisha atasema mara tatu hii mwimbo ya Kheruvikon na atafukiza na chetezo kusema hii (kama ni siku ya Mungu): „Tukiona ufufuo wa Kristu, tumsujudu Yesu Bwana Mtakatifu aliye peke yake bila zambi. Tunausujudu msalaba wako, ee Kristu, tena tunausifu na kuutukuza ufufuo wako takatifu....“. (Kama haiko siku ya Mungu na siku ingine ya juma, atasema: „ Njooni tumwinamie na tumsujudu Mungu na Mfalme wetu. Njooni tumwinamie na tumsujudu Kristu na Mungu Mfalme wetu. Njooni tumwinamie na tumsujudu Yeye Kristu aliye Mfalme na Mungu wetu. Na kisha Zaburi 50 (51). Unirehemu, ee Mungu, sawasawa na

wema wako; sawasawa na wingi wa rehema zako uzime makosa yangu. Unioshe kabisa na uovu wangu, na kunisafisha na zambi yangu. Maana ninajua…..". Kisha mpadri anapiga magoti kusujudu mara tatu Meza Takatifu, anabusu Antiminsio. Kisha anaomba hurumia toka wapadri na mashemasi yote. Kisha anasimama mbele ya waaminifu na anaomba hurumia. Kisha anabusu mara tatu Vitu Vitakatifu (Kikombe na Sahani Takatifu) yenye ni pa Meza ya Proskomidi. Mpadri anatumika sasa sawa wale Mitume na Mirofori wenye walimuzika Maiti ya Yesu Kristu. Tena anaonyesha hali ya toba ya roho yake. Vile anataka kutuonyesha ya kama na sisi tunapaswa kutayarisha roho yetu katika toba na woga ya Mungu. Kisha mpadri anaweka Kitambaa, inayeitwa Aeras pa ribeka yake na hii inakumbuka jiwe ile ilijiweka pa Kaburi ya Yesu.

## Kuingia Kubwa.

Kwa Kuingia hii kubwa, mpadri anafunika nyuso yake na Vitu Vitakatifu kusema: Bwana Mungu, utukumbuke sisi wote katika ufalme wako…". Kondoo wa Mungu Yesu Kristu anakuja kwa sandaka. Anaingia ndani ya Yerusalema, anajitoa pa mulima Kalvario, anajiweka Kaburini kwa mikono ya Mitume Yosefu na Nikodimo, nikusema anajiweka pa Meza Takatifu na pa Sahani Kimungu. Ubani (uvumba) mbele ya Kuingia Kubwa inatuonyesha manemane na manukato ya Nikodimo, aliyepakaa Mwili ya Yesu Kristu. Tena, wakati mpadri ataweka Vitu Vitakaitfu pa Meza, atayafukiza na uvumba na hii inatuonyesha manukato ya harufu ya wanawake wababaji, manukato.

Kisha mpadri atapaza sauti kusali juu ya uzima na magumu ya waaminifu, kama wataondoka ku mwisho inje ya kanisa. Nikusema anaomba kwa Mungu kwa kutuma malaika mulinzi ya nafsi ya waaminifu wote, maondoleo ya zambi zao, ya kutafuta kabisa vile vite yatawasaidia mu uzima yao ya kiroho na juu ya kuwa miaka yao ya mwisho katika imani na woga ya Mungu.

## Symvolo (Fundisho) ya Imani

Ile saa tunaonyesha mapendo yetu mbele ya wa ndugu weingine mukusema: "tupendane sisi kwa sisi, ili kwa nia moja tuungame. Tena na mpadri atasema mbele ya Mungu: „Nitakupenda, ee Bwana, nguvu yangu; Bwama ni imara yangu msaada wangu, kimbilio changu na Mwokozi wangu". Kisha sisi wote tunaungama Imani yetu mbele ya Utatu Mutakatifu. Mbele ya kuungana wapadri ndani ya Altari wanabatiana katikati yao juu ya kuonyesha ya kama katika upendo na amani watasema Imani ya Utatu Mtakatifu,. Shemasi atasema: "Milango milango, tusikilize kwa hekima". Nikusema mufunge, mufunge milango, juu hapana kuingia ndani mtu moja bila kuwa mwaminifu ao mukosefu ya imani, kwa sababu hii Matoleo ni paka ya waaminifu, wenye waliisha kubatizwa. Tena, milango ni na masikilizo ya kila mtu. Nikusema kila mtu ataangalia masikilizo yake, nikusema ma macho, masikio, pua, kinywa chake juu ya kumuungama na kumutukuza Baba Mungu wetu.

Hii Symvolo ya Imani ni hesabu ya ma zawadi ya Mungu na maungamo ya shukrani ya mtu mbele ya Mungu. Ni onyesho ya upendo yetu mbele ya upendo ya Mungu. Tunachunga hii mafundisho tulijifunza juu ya Mungu, kwani Huyu ni Hekima ya kweli.

Ile saa msomaji anasoma Symvolo ya Imani, mpadri anatenga ile Kitambaa inayeitwa Aeras juu ya Kikombe na Sahani Takatifu. Hii tendo yake inatukumbusha ile tetemeko iliyefanyika kwa Ufufuo ya Bwana Yesu Kristu. Mpadri anasimama hii kitengo ya Kitambaa, wakati msomaji atasema: "Na aliyefufuka katika siku ya tatu".

## Mwanzo ya Sandaka isiyo kumwangisha damu

Kutoka hii fasi inaanza Fumbo Takatifu ya Eukaristia (Komonyo Takatifu). Mpaderi anatoa Mukate na vinyo kwa Mungu na anasema: „Tusimame vizuri. Tusimame na woga! Tusikilize kwa kutolea sadaka takatifu kwa amani". Kutoka ya huku tunapaswa kuangalia kwa sababu tunapaswa kupandisha roho yetu usafi mbele ya Mungu, bila ma shuruli na masubuko na magumu ya hii dunia. Na taifa ya waaminifu anajibu: "Huruma ya amani, zabihu ya sifa", nikusema tunatoa sabihu ya shukrani katika wimbo na matendo mazuri yetu ao tunaweza kusema hivi: Tunaishi sawa vile anataka Mungu juu ya kutukuzwa kwa milele. Hii sandaka anapenda Mungu kupita ya ma sandaka ingine ya kuchinja ma nyama.

Hii baraka inafwata ni toka Mtume Paulo: "Neema ya Mungu wetu Yesu Kristu, na mapendo ya Mungu na Baba ya ushirika wa Roho Mtakatifu uwe nanyi nyote". Kitoleo ya Mwana wa

Pekee pa Musalaba ni neema, kwa sababu sisi tulijisikilizana na Mungu Baba kwa sandaka ya Yesu Kristu. Zamani tulikuwa wa adui Yake lakini sasa yeye alitupenda na alituokoa. Kwa sababu ushirika yetu na Utatu Mtakatifu inafanyika kwa Roho Mtakatifu, tunaita hii mapatano ushirika pamoja na Roho Mtakatifu. Kwa hii sala Mpadri anaomba juu vile vitu vitakatifu kubakia kwa sisi kwa milele.

Kisha taifa ya waaminifu wanaomba juu hii baraka ibakie na kwa huyu mpadri, mukujibu hivi: “na kwa roho yako”.

Mpadri anasema: “Tuweke mioyo yetu”. Mpadri anatwambia ya kama hii mapatano na Bwana Yesu inatimizwa mulimani juu pia ya Mapendo ya Baba, pahali inamalizwa Fumbo Takatifu ya Ushirika pamoja na Roho Mtakatifu. Roho ya mwaaminifu inaanza kupanda juu pia kwa upendo juu ya kukutana na Yesu Kristu.

Waimbaji wanajibu kwa jina ya taifa: “Tunayo kwa Bwana”, nikusema wanakikisha ya kama waliisha kupanda na kupatana na Bwana Yesu Kristu. Walizarau kila shuruli ya hii dunia na walipanda pa Kiti ya Bwana Yesu.

Kisha mpadri anawaambia kwa waaminifu juu ya kumushukuru Bwana. Namna kabisa nzuri juu ya kukumbusha ma zawadi ya Mungu ni kama sisi tunayakumbuka na tunamushukuru Mungu.

Waaminifu wanaichika ya kama shukrani mbele ya Bwana ni wajibu na haki..”.

## Sala ya kutoa Sandaka.

Hii sala ni kabisa kubwa na inaanza ya hii ombi: “Ni wajibu na haki kukuimbia, kukutukuza, kukusifu, kukushukuru na kukusujudu, pahali popote pa utawala wako…”. Tunamutukuza Mungu na tunamushukuru kwa ma zawadi yake yote yenye tunajua na yasiyokujua. Hii sala inafika ku mwisho kwa mwimbo ya shangwe: “Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu Bwana Savaothi. Mbingu na inchi zimejazwa kwa utukufu wako…”. Hii ni mwimbo ya malaika, wenye wanaimba mbele ya Mungu, bila kusimama. Kipande ya mbili ya hii mwimbo: “Hosana juu pia, muhimidiwa yeye anayekuja kwa jina la bwana! Hosana uliye juu pia”. Ni ile mwimbo waliimba taifa ya Ebrania, wakati walimupokelea Yesu Kristu mujini Yerusalema, juma moja mbele ya Ufufuo yake.

Hii mwimbo ni maana ya mbili. Ku mwanzo ni utukufu juu ya ile ushindi iliyetimizwa kwa ujio na Ufufuo ya Mwokozi wetu hapa duniani na ya mboli ni unabii juu ya Ujio yake ya Mbili.

Mbele ya hii mwimbo shemasi anasema: “akiimba, wakilia, wakipaza sauti na kusema wimbo wa shangwe”, kwa sababu Majeshi ya malaika, yenye yalikuwa sula ya nyama ine waliimba hivi, katika Nabii Iezekieli (1,10-14) na Ufufnuo 4, 7-8). Nyama ya kwanza alifanana sawa ndege kwazi kibeba kuku (kwani huu ni mufalme ya ma ndege yote). Nyama ya mbili alikuwa sawa ndumbe (ngombe mwanaume), kwani huu ni mufalme ya ma nyama ya nyumba ya watu. Nyama ya tatu alifanana sawa simba, kwani huu ni mufalme ya ma nyama ya pori na ule ya inne alifanana sawa mutu, kwani huu ni mufalme ya viumbe vyote vya ulimwengu. Hawa ma nyama wanatuonyesha na Waevangelizazi wa Ine.

## Ukumbusho.

Ulimwengu nzima inatuma mashukuru na utukufu kwa Mwokozi ya dunia nzima. Tena na mpadri anasema: „Hata sisi pamoja na majeshi heri hawa, ee Rabi Mpenda-wanadamum tunapaza sauti tukisema: Wewe ni Mtakatifu, Mtakatifu kamili, Wewe na Mwana wako wa pekee na Roho Yako Mtakatifu....Wewe uliyeupenda ulimwengu wako, hata ukamutoa Mwana wako wa pekee...“. Kisha mpadri anasema: Twaeni, kuleni, huu ni mwili wangu unaomegwa kwa ajili yenu...Nyweni ninyi wote, Hii ni Damu yangu ya Agano Jipya...“.

Liturgia Kimungu inatuonyesha urefu ya Upendo takatifu ya Mungu. Na Upendo Yake ni Mwana wake wa pekee, aliyemutuma duniani. Hii sandaka haiko alama ao mufano, lakini ni sandaka ukweli. Yesu Kristu anajitoa sandaka kwa waaminifu sawa Mwana Kondoo ya kumuchinja na mara moja sawa mwenye ufufuo. Sandaka ya Kristu pa mulima Kalvario na sandaka ya Liturgia Kimungu ni umoja kwa sababu mmoja ni Mwana Yesu Kristu wa pekee. Kwa hivi Yesu Kristu alisema: „Fanyeni hivi kwa kunikumbuka“ (Luka 22,19). Na sisi, kama tunapewa Mwili na damu yake, tunaishi mara ingine Sandaka yake pa Kalvario.

Tunamushukuru Mungu, basi, kwa ma zawadi yake yoyote mukusema: „Vilivyo vyako kutoka vilivyo vyako tunakutolea kadiri ya vyote na kwa ajili ya vyote“. Tunafamia ya kama vile vitu vyetu ni vitu vyake. Na Yesu, anaangalia hali ya shukrani ya watoto ya roho yake na anawarudishia sasa hapana mukate na vinyo, lakini Mwili na Damu yake. Sisi tunamupatia kila kichote tukona yo na Huyu anatupatia vitu vyovyote vyake, nikusema Mwili na damu Yake.

## Wito ya Roho Mtakatifu

Mpadri anaendela kusema na sauti chini: "Tena tunakutolea ibada hii ya akili na bila damu, tunakuomba na kukusihi na kukuronga, utume Roho yako Mtakatifu juu yetu sisi na juu ya vipaji hivi vilivyo mbele hapa. Kristu ufanye mkate huu kuwa Mwili Mheshimiwa wa Kristo wako. Amina. N ailiyo ndani ya Kikombe hiki kuwa Damu heshimiwa ya Kristu wako. Ukivigeuza kwa Roho yako Mtakatifu. Amina, amina, amina".

Vile Vitu, mukate na vinyo, ni pa Meza Takatifu kwa hii wito ya Roho Mtakatifu yanageuzwa kwa siri ya kuwa Mwili na Damu ya Kristu. Hii geuzo ya ajabu inafanyika kwa uwezo ya Utatu Mtakatifu. Kisha hii mkata haiko mkate ya bura, lakini ni ya kweli Mwili na Damu ya Kristu. Hii Fumbo inatuonyesha upendo kubwa ile iko na Mungu kwa sisi, wenye tuko watoto wake ya kiroho. Ndani ya Liturgia Kimungu tukona tendo kubwa ya kushuka Roho Mtakatifu sawa vile alishuka ile siku ya Pentikote (ma siku makumi tano kisha Ufufuo ya Kristu). Kama Roho Mtakatifu hasikukuwe ndani ya Kanisa, haikukuwe Kanisa ya Kristu. Kwa sababu Kanisa ya Kristu iko, Roho Mtakatifu ni ndani ya Kanisa Yake.

Kisha mpadri anakumbuka ma jina ya Wababu, wababa, wapatriarkhe, Manabii, Mitume, Waevangelizaji, Mashahidi na ya kila nafsi aliyekufa katika imani na toba kwa jina ya Kristu. Kabisa inafanyika ukumbusho ya Mzazi-Mungu Bikira daima Maria, kwa sababu, kwa ajili yake sisi tunatakaswa.

Kisha mpadri anakumbuka ma jina ya warafiki ya Kristu, nikusema Watakatifu. Kisha anakumbuka ma jina ya wafu juu ya kuwapumuzisha Mungu pahali ni nuru ya Nyuso yake.

Hii Kitoleo inajitoa juu ya ulimwengu nzima na ya Kanisa ya Kristu Katholiki na Apostoliki, kwa wale wanaishi katika utume na woga ya Mungu, juu ya wakubwa ya serkali na ya wale wanapata magumu ya mbalimbali. Ku mwisho mpadri anakumbuka ma jina ya wale wa ndugu wanakumbuka hii dakika. Nikusema, ee Bwana, kumbuka na ma jina ya wale wa ndugu wanasali hapa sasa waaminifu ya Kanisa yetu.

Hii sala ya kutoa sandaka inayeanza toka «Nasandiki Mungu moja… » inaisha wakati mpadri anasema: «Rehema za Mungu wetu mkubwa na Mwokozi Yesu Kristu, jitakuwa pamoja nanyi nyote». Kisha mpadri ao shemasi ataendelesha na maombi ingine (Ekteni Kubwa).

Mungu mpenda-wanadamu alitakasa tuu Vitu Vitakatifu na aliyapokelea pa Altari yake juu pia na mpadri anamuomba juu ya kutuma kwa sisi wote Neema ya Roho Yake Mtakatifu. Na sisi tunaomba juu hawa Vitu Vitakatifu kutusaidia juu ya kuchukua neema ya Mungu kwa kutembea katika mapenzi yake. Ku mwisho tunamuomba Mungu atupatie unganisho ya imani kwa sababu paka hivi iko namna ya kukaribiasisi na ya kupewa Mwili na Damu ya Kristu. Na sisi tunamulaka ya kama «Hata maisha yetu pia, tujiweke mikononi mwa Kristu, Mungu wetu». Kama tunakaribia ya kupewa katika imani moja, upendo, usamehe na toba, tunapata ya kweli maondoleo ya zambi, ushirika ya Roho Mtakatifu na hapana ya kuwa kwa hukumu ya nafsi yetu.

Takatifu Komonyo wanaweza kuchukua paka Waorthodoksi, wenye wanasadiki ya kama Yesu Kristu ni Mungu na asili umoja na Baba wake. Tunamukomunyika kwa sababu tunamusadiki ya kama Huyu ni Mwokozi na Mungu wetu. Inakatazwa kupewa Mwili na Damu ya Kristu hawa wasiyobatizwa, wakosefu ya imani na wapagano. Kama wapadri watawapatia Komonyo Takatifu, watasema nini mbele ya Kristu ?, kwa sababu anasema Kristu : « Musiwape imbwa kitu kilicho kitakatifu » (Matayo 7,6). Hii haiko mufano mbaya ya Kanisa yetu, lakini ni ubinadamu ya Mama Kanisa yetu, kwani anasikia huzuni na upendo ya watu wote. Anawapenda kweli, lakini hasiweze kuwatupa kwa uhukumu ya Mungu ao kwa moto ya gehena, kama watakomunyika bila kuwa stahili.

### Baba yetu uliye mbinguni…”

Na Symvolo ya Imani tulikikiri ya kama tunasadiki kwa Mungu Moja Mwenyezi na Muumba. Kwa hii sala ya Kristu tunazungumuza kwea Mungu Baba, sawa sisi tuko watoto wake. Hii mapatano yetu inatuonyesha ile mapatano tutapata mu uzima ya milele. Kisha, kwa sababu inakaribia saa ya kupewa mwili na Damu ya Kristu, mpadri anatubariki mukusema: “Amani kwa wote”. Vile na Yesu alisimama katikati ya Mitume mwake na alisema “amani kwa wote”. (Yoane 20,26). Kisha anatwaambia mpadri juu ya kuinamisha vichwa vyetu. Hivi tunamufamia Mungu sawa Rabi na Muumba yetu na sisi sawa watumwa wanyenyekevu tunamushukuru kwani tulifanyika watoto ya roho yake. Kila mwaaminifu eko na magumu na ushindani ya roho yake na Rabi wetu anatupatia ma zawadi yake katika matatizo yetu.

### Sala ya kupanda juu pia Mwili ya Kristu

Kristu alichukua mwili yetu na alikuja karibu yetu, bila ya kuacha Kiti ya Baba yake mbinguni. Kisha ya Kupanda kwake mbinguni aliikaa mara ingine pamoja na Baba yake, lakini mara moja ni na karibu yetu ndani ya Liturgia katika Mwili na Damu yake. Vile na yeye alisema, ile usiku alitoa Fumbo ya Mwili yake kwa Mitume wake : « Nyuma ya wakati kidogo, dunia haitaniona tena, lakini ninyi mutaniona » (Yoane 14, 19). Wale watu wanaishi ndani ya giza ya shaka kwa Nyuso ya Kristu, hawaweze kumufamia na kumuchukua ndani yao Yesu Kristu. Lakini Yesu ni karibu yetu na anataka kuikaa ndani ya roho yetu. Kwa hivi na mpadri anasema: «Usikilize, ee Bwana, "toka makao yako",utujie ututakase, wewe unayekaa mbinguni pamoja na baba, tena uliye hapa pamoja nasi bila kuonekana...“. Utuangalie, ee Bwana, toka makao yako ya mbingu na ututakase, kwa sababu uko pamoja na sisi. Lakini mbele ya kupewa Mwili na Damu yake, tunakikisha ya kama hawa Vitu Vitakatifu yanajitoa kwa watu watakatifu na hapana kwa watu wowote. Kisha taifa ya waaminifu wanamujibu ya kama «Mtakatifu ni mmoja peke yake, Bwana ni mmoja peke yake. Yesu Kristu, katika utukufu wa Mungu Baba. Amina”, kwa sababu paka Huyu ni Mtakatifu ya kweli. Sisi tunaitwa watakatifu, kwani tunataka kuwa na kama tunaendelea kupokelea ma baraka ya utakaso yetu. Kwa hivi na tunapewa na mwili na Damu ya kristu. Hii dakika mpadri ananyanyua Mwana Kondoo (Mwili ya Kristu) na mikono yake. Hii inaonyesha Ufufuo ya Yesu. Saa ya kuchukua Mwili na Damu ya Kristu inakaribia.

### Mwimbo ya Ushirika (Kinonikon)

Hii mwimbo ni shairi moja inayetokea ya zaburi ya Nabii Daudi. Mwisho yake inaisha na neno: Aliluya, nikusema: Musifuni Bwana. Kinonikoni haiko paka moja, lakini ni ingine ya kila Siku Kuu. Paka ya kila siku ya Mungu ni umoja, hii: Musifuni Bwana toka mbingu. Aliluya“. Ile saa waimbaji wanaimba Kinonikoni, mpadri ndani ya Altari:

1.Anagawanya Mwili ya Kristu. Kwa Liturgia ya kwanza, ile alifanya Yesu Kristu mu karamu Kubwa pamoja na Mitume wake, huyu wa pekee aligawanya Mwili yake. Hii tendo inafwata ya kila Liturgia na hii kazi anafanya mutumishi wa Mungu na anapatia kwa waaminifu kila kimoja Kipande Kitakatifu ya Mwili ya Kristu pamoja na Damu yake. Ni kweli ya kama ya kila kipande Kitakatifu ni **Mwili muzima** ya Bwana Yesu Kristu na hapana kipande chake. Chakula yoyote ya dunia iko namna ya kuisha siku moja, lakini Mwili ya Kristu haitaishe.

2.Kisha ya kupandisha Mwili ya Kristu mpadri, unajifata unganisho ya Mwili takatifu pamoja na Damu yake. Nikusema mpadri, aligawanya Mwili ya Kristu ya vipande ine, kisha aliyaweka na alama ya Musalaba pa Sahani Takatifu. Kisha anakamata moja-moja na anaiweka ndani ya Kikombe Kitakatifu. Hivi inaonekana na inahurumiwa unganisho kwa Nyuso moja ya ma asili mbili ya Kristu. Tena inaonyeshwa na unganisho ya Sandaka na Neema Takatifu, ile inajitoa kwa waaminifu katika Komonyo Takatifu.

Kisha mpadri anamwangisha ndani ya Kikombe na maji ya kivukutu juu ya kuwa Damu ya kweli, nikusema sawa sasa ilitokea toka mbavu yake. Hii kazi ya mpadri inaonyesha kushuka Roho

Mtakatifu, kwa sabubu na Roho anaitwa Majii ya muzima na alionekana sawa ulimi ya moto ile siku ya Pentikosti na ilisimama pa vichwa vya Mitume vyote. Roho Mtakatifu anasabitisha uzima yetu.

**Anakomunyika ku mwanzo mpadri.**

Mu nyuma aliisha kusoma mpadri ma sala ya Komonyo Takatifu, na sasa atapewa Mwili na Damu ya Kristu. Kila Liturgia ni Ufufuo wa Kristu, sawa vile na sisi tuliisikia. Kila mwaaminifu anayekula Mwili na Damu ya Kristu anakikisha Ufufuo ya Kristu na ufufuo ya nafsi yake. Anaishi tangu hii uzima Pasaka kubwa na ataendelesha kufurahi hii Pasaka na mujini Yerusalema juu pia ya Paradizo. Kwa hivi uzima muzima ya kila mwaaminifu orthodokse ni kila siku shangilio moja kubwa na Pasaka moja ya milele.

Ile saa mtu anapokelea ndani ya mwili yake Mwili na Damu ya Kristu, ni saa ya upendo kubwa ya Kristu. Mungu ni upendo ukamilifu na sasa anajitoa kwa kila mwaaminifu. Kwa kukaribia ya kupewa Mwili ya Kristu tunapaswa kufika katika „woga wa Mungu na imani na mapendo“. Zamiri usafi, mafungo ya kula na sala ni namna nzuri juu ya kupokelea stahili Mwili na Damu ya Kristu.

Tunajua sisi wote ya kama tunaenda Kanisani kwa kupewa Mwili na Damu ya Kristu. Kama waaminifu walichunga rohoni yao nzuri na hawakufanye zambi mpaka maungamo yao ya mwisho, wataweza na mara ingine ya kuchukua Mwili na Damu ya kristu katika baraka ya mpadri ya roho wao.

Yesu Kristu ni muzima sasa ndani ya Kikombe Kitakatifu na anatuita juu ya kupima ya kama Huyu ni Kristu, Mwokozi wetu, sawa vile alisema hivi  na kwa Mitume wake, kisha ufufuo wake: „Tazameni mikono yangu na miguu yangu na mujue kwamba ni mimi mwenyewe. Muniguse mwone, kwa maana muzimu hana mwili wala mifupa kama munavyoniona mimi kuwa nayo“. (Luka 24,39). Kwa hivi inamalizwa kwa kila Liturgia Kimungu mapatano kati ya Mungu na mtu. Kwa hivi na mpadri anaita kila mukristu na jina lake: „Mutumishi wa Mungu..............(jina lake) anapewa Mwili na Damu ya Kristu kwa maondoleo ya zambi na uzima ya milele“. Hivi waaminifu, kwa sauti ya waimbaji, wanaimba ya kama walipokelea ndani yao Nuru ya kweli, na mpadri anarudia ndani ya Altari mukusema: „Ee Mungu, okoa taifa yako na bariki uriti wako“. Kisha anaweka Vitu Vitakatifu pa Meza na anafukiza hizi na chetezo mukusema: „ee Mungu, utukuzwa juu mbinguni na utukufu wako uwe duniani yote“. Ubani inaonyesha ile pepo ilishuka kwa kushuka Roho Mtakatifu pa vichwa vya Mitume, kisha Ufufuo wake. Kila mara, kama mukristu moja anachukua Komonyo Takatifu, anapokelea Jua ya Uhaki, anaye eko Nuru, Mwangaza, furaha, uzima, chakula na kinywaji..“. Kwa hivi anaimba: Tumeona nuru ya ukweli...“. Yesu Kristu anatuokoa toka giza ya hii dunia. Huyu anatusindikiza ya kupita hii njia ya dunia. Huyu ni Pasaka yetu, kwa sababu maana ya Pasaka ni mapito toka uzima ya zambi mu Ufalme mbinguni.

Kisha Komonyo Takatifu tulifika ku mwisho ya Liturgia Kimungu. Padri anasema na sauti chini: Daima sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina“, na anaonyesha mara ya mwisho mbele ya ma macho ya waaminifu Vitu Vitakatifu, pahali ndani ni Yesu Kristu muzima. Hii tendo ya mpadri ya kupandisha mara ya mwisho Vitu Vitakatifu inatukumbusha Kupanda Yesu Kristu mbinguni na ya kama ulimwengu nzima ilijaa kwa utukufu yake.

Kisha mpadri anashukuru mara ingine Yesu Kristu kusema hivi: „Simameni. Tukishiriki Fumbo za ajabu za Kristu, Fumbo za umungu, takatifu bila doa, za kutokufa, za mbinguni na zenyi kuleta uzima, tumushukuru Bwana“. Hii ushukuru yetu ni sawa ile shukrani walifanya na Mitume, kisha Karamu Kubwa wao pamoja na Mwalimu mwao Yesu Kristu. „Na wakati walipokwisha kuimba wakaenda katika mulima wa Mizeituni“ (Matayo 26, 30).

**Sala opisthamvonos.**

Liturgia Kimungu ilianza na hii ombi: Kwa amani tumwombe Bwana“, na hii amani tuliisikia mara mengi sawa baraka na sasa, pahali Liturgia inatembea ku mwisho, mbele ya kurudia nyumbani yetu, mpadri anatupatia hii baraka mara ingine kusema: „Twendeni na amani“.

Kazi kubwa ya Liturgia ilitimizwa na hii ni kipatano na unganisho katikati ya Mungu na mtu, kwa sababu tulichukua ndani yetu Mwili na Damu yake. Sasa tunaitwa ya kuwa washuhuda ya uzima ya Kristu ndani ya dunia. Tena tunaitwa kutoa upendo na amani katikati ya warafiki, wa ndugu, wajirani na wasaidizi wetu. Uzima ya mwaminifu moja kila siku ni paka amani na mapendo. Kama mukristu

moja hana na amani na mapendo, inapaswa kutafuta ndani yake shetani gani anamuuzi na anamusikitisha.

**Jina la Bwana himidiwe tangu sasa…**

Hii haiko ni ombi, lakini ni utukufu moja ya Jina ya Mungu na ilijikamata ku zaburi 112, shairi 2. Hii zaburi ni ya kwanza ya kundi moja ya ma zaburi yenye waliimba taifa ya Ebrania ile magaribi ya Pasaka yao. Na sisi sasa tunamuhimidi Mungu wetu, kwani alitustahilisha kukomunyika Mwili na Damu yake. Kisha mpadri anaenda ku Meza ya Proskomidi na anaomba kwa Mungu ya kujaa ma roho yetu na furaha ya malaika na hapana furaha ya hii dunia. Hii furaha kama itaingia rohoni ya mtu moja anasikia ya kama ni mutajiri na mwenye heri kupita ya watu wote ya dunia.

## Kuaga.

Mpadri sasa anabariki taifa ya waaminifu na anatakia ikuje rehema yake mu uzima na roho yetu ma siku zote zetu. Namna gani tutachukua baraka yake? Mungu anatufurahisha katika neema yake, kwa sababu anaangalia kwa unyenyekevu ya watumishi wake (Luka 1,48). Anabariki taifa ya kurudia nyumbani yao kusema hii ombi : Kristu hatuhurumie kwa maombezi ya Mzazi-Mwake na ya Watakatifu wote, hapana kwa sababu tuko na kitu kimoja yetu ya kumuonyesha, hata kama tunafunga ya kula, ao tunaungama na tunakomunyika, lakini kwani kunatumainia paka kwa upendo wake binadamu. Kwa ajili ya rehema kubwa ya Bwana Yesu Kristu sisi tunatumainia ya kuokolewa.

Kisha mpadri anagawanya antidoro, maana yake ni hii: Wale waaminifu wataondoka bila ya kupewa Mwili na Damu ya Kristu, Kanisa pahali ya Komonyo anawapatia hii kipande ya mukate, inayetokea toka Prosforo, pahali inatokea Mwili ya Kristu. Waaminifu wanakamata katika heshima na pasopo hii antidoro na wanabusu mukono ya mpadri, kwa sababu mu nyuma kidogo alikamata huyu Mwili na Damu ya Kristu.

Liturgia kimungu haiko ono ao kitu ya kuisikia, lakini ni tendo ya Mungu na pamoja naYe anatumikia na taifa yake yote. Kwa hivi Kanisa anatuita juu ya kupatana na sisi hapana sawa wageni ya kutazama, lakini sawa watumishi pamoja na wapadri.

Ndani ya hii Liturgia kila mwaaminifu anasikia sawa ya kuzaliwa mara ya mbili. Anatosha kila matakio mbaya, kila shuruli ya hii dunia, anapata ma nguvu mapya juu ya kuendelesha mwendo yake pamoja na Kristu. Inapaswa sasa ya kurudia ku kazi yake ndani ya dunia, hivi:

Kupita munyenyekevu na mupole mbele ya mapatano yake na watu weingine.

Kupita muvumilivu ya kunyanyua uzito ya magumu (musalaba)yake.

Kupita mwenye nguvu ya kutumika matendo katika upendo ya Kristu.

Kupita mwenye kufufua katika roho yake.

Anakamata mpango juu ya kutimiza kusudi ya uzima yake, kusudi ile Mungu alimuumba, nikusema ya kufanana katika sula ya Kristu na atakuwa muletaji ya Roho Mtakatifu.

# MA FUMBO TAKATIFU YA KANISA ORTHODOKSE

Asili kimutu, kisha kosa ya wazazi ya kwanza, iliharabika na ilifanana sawa shamba moja ya kujaa na miiba. Alikuja Yesu Kristu juu ya kutengeneza hii asili kimutu. Hii kazi aliendelesha kuimaliza pamoja na Mitume mwake na mpaka leo inamalizwa kwa uwezo ya ma Fumbo Takatifu. Kwa sababu tuko watu na hatuweze kuisikia ma fumbo Takatifu katika akili yetu, tunayapokelea kwa imani na tunatakaswa, kwani toka ma Fumbo inakuja kwa sisi neema ya Roho Mtakatifu.

Ma Fumbo Mtakatifu ni ma ibada yalitokea toka Mungu wetu Yesu Kristu. Ma fumbo (mystere) yote yanatupatia Neema kimungu na tunalazimishwa yoyote kwa wokovu wetu. Ni lazima kabisa kubali ma Fumbo ya Ubatizo, Krisma Takatifu, Komonyo Takatifu na Maungamo. Ma fumbo ya Ndoa, Upandirisho na Kupakaa na Mafuta haiko ulazimisho ya kila mutu, lakini katika mapenzi ya Mungu na yake.

Ma Ibada haya yanaitwa ma Fumbo kwa sababu mbili: Ku mwanzo, kwa sababu, katika mt. Yoane Krisostomo, tunaangalia vitu vingine na tunasadiki kwa vitu vingine, nikusema tunasadiki ya kama ni Neema Kimungu, lakini haionekane. Ya mbili, kwani haipaswe kuangalia na kusikia ma Ibada haya wale wasiyoamini ao wapagano, lakini paka wale walibatizwa Kanisani orthodokse. Ma

Fumbo haya hakuna namna ya kubali hawa watu wanaishi uzima bila woga na neema ya Mungu. Hakuna mapatano katikati ya ma Fumbo Takatifu ya Kanisa Orthodokse na ya mafumbo ya wapagano ao ya ma „kanisa“ ingine.

## Namna gani ma Fumbo ni ya kweli?

Juu ya kuwa Fumbo moja ya kweli, nikusema juu ya kupatia kwa mwaminifu moja neema kimungu inalazimiswa vitu hizi:

1.Mpadri inapaswa kukamata cheo ya upandirisho yake kwa askofu yake katika sheria ya Kanisa Ortodokse.

2.Vile vitu ya kuonekana ya kila Fumbo ni ya mbalimbali ya kila Fumbo.

3. Kila Fumbo iko na Ibada na wimbo yake yake.

Fumbo kubwa kupita ya ingine ni Fumbo ya Komonyo Takatifu. Ni sandaka kubwa, kwa sababu Yesu Kristu anatoa Maungu yake kwa wokovu ya watu wote ya ulimwengu.

Fumbo ingine kubwa ni Ubatizo.

Maana ya jina ubatizo ni ya kuingisha mtu moja ndani ya maji mwili yake muzima. Kama mtu ao nyama moja ataanguka ndani ya maji, atakufa na inalazimishwa mtu moja ya kumuokoa. Huyu eko Bwana Yesu Kristu, aliyetuokoa kwa usulubio Yake na alitutosha inje ya hadeze, pahali alikuwa tangu zamni mataifa yote. Na sisi, kama tunabatizwa mara tatu ndani ya maji, tunakufa katika uzima yetu ya zamani, sawa na Yesu Kristu aliingia ndani ya kaburi yake ma siku tatu na alifufuka katika utukufu wake. Vile na sisi, tunatoka inje ya maji sawa ya kuzaliwa mara ya mbili, kwa sababu tulifufuka kwa jina ya Utatu Mtakatifu. Ufufuo ya Bwana Yesu Kristu ni alama ya ubatizo yetu. (Angalia Yoane 3,4-7. Waroma 6,3-9. Waebrania 12,23). Maana ya hii Fumbo ni hii: Tunatokea ku uzima ya zambi na tunavaa sawa nguo neema kimungu ya Kristu na tunapata wokovu ya nafsi zetu kwa saidio ya Mungu na matendo mazuri yetu.

Tunapata alama hii Fumbo ndani ya Agano la Kale na Agano Jipya. Bwana Yesu, wakati alizungumuza na mufarisayo Nikodimo, alimwambia: “Kweli, ninakuambia: mutu asipozaliwa kwa maji na Roho, hawezi kuingia katika ufalme wa Mungu” (Yoane 3,5). Mwanzo na matoleo ya hii Fumbo ilifanyika kisha Ufufuo wa Kristu, ile wakati alisema kwa wanafunji wake: “Basi kwendeni kwa watu wa mataifa yote mukawafanye kuwa wanafunzi wangu, mukiwabatiza kwa jina la Baba, na la Mwana na la Roho Mutakatifu…” (Matayo 28,19). Na huyu Bwana Yesu alisema ya kama hasiweze kuokolewa mtu moja kama atabaki bila ubatizo. “Anayeamini na kubatizwa ataokolewa, lakini asiyeamini atahukumiwa”. (Marko 16,16).

Vile vitu vya kuonekana ndani ya Fumbo ya Ubatizo ni tatu: 1) Maji, 2) ya kuingisha mtu ndani ya maji mara tatu na 3) ma sauti ya mpadri: “Anabatizwa mutumishi wa Mungu…kwa jina la Baba na la Mwana na ya Roho Mtakatifu”.

Kwa hii Fumbo inajitoa kwa ule mtu atabatizwa:

1) Maondoleo ya zambi zake zote. Nikusema Neema kimungu itamusafisha ya ile kosa ya Wazazi wa kwanza Adamu na Eva na tena itasafisha na zambi zake, kama huyu atabatizwa na kipimo kubwa yake.
2) Kuzaliwa katika kiroho mara ya mbili na uwezo yake ya kuwa tangu ile saa mtoto wa roho ya Bwana Yesu Kristu. Huyu anayebatizwa anarudia mu uzima ya Wazazi aa kwanza, mbele ya kosa yao mbele ya Mungu. Kwa hivi, japo atakufa katika mwili yake, lakini katika uzima ya kiroho ataishi kwa milele, kwa sababu lufu ya mwili haiweze kumusimamisha na kumurudisha ndani ya gehena. Basi, ni lazima kabisa na huyu mukristu kujaribu kila siku juu ya kuishi katika sheria ya Mungu.

Juu ya kubatizwa mtu moja inapaswa kuamini kwa Nyuso ya Yesu kristu. Hii imani hatuweze kuikombola na makuta wala na marafiki wala na hii uzima yetu. Mashahidi ya Kanisa yetu, walikufa kwa imani yao mbele ya Kristu.

Hii imani inaikaa na vipande tatu:

1.Kukataa shetani na ya kuepuka kila kitu kibaya ku uzima ya huyu anayetaka kubatizwa. Kwa hivi na mpadri anamufiga na anamufukuza shetani katika sala ya Kanisa.

2. Kukamata mpago ule mutu ya kama atafata mwendo na mafundisho ya Yesu Kristu mu uzima nzima yake. Nikusema atasimama ya kuwaza na kutenda sawa aliishi zamani. Uzima yake itakuwa ya kujaa katika mwangaza na upendo ya Yesu Kristu.

3.Kukamata mpango ya kama tangu ile siku ataabudu na atasujudu paka Bwana Yesu Kristu.

Ma fumbo yote hakuna namna ya kusikia mtu moja katika akili yake,lakini anasikia ndani yake paka uwezo na nguvu yao katika neema ya Roho Mtakatifu. Ufamio ya Fumbo haitoke ku nguvu ya akili ya mtu, lakini kwa upendo ya Mungu. Hasitafute kondoo muchungaji yake, lakini muchungaji anatafuta kondoo yake, anasema mt. Nikolao Kavasilas. Vitu vyote vinatokea toka Mungu. Na, wakati atabatizwa mtoto moja, hasisikie neema kimungu, kwani nguvu ya akili ni kidogo. Lakini Mungu anamufurahisha na anamujaa na neema kimungu yake. Hata, kama mutu ni mkubwa, hasiweze kusikia namna gani Mungu anatumika katika neema yake ndani ya akili na uzima yetu. Na zamani watu walibatizwa na kipimo urefu, lakini hii haiseme ya kama hawakubatizwa na watoto. Wakati wazazi waliamini kwa Kristu, jamaa yao ilibatizwa muzima. Na Yesu Kristu aliita na alibariki watoto (Matayo 19,14-15). Mtakatifu Irineos, askofu ya muji Lugduno ya Fransa aliandika ku mwaka 150, kisha kuzaliwa kwa Kristu, ya kama ilikuwa zoezo ya kubatizwa watoto mu wakati yake. Vile alisema na mt. Kyprianos, askofu ya muji Karkhidona ya Livii ku mwaka 250. Na Mt. Grigorio Mutheologo alisema ya kama inapaswa watoto kubatizwa na umri yao udogo.

Kama mtoto moja ni ya hatari ya kifo, Kanisa yetu inafamia Ubatizo pa pepo kwa jina ya Utatu Mutakatifu. Nikusema mukristu moja ananyanyua huyu mtoto juu pia mara tatu na anamubatiza pa pepo kwa jina ya Utatu Mtakatifu. Kama mtoto ataishi, wazazi yake watamubatiza katika sheria Kanisani ya Kristu.

Hawa watoto wanakufa bila ubatizo, Watakatifu wingi wanasema fasi yao ni katikati, nikusema wala wanatukuzwa, wala wanateswa ndani ya gehena.

## Fumbo ya Krisma (kwa kumimiya).

Uzalio ya kiroho kwa Ubatizo haiko kamilifu. Huyu mtu aliyebatizwa ni sawa mtoto katika uzima ya Kristu na eko na ulazimisho ya saidio. Hii saidio ni ma zawadi ya Roho Mtakatifu, yenye yanajitoa kwake kwa hii Fumbo ya Krisma.

Mu Agano Jipya hakuna ushuhuda kusema ya kama Yesu Kristu alipatia kwa Mitume mwake hii Fumbo. Lakini Mitume wa Kristu walitupatia hii fundisho na hii Fumbo kwa hii maneno: „Lakini Kristu amemimiya Roho Mutakatifu juu yenu, kwa hivi ninyi wote munajua yaliyo kweli“. (Barua ya kwanza ya Yoane 2,20). Na „Basi Mungu amewaweka ninyi alama ya jina lake, akiwapa ninyi Roho Mutakatifu aliowaahidi“ (Waefeso 1,13-14). Tena toka kitabu „Matendo ya Mitume“, inaonekana safi ya kama waliisha kubatizwa watu kwa shemasi, bila ya kukamata Roho Mutakatifu na kisha Mitume waliweka mikono pa vichwa vyao na wale Wakristu walikamata Roho Mutakatifu (Matendo ya Mitume 8,17). Tena na Mt. Yoane anasema sauti juu ya Roho Mtakatifu (7,39). Wale walikamata ku mwanzo Roho Mtakatifu walikuwa Mitume wa Kristu ile siku ya Pentikosti.

Vile vite vya kuonekana ni ya ine:

1.Manukato (parfum). Ni mafuta pamoja na manukato makumi ine (40), yenye yanaonyesha ma zawadi mengi ya Roho Mtakatifu.

2.Sala ya mpadri.

3.Kumimiya pa fasi ya mbalimbali ya mwili ya mtu.

4.Ma neno ya mpadri, anayesema : «Alama ya zawadi ya Roho Mtakatifu. Amina».

Kwa vile vitu ya kuonekana mpadri anapatia kwa mukristu Roho Mtakatifu.

Kama mukristu moja atapotesha akili yake, atakataa imani ya Kristu ao atafata ingine: «kanisa» ya uwongo na kisha anataka kurudia Kanisani Orthodokse, mpadri atamupokelea na hii Fumbo ya Krisma. Ma zawadi ya Roho Mtakatifu yanatumikia paka kwa kitubio, maungamo na Komonyo Takatifu.

## Fumbo ya Maungamo na kitubio

Kama Mukristu moja anakamata mpango ya kuungama, inapaswa ku mwanzo kutubu. Nikusema inapaswa kugeuza mawazo na tabia yake na atafata sheria ya Mungu. Inapaswa kusimama ya kutembea na kutenda sawa alifanya zamani na kisha atafata sauti ya mpadri ya roho yake na hamuri ya Kanisa. Vile atapata tunda ya kitubio ya kweli (Matayo 3,8).

Hii Fumbo alipatia Yesu Kristu kwa Mitume Wake, kisha Ufufuo wake, wakati aliwaambia: "Mupokee Roho Mutakatifu. Wowote mutakaowasamehe zambi, watasamehewa; na wale musiowasamehe, hawatasamehewa". (Yoane 20, 22-23).

Vile vite vya kuonekana ni ya tatu:

1.Maungamo ya zambi mbele ya mpadri ya roho na namna ukweli.

2.Ya kuweka mukono yake Mpadri pa kichwa ya ule Mukristu.

3.Somo ya sala ya usamehe, ile anasoma mpadri, lakini Yesu Kristu anasamehe zambi zake.

Hii Fumbo inafanyika kwa siri. Haipaswe hata mpadri ya roho kutangaza hata zambi moja kwa watu weingine, wala mtu mwingine haipaswe kwenda kwa mpadri kutafuta ma tangazo ya mutu fulani. Mpadri haipaswe kusema kitu. Tena na ule mukristu haipaswe kusema kwa watu weingine hile sauti mpadri alimwambia, kwa sababu ma shauri hizi ni paka ya huu na hapana ya mtu mwingine.

Iko namna Mpadri ya roho amupatie ma hamuri nguvu kwa ule Mukristu, nikusema atakataa kumuacha ya kupewa Komonyo Takatifu. Hii haiko malipizo, lakini ni sawa dawa juu ya kuponyesha mpadri malari na ma kosa ya roho yetu. Tunaungama kwa ule mpadri sisi tunamuchagua. Bila maungamo, hakuna wokovu. Huyu anayeutii kwa mpadri ya roho yake, anapata nguvu na namna ya kila matatizo yake na, tena ataokolewa.

Kama tunaenda kuungama hatusema (historia) hadisi, lakini zambi zetu ! Tunasema zambi paka zetu na hapana zambi ya watu weingine. Tunaweza kumuuliza mpadri yetu ya kila ulizo na mambo yetu juu uzima yetu ya kuwa katika mapenzi ya Mungu na Evangelio yake. Kama atasimama kuungama Mukristu moja, ataanguka, atapotesha imani na kitumaini yake na atapotesha tena na wokovu yake, kama mpaka mwisho ya uzima yake atakataa kuungama.

## Fumbo ya Upadirisho (Ordination)

Bwana Yesu tangu mwanzo ya kazi kubwa Yake, alichagua watumishi ya shamba Yake (matayo 20,1), Mitume kumi na wawili na aliwapatia cheo ya upadirisho, kwani na Huyu alikuwa Askofu Mkubwa.

Mitume kwa uwezo ya Roho Mtakatifu walipatia hii uwezo kwa wafwasi wao, wenye weko wa askofu na hawa kwa wanafunji wao na hivi inakuja hii mustari mpaka leo Kanisani Ortodokse.

Ndani ya Agano Jipya tunapata ma fasi mengi pahali Yesu Kristu alichagua Mitume wake na aliwapatia ma cheo tatu ya kuwa kila moja: askofu, Mwalimu na mufalme. Sawa vile na Yesu Kristu ni Askofu Mkubwa, Nabii, nikusema mwalimu na mufalme (Matayo 9,38. 10, 1-32 na Luka 10,17-24). Na Mitume ya kuweka mukono mwao pa vichwa ya wanafunji wao waliwapatia zawadi ya Roho Mtakatifu (Matendo 8,18. barua ya Kwanza ya Timot.4,14. Barua ya Mbili ya Timot.1,6. Waebrania 6,2).

Vile vitu vya kuonekana ni ya mbili:

1. Ya kuweka mikono yake askofu pa kichwa ya ule mutu atapokelea cheo ya kuwa mpadri (Lakini huyu askofu inapaswa kuwa na ufwasi kutoka Mitume).
2. Sala hii: «Neema Takatifu inayeponyesha makosa ya watu na inatimiza yenye yanakosea inastahili mweshimiwa …(jina lake) ya kuwa shemasi ao mpadri ao askofu. Basi, tunaomba ikuje kwake neema ya Roho Mutakatifu kamili.

Hii Fumbo haifanyike mara ya mbili. Na kanuni ya Makutano ya Ulimwengu ya Sita ku mwaka 681, kisha kuzaliwa kwa Kristu, ilijikamata mpango juu wa askofu wote watakuwa ku mwanzo watawa, nikusema inakatazwa kuowa. Lakini wapadri na ma

shemasi wanaweza, mbele ya upadirisho yao, ya kufanya ndoa yao, lakini inakatazwa ndoa, kisha upadirisho yao, kama atakufa kwa mufano bibi ya mpadri moja.

Upadirisho moja inafanyika ile saa ya Liturgia Kimungu. Upadirisho ya shemasi inafanyika kisha utakaso ya Vitu Vitakatifu, ya mpadri, kisha mwimbo ya Kheruvikon juu ya kuwa ile saa ya utakaso ya Vitu Vitakatifu na ya askofu inafanyika, kisha ya kuimba mwimbo ya Trisayon: Mungu Mutakatifu, mweza Mutakatifu, Musiyekufa Mutakatifu, utuhurumie" juu ya kubariki na kufundisha taifa ya waaminifu.

**Neema kubwa ya hii Fumbo.**

1. Askofu anachukua neema ukamilifu ya hii Upadirisho juu ya kumaliza ma ibada na matendo yoyote ndani ya Kanisa ya Kristu. Hii achanisho inayeonekana sawa moja ni askofu mwingine mitropoliti, ao Patriarshi ni ma cheo ya kazi yao, kwani cheo ya upadirisho yao ni umoja, nikusema wote weko paka wa askofu.
2. Mpadri anachukua neema ya upadirsiho kwa kufanya ma ibada na ma Fumbo yote, ila tu Ibada ya Utakaso ya Myro (manukato) Takatifu, fumbo ya upadirisho na ubatizo ya ma kanisa, kwa sababu hizi yote anayafanya paka askofu.
3. Shemasi moja anamusaidia askofu na mpadri na hasifanya huyu wa pekee hata ibada moja.

Kazi kubwa na uwezo ya cheo ya Upadirisho anatwaambia hivi mt. Kosmas wa Etolos. Anasema: „Kama utaangalia malaika moja na mpadri moja, ku mwanzo utasalimia na utabusu mukono ya mpadri, kwa sababu huyu anamaliza Sandaka isiyona damu ya Kristu na hii sandaka tena na malaika wanainamisha vichwa vyao na wanaiangalia na ushagao". Hii uwezo ya wapadri hata wa malaika hawakuwa nayo. Kwa hivi hii cheo ya upadirisho inapaswa kuichukua paka wale weko wa stahili.

Huyu anayetaka kuwa mpadri inapaswa:

1.Kutaka paka kwa ajili ya upendo na heshima yake mbele ya hii cheo kubwa.

2.Inapaswa kusema ushuhuda nzuri juu yake waaminifu weingine yote.

3. Haipaswe kuanguka mu zambi moja mnene sawa zambi ya uzini na usharati, ya kuua mtu ao zambi ingine mnene.

4.Inapaswa kuwa na zawadi ya kiroho na nguvu ya akili na mwili yake ya kutumika kazi ya Mungu.

Kazi ya kupata wapadri ni kazi ya waaminifu wote. Sisi, hata kama mpadri moja anaishi mbaya hatuna na uwezo ya kumuhukumu, lakini mkubwa yake ni askofu yake. Sisi, kama tunakunywa maji, hatuwaze kama mupila pahali maji inapita ni mubaya ao ni ya zamani! Vile na kwa jambo ya mpadri moja. Tunakamata ma baraka yote toka mikono yake, kwa sababu Neema takatifu inapita na ku mikono ya mpadri hasiye na stahili na jibu mbele ya Mungu atapatia huyu na mkubwa askofu yake.

## Fumbo ya Ndoa

Ndoa ni ibada ya kuunganisha mwanamume moja na mwanamuke moja kwa jina ya Utatu Mtakatifu. Haiko uzima moja ya bure, wala sheria ya dunia, lakini ni Fumbo kubwa ya Kanisa. Mungu alibariki tangu mwanzo ya kiumbe mukusema kwa wazazi wa kwanza juu ya kuzala watoto na ya kwa kuwa wingi (Mwanzo 1,28). Tena na Bwana Yesu Kristu alibariki ndoa mujini Kana ya Galilaya (Yoane 2,1-11). Mtume Paulo alifundisha ya kama ndoa ni «Fumbo kubwa kwa jina ya Kristu na kwa Kanisa», nikusema haiko paka Fumbo kubwa, lakini ni unganisho ya watu wa wili, mwanaume na mwanamuke, mpaka mwisho ya uzima yao. Na' basi mutu asiwatenganishe wale Mungu aliowaunganisha». (Matayo 19,6).

Vile vitu ya kuonekana ndani ya Fumbo Takatifu ni ine :

1. Sikilizano katikati ya wale vijana wanataka kuowa.
2. Ya kuweka taji pa vichwa vyao kwa ile Ibada.
3. Ya kuunganisha mikono yao.
4. Baraka ya Kanisa.

Kanisa inatukuza na ma taji pa vichwa ya wale vijana sawa walivaa zamani taji ya kitawi wale watu walicheza ndani ya kiwanja na waliwina vijana weingine. Hii taji pa vichwa vyao inaonyesha ya kama hawa vijana walichunga uzima wao ubikira mpaka ile saa na Kanisa inawatukuza, kwani walijaribu kuchunga hii uzima yao takatifu. Ushindi ya kijana moja anayekuja kuowa ni hii: Ya kama alikuja kwa ile Fumbo na uzima yake usafi na ubikira. Lakini wale vijana, walianguka ku zambi ya uzini ao ya usharati mbele ya ndoa yao, wanatukuzwa na taji pa vichwa vyao, lakini kwa bure. Kanisa inawapatia baraka ya mbili, kama watakuja katika kitubio na kukamata mpango ya kama wataishi kisha uzima katika hamuri na woga ya Mungu.

Katika baraka ya Kanisa hii unganisho ya hawa watu itabaki mpaka mwisho ya uzima yao na Mungu atawasaidia kwa kutimiza kusudi ya hii ndoa yao:

1.Kusudi ni juu ya kusaidia na kutimiza mtu moja kwa mwingine juu ya kupata hawa wa wili wokovu ya nafsi yao.

2.Kusudi ya ndoa ni juu ya kuendeleshwa uzima ya watu hapa duniani na kwa kukomesha watoto wao katika mafundisho na adabu ya Bwana“ (Wafeso 6,4).

**Ma shauri ya hawa vijana wanataka kuowa:**

1.Uzima yao juu ya kuwa nzuri hawa vijana wa wili inapaswa kusaidia moja mwingine. Hivi inatokea majivuno na kila mtu anaangalia namna gani atafurahisha ndugu na mwenzake.

2.Wanajaribu hawa wili ya kutimiza moja mapenzi kwa mwingine.

3. Anakataa kumutukana bwana bibi yake, hata kama bibi yake eko mukosefu. Lakini atamushauria saa ingine, wakati na bibi na huyu watakuwa na ukimya na amani.

4. Bwana ao bibi anatafuta kupata matendo ao ma sauti mazuri ya bibi (ao ya bwana) yake juu ya kumutukuza, bila kuangalia matendo mabaya yake, kwa sababu, kama hasitafanye hivi itaonekana makelele na funjo katikati yao.

5. Kila moja anakamata mpango kuvumilia mbele ya kila mateso na magumu yao. Anaishi bila udanganyifu na anawaza ya kama Mungu ni mkubwa na atatengeneza magumu ya maisha yao.

6. Anaanganlia vitu vya maisha yake , bila kusikitika ya kama anakosa ya vitu vingi. Mbele ya vitu vya kiroho anaangalia vitu ya ngapi anakosea na hapana ma fazila ngapi eko nayo. Hivi anaishi bila sikitiko.

7. Anajaribu kila siku ya kutimia mara mengi hii sauti: „Unihurumie“. Anaomba hurumia juu ya kosa fulani yake, mbele ya bibi ao mbele ya watu weingine.

8. Anazarau udanganyifu, upumbafu na anakataa kuangalia makosa ya watu weingine. Anataka kusema ma siku zote paka kila sauti ya kweli na anajaribu juu ya kufurahisha kabisa bibi (ao bwana) yake.

9. Mbele ya kila ugomvi na funjo anaichika kusema makosa yake na anakombana ya kusimamisha ma zoezo mabaya yake.

10. Kama katikati yao hakuna masikilizano, wanakimbilia kwa mpadri ya roho yao. Wanafata sauti na shauri ya mpadri ya roho yao na hivi inafanyika mapenzi ya Mungu katikati yao.

## Fumbo ya Kupakaa na Mafuta Takatifu

Mwanzo ya hii Fumbo inaonekana ndani ya Agano Jipya, ile wakati Yesu Kristu alipatia kwa Mitume wake uwezo kwa „kufukuza mashetani na kuponyesha kila namna ya ugonjwa na uzaifu“ (Matayo 10,1). Na Mitume, wafwasi ya ma sauti ya Mwalimu wao, walirudia ku kila mwendo yao katika furaha na walisemaka: „Bwana, hata mashetani wanatutii wakati tunapowaamuru kwa jina lako“ (Luka 10,17). Kwa hivi na Mwevangelizaji Marko anasema ya kama Mitume „Kuwapakaa wagonjwa wengi mafuta, wakawaponyesha“ (Marko 6,13). Hii mapokeo iliendeleshwa na kisha ya ile siku ya Kushuka Roho Mutakatifu kwa Mitume na wanafunji wao. Kwa hivi hii Fumbo ilibaki ndani ya kanisa ya Kristu na Mtume Yakobo, Ndugu wa Bwana Yesu Kristu, aliandika ndani ya barua yake kati ya miaka 55-56): „Kati yenu kuna mutu aliye katika mateso? Aombe kwa Mungu. Kuna yeye anayefurahi? Aimbe nyimbo za sifa. Kati yenu, kuna mugonjwa? Awaite wazee wa kanisa nao watamwombea na kumupakaa mafuta kwa jina la Bwana. Na wakiomba kwa imani, mugonjwa atapona“ (Yakobo 5, 13-15).

Vile vitu vya kuonekana ni tatu:

1.Mafuta usafi.

2.Kazi ya kupakaa pa fasi ya mbalimbali ya mwili ya ule mugonjwa, na

3.Ombi ya mpadri: Ee Baba Mtakatifu, mganga wa roho na miili wewe uliyemutuma Mwana wako wa pekee…ponyesha tena mtumishi wako (jina lake) ku ugonjwa wake wa mwili na wa roho, kwa neema ya Kristu wako na umupe uzima kadiri ya mapendo yako… ».

Hii Fumbo ya Kupakaa na Mafuta inafanyika kwa watu wagonjwa na wale weko karibu ya kifo na hapana kwa mufano, juu ya kupitisha mwezi moja muzuri ao kwa kufukuzwa ma shetani ao kwa kuingia nyumbani baraka ya Mungu, kwa sababu hali ya maisha ya hawa watu ni mbaya ao juu ya magumu ingine. Lakini tunaweza kufanya Ibada Ya maji ya baraka juu ya kila ugumu na matendo mabaya ya uzima yetu. Hii Fumbo, pamoja na maponyesho ya magonjwa ya mwili, mpadri anasoma na maombi ya usameha ya zambi ya wale waaminifu wanakuja kwa hii Fumbo. Vila ansema Mt. Yakobo:«Ikiwa amefanya zambi, atasemehewa». Tunaomba usameha ya zambi, kwa sababu na Huyu Yesu Kristu alitufundisha ya kama magonjwa mengi ya mwili yanatokea kwa ajili ya zambi zetu na ya mbili kwa sababu kila zambi inaacha alama mbaya yake ndani ya ma roho na miili yetu, tena na kisha maungamo na kitubio yetu.

Mbele ya kufanya mwaaminifu moja hii Fumbo ya Kupakaa na Mafuta, inapaswa kufanya maungamo kwa padri ya roho yake.

Hii Fumbo inamalizwa katika desturi na wapadri saba, kwa sababu saba ni na somo ya Matendo ya Mitume (Apostolos) na saba ni somo ya Evangelia. Tena tunawaakisha mishumaa saba (hesabu ya saba inaonyesha ukamilifu). Kama hakuna namna ya kuonekana wapadri saba, Hii Fumbo inamazilwa na wapadri tatu hata na mpadri paka moja. Hii Fumbo inaonyesha upendo na wema ya kanisa muzima juu ya kila mugonjwa, hata kama atateswa katika roho ao mwili yake.

Ndani ya ma Kanisa ya Kristu hii Fumbo inafanyika mu Kazi tatu Mkubwa magaribi juu ya kutayarisha waaminifu mbele ya siku Kuu Kubwa ya Ufufuo ya Bwana Yesu Kristu. Vile wanafanya waaminifu wingi mbele ya Siku Kuu ya Kuzaliwa Yesu Kristu. Juu ya kufanya mukristu moja hii Fumbo, kuliko nzuri ni ya kufanya pamoja na watu weingine ya jamaa yake maungamo. Tena kisha watafanya Liturgia kimungu juu ya kukomunyika ule mutu mugonjwa. Wale waaminifu, wenye wanataka kufika kwa hii Fumbo, inapaswa kusali pamoja na watu weingine.

Kama Mungu anakataa kutimiza maombi yetu kwa hii Fumbo, hii inatuonyesha ya kama :

-Hatusadiki katika unyenyekevu ya kama Mungu anaweza kumaliza kila tendo katika uwezo wake.

-Maombi yetu haiko katika sheria na roho ya Evangelio ya Kristu. Nikusema sisi tunapaswa kusema kwa Yesu Kristu ya kumalizwa mapenzi yake na hapana mapenzi yetu (Matayo 26,39).

-Tunaomba kupita uponyesho ya mwili na hapana kabisa uponyesho ya roho yetu.

Tena tunapaswa kujua sisi ya kama Mungu anatupenda sana na iko namna hii kitu sisi leo tunaiomba Yeye iko namna kutuipatia kesho na kupita mnene! Kwa hivi na Mt. Yoane Krisostomo anasema: Iko namna sisi ya kumushukuru Mungu kupita nguvu kwa sababu hasitupatie vile vitu sisi tulimuomba na hatumushukuru kwa ajili ya vile vitu yeye aliyatupatia».

# MA IBADA YA KANISA ORTHODOKSE

Ma ibada yanaitwa ma siku ile Kanisa yetu inakumbuka matendo na ma jambo ya ajabu ya Watakatifu wetu, Ya Mzazi-Mungu Bikira Maria na ya malaika.

Ma shangilio ya Kanisa yetu yanatufurahisha katika kiroho na kimwili. Ku mwanzo ni wakati moja ya kumuabudu Mungu, ya kusoma fundisho ya Kanisa na ya kufata ma Fumbo Takatifu. Tena yanatusaidia kwa sababu yanatuunganisha pa fasi moja, ndani ya kanisa, pahali sisi wote tunasikilikwa sawa wa ndugu katika Kristu, hakuna kugawanya katikati yetu na ile siku ya shangilio wakristu wote inapaswa kutembelea wa ndugu wao wagonjwa na kufanya nguvu ya kusaidia watu wamaskini. Tena ma shangilio hizi yanatupatia wakati uhuru juu ya kupumuzisha mwili yetu kwa muchoko ya juma muzima na yanatukumbusha uzima ya milele ya kama sisi hatutaishi hapa kwa milele, lakini siku moja tutakufa kufatana ma sheria ya mtu ya hii dunia.

Mwaka ya ma siku Kuu ya Kanisa inaanza tangu mwanzo ya mwezi Septemba na inakamata ma shangilio hapana paka ya kutengwa sawa, shangilio ya Mtakatifu Dimitrios (mu tarehe ya 26 Oktoba), ya Kuzaliwa Kristu (mu tarehe 25 ya Desemba) ao ya Kulala Mzazi-Mungu (mu tarehe 15 ya Augusti) lakini iko na na shangilio ya kujitenga. Nikusema kila mwaka shangilio ya Watakatifu ni ya wakati ingine. Kwa mufano Siku Kuu ya Ufufuo ya Kristu kila mwaka ni ya wakati ingine. Hii kitengo ya ma Siku Kuu ya Watakatifu inatokea ku mpango ya Watakatifu wapadri ya Makutano ya Kwanza ya Ulimwengu ku mwaka 325, kisha kuzaliwa kwa Kristu. Wale Watakatifu walisema ya kama tutakuwana kila mwaka Pasaka mu Juma ya kwanza kisha Panselinos (ile siku muezi inaonekana muzima mbinguni) ya tarehe makumi mbili na moja (21 ya Mwezi ya tatu. Kwa sababu Panselinos haiko kila mwaka ndani ya siku moja, kwa hivi ma shangilio ile wakati yanatengwa. Ma shangilio yenye ni ya kutengwa ni mu wakati mbili. Ku mwanzo ni ndani ya wakati ya Triodi (mbele ya Pasaka) na mu wakati ya Pentikostari (kisha Pasaka) ma siku makumi tano (50).

Tukona Kanisani yetu ma Shangilio ya Bwana Yesu Kristu, yenye yanaitwa Despotikes na ingine ya Mzazi-Mungu, yenye yanaitwa Theomitorikes. Tena tukona shangilio ya Musalaba ya Kristu na ya Watakatifu. Ma shangilio ya Watakatifu ni juu ya Mt. Yoane Mutangulizi na Mubatizaji, juu ya Mitume, Mashahidi, Watawa, waaskofu, Manabii na ma kundi ya Watakatifu ingine.

Kila shangilio ya Yesu Kristu na ya Muzazi mwake inashangiliwa hapana paka siku moja, lakini ma siku tatu, kwani kila shangilio inaanza siku moja mbele ya ile siku ya ukubusho yake na inaendelea na siku moja kisha ile siku ya shangilio yake. Tena kisha juma moja tunaimba mara ya mbili hii Ibada ya shangilio ya Yesu ao ya Mama mwake na hii inaitwa Sindikizo, mu lugha kigreki Apodosis.

## Ma siku Kuu ya Bwana wetu Yesu Kristu.

1.Habari Njema ya Mzazi-Mungu mu tarehe 25 ya mwezi ya tatu (Martie). Ni siku Kuu bila kutengwa.

2.Kuzaliwa kwa Kristu, mu tarehe 25 ya Mwezi Desemba. Siku Kuu bila kutengwa.

3.Kupokelea Symeoni Yesu Kristu Hekaluni, mu tarehe 2 ya mwezi ya Februarie.

4. Ya kuoenakana Yesu Kristu (Epifania ya Kristu), mu tarehe ya 6 Yanuarie. Ni bila ya kutengwa.

5. Hekima ya Yesu Kristu. Ni Siku Kuu ya Kati ya Pentikosti. Ni Siku Kuu ya kutengwa.

6. Mageuzo ya Sula ya Bwana Yesu Kristu, mu tarehe 6 ya mwezi ya Augusti. Bila kutengwa.

7.Ufufuo ya Mt. Lazaro. Siku Kuu ya kutengwa.

8. Kuingia Yesu Kristu mujini Yerusalema. Mu Juma ya Matawi. Siku Kuu ya kutengwa.

9. Mateso na Usulubio ya Yesu Kristu. Siku Kuu ya kutengwa.

10. Ufufuo ya Bwana wetu Yesu Kristu. Siku Kuu ya kutengwa.

11. Kupanda Yesu Kristu mbinguni. Siku Kuu ya kutengwa. Ma siku makumi ine kisha Ufufuo ya Kristu.

12. Pentikosti. Siku ya Kushuka Roho Mtakatifu. Ma siku makumi tano kisha ya Ufufuo ya Kristu. Ni Siku Kuu ya kutengwa.

Na ma siku Kuu ya Musalaba ni ma shangilio ya Yesu Kristu. Siku Kuu ya musalaba tukona tano:

1. Ya kupanda Musalaba, mu tarehe kumi na ine ya mwezi ya Septemba ku Mtakatifu Helena ku mwaka 326, kisha uzalio ya Kristu.

2. Kupandisha Musalaba mara ya mbili. Ile wakati mufalme ya Konstantinopoli Iraklios aliwina taifa ya Persia ku mwaka 626 na alimurudisha Musalaba ndani ya muji Yerusalema.

3. Ya kupata Musalaba mu tarehe 6 ya mwezi ya Martie (Tatu), lakini kwa sababu ile wakati ni Kwarezima, kanisa alipeleka hii shangilio mu Juma tatu ya Kwarezima. Ile Juma tunasujudu Musalaba ya Kristu.

4.Ukumbusho ya kuonekana mbinguni alama ya Musalaba juu ya mujini Yerusalema mu Juma ya Pentikosti ya mwaka 351, asubui saa ya tisa. Inashangiliwa mu tarehe ya 6 ya Mwezi ya Mai (Tano).

5.Ukumbusho ya kujuguluka Musalaba Takatifu ndani ya ma kanisa yote ya muji Konstantinopoli na usujudu yake tangu mwanzo mpaka mu tarehe kumi na tatu.

## Ma siku Kuu ya Mzazi-Mungu

1.Kuzaliwa kwa Mzazi-Mungu, mu tarehe ya mnane ya Septemba.
2.Kuingia Hekaluni Mzazi-Mungu, mu tarehe ya makumi moja ya mwezi Novemba.
3. Habari Njema ya Mzazi-Mungu, mu tarehe makumi mbili na tano ya Mwezi Martie (Tatu).
4.Ya kumupokelea Symeoni Yesu Kristu Hekaluni, mu tarehe ya mbili ya mwezi Favruarie.
5. Kulala kwa Mzazi Mungu, mu tarehe kumi na tano ya mwezi ya Augusti.
6. Ya kupata mimba Mt. Anna kwa Mzazi-Mungu Maria, mu tarehe ya Tisa ya mwezi ya Desemba.
7.Mufuniko ya Mzazi-Mungu, mu tarehe mwanzo ya Mwezi Oktoba. Hii Shangilio iliingia tangu ku mwaka 886, wakati mtakatifu Mutawa Andrea mazimu katika Krikstu, pamoja na mwanafunji wake Epifanios alimuona Mzazi-Munbgu Maria ndani ya kanisa ya Vlahernes ya kufunika na Maguo yake takatifu waaminifu wote, waliyokuwa ndani ya Kanisa.
8.Ma shangilio ingine ya kidogo ya Mzazi-Mungu ni ya kuweka Kanzo Takatifu ya Mzazi-Mungu Maria ndani ya kanisa ya Vlahernes, ku mwaka 473, mu tarehe ya 2 mwezi ya saba (Yulie).
9. Ya kuweka Musipi takatifu ya Mzazi-Mungu Maria Kanisani ya Khalkopratia, ku mwaka 530 ya tarehe 31 mwezi ya Augusti.

### Ma shangilio ya Watakatifu

Angalia mu sehemu „Watakaitfu ya Kanisa", mu ukurasa ....

## Kundi ya ma shangilio ya juma moja muzima

Bila tuu ya shangilio ya mwaka muzima, tukona na ma shangilio ya Watakatifu ya mu juma. Nikusema tunashangilia Watakatifu filani siku moja ya juma muzima. Pahali mu wakati ya dini ya Ebrania watu wa Israeli walisifu siku ya Sabbato (Posho), sisi Wakristiani tunabadilisha siku Kuu ya Mungu na tunasifu siku ya mu Juma. Kwa hivi tukona:

1. Mu Juma. Ni siku ya Ufufuo ya Bwana Yesu Kristu. Tangu magaribi tunatayarishwa sawa wale wanawake wamabaji manukato (Mirofori) juu ya kumupokelea Kristu kwa Komonyo Takatifu.

2. Siku ya mu Kazi Moja inajitolea kwa majeshi yote ya Malaika. Tunaomba saidio yao juu ya kusihi na sisi katika roho ya uzima ya wa malaika.

3. Siku ya mu Kazi Mbili inajitolea kwa Mt. Yoane Mutangulizi na Mubatizaji. Mt. Yoane anatuonyesha Mwana Kondoo wa Mungu.

4. Siku ya mu Kazi Tatu inajitolea kwa mateso ya Bwana Yesu Kristu (masikilizano ya makuhani ya dini ya Waebrania pamoja na Yudasi, mwanafunji ya Kristu). Tena hii siku tunashangilia na Mzazi-Mungu Bikira Maria, aliyepatia sawa deni mwili yake Kwa Neno Yesu Kristu na hivi sisi tunaweza kukomunika Mwili na Damu Yake.

5. Siku ya mu kazi Ine, inajitolea kwa Mitume na kwa wa askofu, halafu kabisa kwa ukumbusho ya mt. Nikolao, mufwasi ya Muchungaji Muzuri Yesu Kristu.

6. Siku ya mu Kazi Tano, inajitolea kwa kumbuka sisi mateso na lufu matata ya Yesu Kristu. Toka ubavu yake yalatokea maji na damu juu ya kuweza sisi kubatizwa ndani ya maji na kupewa Mwili na Damu ya Kristu.

7.Siku ya Posho inajitolea kwa mashahidi na kwa wafu, ikiwa lufu hakuna namna ya kutuachanisha, kwani ndani ya Komonyo Takatifu sisi wote tunaunganishwa na tunafanyikwa mwili moja ya siri. Ni Mwili ya kanisa ya Yesu Kristu.

# IBADA YA TRIODI

Triodi inaitwa Kitabu moja ya Kanisa Orthodokse na inakuwa na wimbo ya sala ya Magaribi (Njioni) na ya asubuyi na inajitimia pempeni ya Vitabu ya Mineo (Wimbo ya Watakatifu ya kila mwezi) na Kitabu ya Paraklitiki (wimbo ya Ufufuo ya Kristu na ya kutubu). Kitabu ya Triodi iko na wimbo ya wakati ya Kwarezima, mbele ya Ufufuo ya Kristu.

Triodi inagawanya kwa wakati tatu :

1.Wakati ya kwanza inaanza ku siku ya Mungu ya Mufarisayo na Mutozakondi mpaka mwazno ya Kwarezima, nikusema ni ya ma siku makumi mbili (22).

2.Wakati ya mbili ni toka mwanzo ya kwarezima mpaka siku Kuu ya Matawi.

4. Kutoka Siku Kuu ya Matawi mpaka muposho Mkubwa, siku moja mbele ya Pasaka.

Inaitwa Triodi, kwa sababu ma Kanuni yote weko na kundi ya wimbo tatu na hapana mnane ao tisa sawa ni zoezo. Hii wakati ya Triodi inataka kutayarishia roho yetu katika kizila na kitubio kwa kumupokelea Mateso takatifu na Ufufuo kitukufu Yake.

Wakati ya kwanza iko na ma siku ya Mungu inne: Kwa ile Siku ya Mungu ya kwanza tunakumbuka mufano ya Mufarisayo na Mutozakodi.

Ile siku ya Mungu mpadri anasoma mufano ya Mufarisayo aliyesali na majivuno mbele ya Mungu lakini sala ya ule mutozakodi ilipanda mbinguni na Mungu aliipokelea.

Kwa hii mfano ya ule mufarisayo Kanisa yetu inataka kutufundisha juu ya kufata na sisi mufano ya mutozakodi na hapana mfano ya mufarisayo. Paka unyenyekevu inaweza kutuchunga bila kuanguka kwa zambi. Na Mtakatifu mutawa mkubwa Antonio aliangalia mitego yote ya kuwa chini ya kiwanja moja na alimuuliza Malaika aliyekuja kwake anni ataweza kupitisha mitengo haya yaote ? Na malaika alimujibu : «Paka unyenyekevu»!

Mu kazi tatu na mu Kazi Tano ya hii juma tunakula chakula yoyote, hatufanye kizila.

Siku ya Mungu ya mbili inaitwa ya Mwana mupotevu. Hii mufano inatufundisha juu ya kijana moja aliyeharabisha makuta na mali ya baba yake na alifika pa hali mbaya juu ya kuchunga nguruwe. Ile saa alitubu na alirudia nyumbani mwake, pahali baba alimupokelea na upendo na wema.

Maana ya hii Mufano ni mnene. Tunaangalia pa fasi gani chini anaweza kufika mtu moja kama ataishi bila kumuogopa Mungu.

Kisha inalazimishwa kitubio juu ya kuweza kurudia mtu moja. Tena ndani ya hii mufano inaonekana ma zawadi ya kiroho ya ule mutu anayetaka kutubu ya kweli. Tena ndani ya hii mufano inaonekana wema kubwa ya Mungu Baba wetu na hivi hata mtu moja haipaswe kupotesha kitumaini yake. Hata zambi moja, japo ni kubwa kabisa, hakuna namna ya kufupisha wema na upendo ya Mungu. Tena tunaangalia ndani ya hii mufano tabia mbaya ya ndugu mkubwa, aliyesadiki ya kama eko mtu mwenye haki na alikuwa stahili ya kupata kila zawadi na furaha toka baba yake. Inatufundisha mufano yake ya kama na sisi, haipaswa kusadiki ya kama tutaokolewa, kwa sababu tuko wakristiani ao kwani tunaingia kila mu siku ya Mungu ndani ya Kanisa. Hatujue namna gani Yesu Kristu atatuhukumu. Kisha wokovu ni zawadi yake, lakini inasaidia na mapenzi ya ule mutu anayetaka kuokolewa.

Kama tutasadiki ya kama sisi wote tuliharabisha mazawadi yote ile Mungu alitupatia, kwa ajili ya zambi zetu, tutasikia ya kama sisi wote hii siku tuko wana wapotevu, kwa sababu tuliondoka mbali ya nyumba Ya Baba Mungu wetu.

Hii juma mu kazi Tatu na mu kazi tano tunachunmga kifungo ya chakula katika desturi ya Kanisa yetu.

Muposho, siku moja mbele ya siku tatu ya Munguy, inaitwa Sabbato ya wafu. Tukona ma Sabbato ya wafu mbili. Moja ni leo na ingine ni mbele ya siku ya Mungu ya Pentikosti. Juu ya nini Kanisa yetu inasimamisha hii siku ya wafu? Kwa sababu katikati ya ma karne yote walikufa watu weingine ndani ya bahari, wengine mulimani na weingine, kwa ajili ya umaskini yao hawa-stahiliwa kuwafanyishia ibada ya ukumbusho na maondoleo ya zambi zao. Tena kwa sababu kesho, siku ya Mungu ya Apokreo tunashangilia siku ile ya Uhukumu mbele ya Mungu, tunamuomba Mungu kwa makumbusho haya juu ya kupokelea na wema hawa wafu na kuwapatia pumuziko ya nafsi yao. Tena na sisi, kama tunafanya hii Ibada ya wafu, tunakumbuka siku ya lufu yetu na tunalamuka kw akutubu ya kweli…

**Siku ya tatu ya Mungu inaitwa ya Apokreo**

Hii siku ya Mungu inaitwa hivi kwa sababu hii siku tunakula mara ya mwisho nyama mpaka ile siku ya Ufufuo ya Yesu Kristu, ila tu ya wale wa ndugu weko wagonjwa. Hii siku ya Mungu Watakatifu wetu waliweka somo ya Evangelio ya kukumbuka sisi ujio mara ya

Mbili Yesu Kristu nduniani juu ya kuhukumu watu wote. Ile siku ya mwisho ya uzima yetu itafanyika uhukumu ya kwanza na uhukumu ya mwisho itafanyika ile siku atakuja Bwana Yesu Kristu ya kuhukumu ulimwengu nzima.

**Siku ya Mungu ya ine inaitwa ya Jivini**

Mbele ya siku moja ni Sabbato na Watakatifu wetu waliweka ukumbusho ya Watakatifu wote, wale walitukuzwa jangwani sawa watawa, wale walikuwa wa askofu, wa shahidi na weingine wote.

Hawa Watakatifu ni mifano mazuri ya ushindani ya kiroho na ya kitubio na wanatusukuma kwa kufata na sisi mifano na uzima kitakatifu wao. Hii Sabbato inaitwa Sabbato ya Watakatifu wote.

Siku ya Mungu ya ine inaitwa ya Jivini na maana yake ni ya kama ma siku haya tunakula kila siku mayayi na maziwa ya kulamata. Hii Juma hatukula nyama ao kuku, lakini tunakula matunda yao, maziwa na mayayi, kwa sababu Kanisa yetu inaachanisha ma chakula ya ile niko na nguvu na ingine bila kuwa na chakula ya nguvu.

Hii siku ya Mungu tunasoma Evangelio ya kukumbula sisi hawa wazazi wa kwanza Adamu na Eva, aliwafukuza Malaika Mihaili kwa sababu walikanyanga hamuri ya Mungu. Tunda ya hii kosa yao ilikuwa ya kama walifukuzwa inje ya Paradizo. Na Kanisa yetu sasa anatuita, kama tunataka kurudia paradizoni, tunapaswa kuishi katika kitubio, unyenyekevu, utii na kizila.

Magaribi ya hii siku ya Mungu ndani ya ma kanisa yote ya Orthodoksi inafanyika Sala ya Magaribi ya Usamehe. Nikusema ku mwisho ya hii Ibada, mpadri anahubiri juu ya kutubu, anaomba huyu ya kwanza usamehe mbele ya waaminifu yake na kisha anasimama mbele ya Ikonostasi (Fasi katikati ya Altari na ile fasi wanasimama Waaminifu) ya kukamata pa mikono yake Evangelio na wanapita waaminifu wote. Wanabusu Evangelio, wanaomba hurumia na wanasimama pempeni yake. Kisha waaminifu weingine wanakuja wanafanya vile vile na wanaomba hurumia katikati yao moja ku mwingine mpaka itaisha hii mustari ya waaminifu wote.

Mpadri atabadilisha manguo Takatifu ya Meza. Atatosha meupe na ataweka nyekunda. Hapana meushi kwa sababu tunamuliliya Yesu Kristu hapana sawa mutu aliyekufa kwa milele, lakini sawa Mungu aliyefufuka. Ku mwisho ya hii Ibada ya Njioni mpadri pamoja na waaminifu wote wanasali kusema hii sala ya Mtakatifu Efremi wa Syria : Ee Bwana na Rabi ya uzima yangu… roho… ». Kama tunasali hivi, tunafanya pamoja na metania tatu (kupiga magoti). Kisha metania kidogo, kumi na mbili na ku mwisho metania moja kubwa.

## Kwarezima Kubwa

Kutoka mu kazi moja, kisha siku ya ine ya Mungu, inaanza wakati ya Kwarezima Kubwa. Ni wakati ya mafungo nguvu ya chakula, somo ya ma Ibada mengi ndani ya Kanisa na matayarisho ya roho nguvu katika sala na kitubio.

Watakatifu ya Makutano Ikumeniki ya Kwanza ku mwaka 325 kisha kuzaliwa kwa Kristu alikamata mpango juu ya kufanya waaminifu wetu kizila ya ma siku makumi inne, sawa na Bwana Yesu Kristu aliishi na kifungo ya chakula jangwani ma siku makumi inne.

Tunafunga chakula juu ya nini? Mtakatifu Yoane Krisostomo anasema hivi Tunafanya kizila hapana kwa Usulubisho ao kwa Ufufuo ya Kristu, lakini kwa ajili ya zambi zetu.

Hii wakati inaitwa Kubwa, kwani ma shangilio ile tunashangilia ni makubwa, sawa Mateso na ufufuo ya Kristu. Na mambo ya mbili, kwa sababu hii Kwarezima ni kupita ukali mbele ya Kwarezima ya Kuzaliwa Kristu, kwa sababu kila siku hatuykula chakula na mafuta, ila tu muposho na mu juma (siku ya Mungu). Ni kweli ya kama hii kifungo wanafata paka hawa wenye afya. Hawa wandugu wekona mambo ya afya yao, kwa baraka ya mpadri ya roho yao, wanaweza kula katika sauti yao. Kizila inasaidia mukristu juu ya kumutosha mazoezo mabaya na ma zambi zake na hapana ya kumuua mwili yake.

Ile siku ya kwanza ya Kwarezima inaitwa mu Kazi moja usafi, kwa sababu hii siku hatukule kitu. Tunafata ma ibada yote ndani ya Kanisa na magaribi tunasoma mara ya kwanza Ibada ya Apodipno Kubwa. Apodipno Kubwa tunasoma kila siku, ila tu mu Kazi tano, kwani hii siku tunasoma Ibada ya Apodipno Kidogo, pamoja na kanuni ya Mzazi-Mungu Mwimbo Akatisti yake. Hii Ibada inaitwa Apodipno, kwa sababu, katika desturi tunaisoma kisha chakula ya magaribi.

Inaitwa kubwa juu ya kuichanishwa toka Apodipno kidogo. Ile wakati ya kwarezima Apodipno kidofo tunasoma mu kazi tano, muposho na mu siku ya Mungu mangaribi.

Ile wakati ya Kwarezima tunafanya na Liturgia ya Proigiasmeni, kwa sababu zamani waaminifu walipewa Mwili na Damu ya Kristu mara tatu ao ine kila juma. Mwili ya Yesu Kristu iliisha kutakaswa kwa siku ya Mungu ile iliyepita. Maana yake Proigiasmeni ni hii: Ya kama Mwili ya Kristu ilikuwa ya kutakaswa tangu mu Juma iliyepita. Iliingia hii desturi ya Liturgia hii kati ya Kwarezima kwa sababu inakatazwa ya kufanya wapadri Liturgia ya Mt. Yoane, kwani hii Liturgia ikona hali ya furaha ya Ufufuo ya Kristu, lakini Liturgia Proigiasmeni ikona hali ya sikitiko. Liturgia ya Mt. Yoanne Krisostomo ile wakati tunafanya paka kila muposho na kwa siku ya Bwana (mu juma). Hii Liturgia inaunganishwa pamoja na ibada ya Magaribi. Na inafanyika mara mbili kila juma.

Mbele ya kwanza hii Liturgia tunasoma Saa ya Tisa. Mpadri kisha ya kusema : Ahimidiwa ufalme wa Baba… » kisha anasoma Ombi Kubwa (Sinapti) ya sala ya Magaribi.

Wakati msomaji anasoma Zaburi, mpadri ndani ya Altari anatosha toka Meza (Artoforio) sanduku takatifu pahali inachungwa Mwili ya Kristu) na anamupeleka pa Meza ya Proskomidi (Matayarisho), juu kisha ya kumaliza Kujuguluka kati ya kanisa pamoja na Vitu Vitakatifu, yenye yaliisha kutakaswa.

Kwa Kuingia Kubwa mpadri anapeleka Vitu Vitakatifu na waaminifu wote wanapika magoti na wanainamisha vichwa vyao chini mpaka bulongo na ndani wanasali hivi: «Kwa maombezi ya Watakatifu wapadri wetu, ee Bwana Yesu Kristu Mungu wetyu, utuhurumie na utuokoe».

Kama mpadri anafanya Liturgia Proigiasmeni hasikumbuke ma jina ya wafu na wenye muzima kwa Proskomidi wala ndani ya Liuturgia. Tena ndani ya hii Liturgias hatufanye makumbusho ya wafu. Trisagio tunaweza kufanya kisha mwisho ya Liturgia.

## Siku ya Mungu ya Kwanza ya Kwarezima ao ya Orthodoksia

Hii Siku ya Mungu inaitwa na siku ya Mungu ya Orthodoksia, kwa sababu hii siku tunashangilia ya usimamisho ya ma Picha Mtakatifu ya Watakatifu na utukufu ya Imani Ortodokse mbele ya mafundisho ya uwongo, nikusema mbele ya wale walikataa kubusu na kuheshimiwa ma Picha ya Watakatifu.

Hii nvita ya kupingana ma Picha ya Watakatifu ilikuwa mujini Konstantinopoli kupita juu ya miaka miya moja. Na kisha bibi ya mufalme Theofilos, jina lake Theodora pamoja na mtoto mwake Mihaili alisimamisha ma Picha pa fasi yao. Hii siku Kuu tunaikumbusha sisi hii siku ya kujuguluka pempeni ya Kanisa na kwa kukamata pa mikono yetu ma Picha ya Watakatifu na tunaimba mwimbo ya hii Siku Kuu. Fundisho moja ya ajabu kabisa sasa tunapaswa kuandika ya kama sisi waortodoksi tunabusu Picha ya Bwana Yesu Kristu, kwa sababu tunamuabudu Huyu sawa Mungu na Baba wetu, lakini tunabusu ma Picha ya Watakatifu, kwani tunaonyesha sifa, upendo na heshima mbele yao sawa wa ndugu wakubwa wetu,. Wenye walitakaswa na waliingia Paradizoni kwa kumuomba Mungu juu ya wokovu wetu. Kitu ingine ni kuabudu Mungu na kitu ingine ni kusifu na kuheshimiwa picha moja ya Mtakatifu fulani.

## Fundisho ya ma Picha ya Watakatifu

Hata mtu moja hasikuone na hasiweze kumuona Mungu Baba. Lakini Mungu anafamiana kwa Picha yake na kwa ujio ya Mwana wake Yesu Kristu, kwani Huyu ni sura ya Mungu mwenyewe" (Barua ya mbili kwa Wakorinto 4,4). Kusujudu ma Picha ya Watakatifu ni fundisho ya kanisa yetu na ilisimamishwa kwa Makutano Ikumeniki ya Saba ku mwaka 787 kisha kuzaliwa kwa Kristu. Kanisa Orthodokse inaheshimiwa kila Picha ya Watakatifu, kwani usujudu ya mukristu moja inaenda kwa nyuso ya huyu Mtakatifu na hapana kwa ragi ao kibao ya hii picha.

Ma Picha ya Watakatifu wanafanya na miujiza. Hii sauti ni ya kweli? Watu weingine wanasadiki ya kama muujiza inafanyika kwa imani ya waaminifu, wenye wanasali mbele ya ma Picha. Ya kama imani inafanya miujiza, haiko shaka. Halafu ni na ma picha yenye yanafanya miujiza. Zawadi ya kufanya miujiza Bwana Yesu Kristu aliwapatia kwa Mitume, lakini na kwa kimvuli yao! Vile inaandika Mandiko Takatifu ! (Matendo ya Mitume 5,12-15). Watu walileta wagonjwa pa vitanda vyao na waliwaweka mbele ya Mtume Petro juu, hata kama itapita juu yao hata kimvuli yake, walisadiki, ya kama wataponyeshwa! Tena na vitambaa ya Mtume Paulo, waliyaweka pa vichwa vya

wagonjwa ao wenye kuwa na shetani ndani yao na waliponyeshwa! (Matendo ya Mitume 19,12). Na sisi wote tunasikia ya kama ilikuwa wema na upendo ya Mungu na hapana vitambaa yalikuwa na nguvu kimoja kimungu. Lakini hapa tunaweza kusikia ya kama uwezo ya Mitume ilifika mpaka na vitambaa yao yalifanya miujiza!

## Siku ya Mungu ya Mbili ya kwarezima

Hii siku Kanisa yetu inashangilia ukumbusho ya Mtakatifu Grigorio Palamas, askofu mkubwa ya muji Thesaloniki ya Uyunani (Grece). Huyu alikuwa mwalimu mkubwa ya mafundisho ya Kanisa ya Kristu na alihuibiri na alisimamisha kabisa fundisho ya neema ya Roho Mtakatifu. Kwa hivi anaitwa na muhubiri ya Neema Takatifu. Neema ya Mungu sawa nguvu kwa wokovu ya kila mukristu haiiko ya kuonekana sawa vile vitu vya dunia yanayoonekana. Lakini ni nguvu kimungu bila kuonekana na ma macho ya mwili yetu. Neema ya Mungu inakaribia kwa mukristu moja, kama huyu anakaribia na anafata ma Fumbo Takatifu ya Kanisa Orthodokse. Paka hivi mukristu moja anaweza kuokolewa na kutakaswa....

Mtakatifu Grigorio alizaliwa na alikomea mujini mkubwa ya Konstantinopoli mu karne kumi na tatu. Wakati alikuwa kijana aliingia Mulimani Takatifu. Kisha alikombanisha fundisho ya uwongo ya mutawa moja katholike, jina lake Varlaamu, aliyezarau neema ya Roho Mtakatifu na alichekelea uzima ya kiroho ya Watawa ya Kilima Takatifu. Patriarhi ya Konstantinopoli alifanya makutano ku mwaka 1341 na 1347, pahali alikuwa na mt. Grigorio na walihukumu mafundisho ya uwogo ya ule mutawa Katholike. Ku mwaka 1346 alifanyika askofu ya muji Thesaloniki ya miaka kumi na tatu (13) na alikufa ku mwaka 1359 na umri yake miaka 63. Maiti Takatifu yake ni muzima ndani ya Kanisa mkubwa yake ya muji Thesaloniki.

## Siku ya Tatu ya Kwarezima
## (Siku ya Kusujudu Musalaba ya Kristu)

Hii Siku ya Mungu ni katikati ya hii wakati ya Kwarezima na Kanisa yetu inasimamisha mbele yetu Musalaba wa Kristu. Juu ya nini? Kwa sababu wakristiani waliisha kuchoka kwa ajili ya ushindani ya roho na kizila nguvu na Kanisa anaweka katikati yetu Musalaba ya Kristu juu ya kupata nguvu na ya kuendelesha ushindani yetu ya kiroho mpaka mwisho ya hii Kwarezima. Musalaba inatupatia furaha, uvumilia, kitumaini na nguvu kimungu juu ya kuendelesha uzima yetu ya kiroho. Kwa hivi hii siku tunaimba pa fasi ya mwimbo: Mungu Mutakatifu...“. „Musalaba wako tunasujudu, ee Rabi, na Ufufuo wako Takatifu, tunatukuza“. Huyu mukristu anayejua nguvu ya Musalaba anaenda kanisani, anaibusu, anaomba saidio yake ile inatokea toka Yesu Kristu, anavaa Musalaba pa kifuo yake na hasiende kufata ma shauri ya walozi na ya wafumu.

Katika desturi ya Monasteri ya mtakatifu Savvas, karibu ya muji Yerusalema, usujudu ya Musalaba tunafanya hapana paka hii siku ya Mungu, lakini na mukazi tatu na mu kazi tano.

## Siku ya Mungu ya Ine ya Kwarezima

Leo tunashangilia ukumbusho ya mt. Yoane, mwandishi ya kitabu "Mugazi ya mafazila Takatifu". Huyu alikuwa muhubiri ya toba na kifungo ya chakula. Alizaliwa mu inchi Palestini karibu ku mwaka 523 kisha kuzaliwa kwa Kristu. na tangu kipimo udongo yake alikuwa mwaminifu kabisa. Alifanyika mpadri mkubwa ya monasteri ya Mt. Ekaterini pa mulima Sinaya na aliandika mahubiri makumi tatu juu ya uzima ya kiroho. Hii kitabu inaitawa Mugazi ya ma fazila. Alikufa ku mwaka 603.

Ukubusho yake ni mu tarehe ya 30 ya mwezi ya Tatu, lakini tunamushangilia na leo juu ya kufata sisi mufano na ma fazila yake. Hii wakati ya Kwarezima tunasoma ndani ya Kanisa, kabisa ndani ya monasteri mahubiri toka kitabu yake. Hii juma inafwata tunasoma Kanuni kubwa ya kutubu ya mt. Andrea askofu ya kisanga Kreta. Tenashangilia na Akathisto Ymno, nikusema wimbo ya Mzazi Mungu.

## Siku ya Ine

Siku ya Tatu magaribi, kati ya ma juma ya Ine na ya tano ya Kwarezima, tunaimba ndani ya Kanisa Ibada ya Kanuni kubwa, katikati ya Ibada ya Apodipno Kidogo. Hii Kanuni ni kubwa kwani iko na wimbo yote 250! Mwandishi aliyeandika hii Kanuni alikuwa mt. Andrea, mutawa ya Monasteri ya Mt. Savvas, karibu ya Yerusalema. Kisha alikuwa askofu mkubwa ya Kreta. Alikufa karibu ku mwaka 740, mu kisanga Lesvos, wakati alirudia toka muji Konstantinopoli.

Fundisho ya wimbo haya ni uzima ya watu wakubwa wote ya Agano la Kale. Lakini maana kubwa ndani ya hii Kanuni ni toba. Hii toba ni mulango ya kuingia mtu moja ndani ya Paradizo. Kwa sababu hatuna na matunda ya kitubio, tunapaswa kumutoa kwa Mungu paka roho ya kuvunjika kwa ajili ya ukumbusho ya zambi zetu. Maana yake kabisa tunaipata ndani ya Kontakio yake. Ni Hii: " Ee roho yangu, roho yangu, amka, sababu gani kulala, gani kulala hivi? Kwani tazama, mwisho umekaribia, na utasamba ku hukumu. Tubu, basi, ee roho yangu, ili Kristu Mungu akusemehe, yeye aliye popote mu ulimwengu wote anayejaza kuwako kwake".

## Akathistos Ymnos
## (Mwimbo ya Mzazi-Mungu)

Mu wakati ya Kwarezima kati ya ma juma ya ine tangu mwanzo, kila siku ya tano magaribi, katikati ya Ibada ya Apodipno Kidogo, tunaimba kipande moja-moja toka hii Ibada ya mzazi-Mungu. Ku mwisho ya kila kipande tunaimba: "Salabu Bibi Arusi usiolewa na Aliluya". Hii Himnos Akathistos tunaimba muzima ndani ya Ibada ya asubui ya Sabbato, mu juma ya siku ya tano.

Wimbo ya kwanza yanaanza na shangilio ya Habari Vema ya Mzazi-Mungu. Kisha yanatukumbusha kupata mimba Mama Bikira Maria, kisha tembeleo yake kwa Elisabeti, mawazo ya Yosefu juu ya kumufukuza Mama Bikira Maria, kisha usujudu ya wenye akili tatu na wachungaji, kisha yanatukumbusha kimbilio ya Yosefu na Mama maria na mtoto Yesu kwa inchi Misri na kisha pokeleo ya Yesu Kristu Kanisani ya Solomono ku Nabii mkubwa Symeoni.

Ndani ya kipande ya mbili, nikusema mpaka mwisho wimbo yanatufundisha namna gani mtu moja anaweza kutakaswa na utukufu na sala ya Mzazi-Mungu.

Juu ya nini hii Ibada ya Mzazi-Mungu inaitwa Akathistos Ymnos? Kwa hii jambo: Ku mwaka 626 muji Konstantinopoli walitaka kuikamata adui Avari na taifa ya Persia toka bahari na ulongo. Mufalme jina lake Iraklios alikuwa ya kufukuza wa adui weingine ndani ya Azia. Hatari ya muji Konstantinopoli ilikuwa mnane. Mkubwa sasa juu ya kuokoa muji alikuwa patriarchi Sergios. Huyu pamoja na wapadri weingine na wa askari kidogo, pamoja na taifa yote walisali juu Mungu ya kuoka muji na uzima yao. Walitumainia kwa Mama Mzazi-Mungu. Na, o muujiza ya ajabu! ile usiku pepo moja nguvu, iliharabisha ma chombo ya wa adui na hawa walikimbia, lakini weingine wingi walikufa ndani ya bahari. Muji iliokolewa kwa sala na ulinzi ya Mzazi-Mungu. Ilikuwa tarehe ya 8 mwezi ya mnane ya mwaka 626. Ile usiku, kisha saidio ya Mzazi-Mungu waaminifu wote ndani ya kanisa kubwa walisimama na waliimba hii Ibada. Maana yake Akathistos, ni ya kusali bila kuikaa, nikusema pa miguu.

## Siku ya Mungu ya Tano ya Kwarezima

Hii siku ya Mungu tunashangilia ukumbusho ya Mt. Mutawa Maria wa Misri. Japo huyu anashangiliwa na mu tarehe ya mwanzo ya mwezi ya Aprilie, lakini tunamushangilia na hii siku juu ya kusaidia hawa wazaifu ya kusimama kuendelesha hii ugomvi ya kiroho.

Huyu Maria tangu kipimo 12 ya uzima yake aliishi uzima mbaya ndani ya zambi ya mwili. Ku umri yake miaka 29, aliendа mujini Yerusalema juu ya kubusu Musalaba ya Yesu Kristu. Lakini hasikuweze kuingia, sawa waaminifu weingine. Alisikia ya kama nguvu moja ya ajabu ilimuzibiliya. Alisikia zambi zake na alikamata mpango juu ya kubadilisha uzima yake. Kwa hivi, kwa saidio ya Mzazi-Mungu alibusu Musalaba ya Kristu na aliondoka jangwani, pa ngambo mbali ya muto Yordani, pahali aliishi huyu wa pekee miaka 47! Ndani ya miaka 17 yenye ya kwanza alikuwa magumu na majaribu mengi, lakini miaka ingine 30, aliishi sawa malaika wa Mungu! Mwana moja, mbele ya kifo yake, alimutembelea mutawa mpadri Zosimas. Mbele yake alifanya maungamo,

alipewa Takatifu Komonyo na kisha alirudia jangwani, pahali ile usiku alikufa. Hii wakati ya miaka 47 ndani ya jangwa hasikutana na hasizungumuze na mtu mwingine. Alijua Biblia Takatifu, bila kuisoma, hata mara moja! Alitembea sawa roho juu ya maji ya muto Yordani na Mungu alimupatia zawadi juu ya kujua ma tangazo yote, mbele ya utimizo yao! Ile siku alikomunyika, alikufa inje ya pango yake. Kisha mwaka moja alikuja mpadri Zosimas alimupata muzima maiti yake na, bila kujua ya kuandika, aliandika chini pa buchanga hivi: "Ee Mpadri Zosimas, fanya maziko hapa maiti ya Maria mupotevu. Nilikufa ile siku kilipewa Mwili na Damu ya Kristu. Omba kwa wokovu yangu". Hii matendo yote yalifanyika ku mwaka 378.

Huyu Mt. Maria, Mt. Pelagia, Mt. Musa toka inchi Ethiopia, Mt. Augustino na weingin na mifano mazuri ya nguvu ya toba. Kwa hivi na sisi haipaswe kupotesha kitumaini yetu mbele ya wema ya Mungu. Tunaweza kufanyika na sisi, kwa saidio ya Mungu, sawa malaika na roho kieupe, kama tutatubu ya kweli, sawa vile huyu Maria wa Misri.

### Sabbato ya mtakatifu Lazaro

Ufufuo ya Lazazo ni muujiza kubwa kabisa, ile aliifanya Kristu mbele ya Ufufuo wake. Alijua Kristu hali ya afya ya Lazazo na alichelewa kufika na haraka mujini Bithania. Kwa hivi wa dada ya Lazaro walimupeleka kaburini ya ndugu yao. Kristu alisema ya kutosha jiwe ku kaburi na mara moja alimuita Lazaro, hivi: Ee Lazaro kuja inje". Na ule mufu aliyekuwa ndani ma siku ine na alioza, alikuja inje muzima.

Lazaro juu hapana kumuua watu wa Ebrania, alikimbia mu Kisanga Kypro, pahali aliishi sawa askofu miaka makumi tatu (30). Alikufa mara ya mbili ku mwaka 63, kisha kuzaliwa kwa Kristu na walimuzika karibu ya kanisa kwa jina lake mujini Larnaka.
Hii siku ya Sabbato ni siku ya furaha ha ya ufufuo, kwani alifufuka Lazazo. Hii siku ndani ya Ibada tunaimba Mahimidi ya ufufuo ya Kristu, hii sala ya ufufuo ya Kristu: "Tukiona ufufuo wa Kristu, tumsujudu Yesu Bwana Mtakatifu...", mbele ya Zaburi 50 (51) na ku mwisho ya Kuaga mpadri anasema: Aliyefufuka katika wafu..... Tangu leo mpaka siku ya Mungu ya Mt. Thomas hatusome sala ya makubusho ya wafu.

## Siku ya  Mungu ya Sita ya Kwarezima

Kisha ufufuo ya Lazaro Yesu Kristu alikimbia mutoni Yordani, kwani walitaka wakubwa makuhani ya dini ya kiebrania ya kumukamata na kwa kumuua.
Ma siku sita mbele ya Pasaka ya dini ya kiebrania, alirudia mujini Vithania, pahali ndani ya jamaa ya Lazaro, dada yake Maria alimupakaa miguu yake na marasi na siku ingine ya Mungu (Siku ya Mungu ya Matawi) aliingia ndani ya Yerusalema kwa kuikaa pa punda moja kidogo.

Ile saa watu walifungula na waliweka chini pa njia manguo yao na walichunga pa miko no yao matawi juu ya kumupokelea Kristu sawa mufalme ya inchi yao. Walimuwaza ya kama Huyu atakuwa mufalme ya inchi yao na Huyu atawaokoa toka utumwa ya utawala ya Roma. na walimupokelea na hii wimbo: "Osana, anayekuja kwa jina la Bwana, Mufalme ya Israeli". Maana ya neno Osana ni "Uniokoe, ninakuomba. Hii nyama juu yake aliika Kristu inatuonyesha ya kama mataifa ya zamani waliishi ndnai ya zambi na dini ya sanamu, lakini sasa walimupokelea Yesu Kristu sawa Mwokozi na Mukombozi yao toka dini ya sanamu.

Yerusalemna nzima ilifurahi kwa hii mapokeo ya Kristu na mpaka leo Yerusalema mupya, nikusema Kanisa Orthodokse ya Kristu anashangilia hii siku, kwa sababu anamupokelea mushindi ya lufu na furaha kwa ajili ya ufufuo yetu toka zambi na utumwa ya shetani.

## Juma Kubwa na Takatifu

Inaitwa Kubwa, hapana kwa sababu iko na ma siku ao saa kupita mengi, lakini ni makubwa matendo na mashangilio yenye sisi tunashangilia. Ndani ya hii Juma tunachukua mafaa ya kiroho makubwa, kwa sababu ilisimama nvita toka shetani ku Mungu. Iliharabika uwezo ya lufu na mamlaka ya shetani, ilikimbia mafigo na ilikuja urafiki na sikilizano katikati ya Mungu na watu wote. Maana haya yote tunapata ndani ya wimbo yote sisi tunaimba hii Juma.

Ibada yote ya hii Juma tunaimba kila siku asubuyi na magaribi, lakini, kwa sababu watu wanatumika kila asubuyi ibada ya asubuyi tunaifanya kila magaribi ya siku moija mbele. Nikusema magaribi ya siku ya kwanza tunaimba ibada ya asubuyi siku ya mbili.

**Siku ya kwanza ya hii Juma. (Siku ya Mungu ya Matawi, magaribi)**

Hii siku tunakumbuka matendo mbili. Ku mwanzo tunakumbuka Yosefu, mtoto ya Yakobo, aliyekuwa alama na mufano ya Yesu Kristu. Huyu Yosefu, walimuchukiza wa ndugu wake, walimuuzisha kwa mufalme ya Misri na kisha huyu, ile wakati ilikuwa njaa pa fasi yote ya dunia, walikuja baba yake Yakobo pamoja na wandugu wake na waliishi pamoja naye. Vile na Yesu Kristu wa ndugu wake, watu ya kabila kiebrania, walimukamata, walimuuzisha kwa makuta 30 na walimuua, lakini kisha Yesu kwa kifo yake aliwapatia kwa watu hapana ngano sawa Yosefu, lakini mwili na Damu yake kwa kupata uzima ya milele.

Kavumu ingine kubwa hii siku tunashangilia ni ukumbusho ya muti muzeituni. Huyu muti Yesu Kristu alimufiga na mara moja alikauka. Alitaka kuonyesha Yesu ya kama na Synagoga ya dini ya ebrania ilisimama kuleta matunda, nikusema hakuna namna watu ya kupata wokovu ndani ya hii dini ya kiebrania.

Ndani ya hii Ibada ya asubui, kisha somo ya Eksapsalme sita, tunaimba hii mwimbo: "Tazama Bwana Arusi anakuja kati ya usiku..."mara tatu. Vile tunaimba na kila asubui ya ma siku ya mbili na ya tatu ya hii Juma. Kwa hivi hii Ibada inaitwa Ibada ya Bwana Arusi.

**Siku ya mbili ya hii Juma. (Siku ya kwanza magaribi)**

Hii siku tunakumbuka ku mwanzo Mufano (Parabola) ya ma Bikira kumi, kwani na sisi tunaitwa ya kumupokelea Kristu na mishumaa ya mafazila, kabisa fazila ya wema. Ya mbili tunakumbuka Parabola ya Talanta, nikusema na sisi tunapaswa kuongeza ma zawadi ya Roho Mtakatifu ndnai ya uzima yetu.

Kanisa yetu inatukumbusha hivi, kwani atakuja mara ya Mbili katikati yetu mara moja bila tangazo yake. Ataomba sisi ya kumuonyesha endeleo yetu ya kiroho hata kama ni kidogo. Ndani ya hii Parabola ya Talanta, alimuhukumu ule mutumwa ya tatu, kwa sababu alifuchama talanto moja ile mukubwa mwake alimupatia ndani ya ulongo.

Tena sisi haipaswe kusahau kundi ya ma bikira tano wasiyo akili, wenye walipotesha Paradizo japo walikuwa watu ya dini...Mufano yao inatuonyesha ya kama haienee paka imani yetu ao utimizo ya mapaswa yetu bila kuwa uzima yetu katika imani nguvu na matendo ya imani ya Kristu. Haipaswe sisi kusadiki na udanganyifu ya kama tutaokolewa kwa sababu tuko waorthodoksi, bila matendo mazuri.

**Siku ya Tatu ya hii Juma (Siku ya Mbili, magaribi)**

Hii siku tunakumbuka ukumbusho ya matendo tatu:

1.Kwa kupakaa na marasi mwanamuke moja kahaba nyuso ya Bwana Yesu Kristu.

2. Makusanyo ya wakubwa ya dini Ebrania juu ya kukamata mpango ya kumuua Kristu.

3. Ondoko ya Yudasi toka kundi ya Wanafunzi ya Kristu na kimbilio yake kwa makusanyo ya wakubwa ya Ebrania na masikilizano yao juu ya kumutoa Kristu. Juu ya hii kazi mbaya ya Yudasi, Kanisa yetu iliweka kifungo ya siku ya Tatu, juu ya kukumbuka sisi hii tendo mbaya ya Yudasi.

Ku mwisho ya hii Ibada tunaimba mwimbo ya mwandishi mwanamuke jina lake Kasiani. Huyu mwanamuke aliandika wimbo ya Kanisa na eko Mtakatifu ya Kanisa yetu.

Magaribi ya hii siku ya Tatu tunafanya ndani ya Kanisa, mbele ya Ibada ya Bwana Arusi, Fumbo ya Mafuta Takatifu. Iko namna kupakaliwa paka waaminifu wa orthodoksi na hapana wakatikumeni, kwa sababu bado kubatizwa.

**Siku ya Ine, ya hii Juma (Siku ya tatu, magaribi)**

Hii Siku ya Ine tunakumbuka:

1. Bwana Yesu Kristu alinawisha miguu ya wanafunzi wake.
2. Karamu Kubwa ya Kristu pamoja na Wanafunzi wake.
3. Sala ya ajabu ya Kristu mbele ya Mungu Baba yake,

4. Utoaji ya Bwana Yesu Kristu ku mwanafunzi wake Yudasi.

Hii magaribi inafanyika Karamu ya Siri na ile saa alikimbia Yudasi juu ya kumutoa Kristu. Kisha Kristu alinawisha miguu ya wanafunzi wake. Kisha pamoja walienda mu shamba ya michi Kedro, pahali, kisha sala ya Kristu, alikuja Yudasi pamoja na kundi yake na alimubusu Kristu sawa alama ya kumutoa. Kisha waaskari walimupeleka Kristu kwa wakuhani Anna na Kayafa. Wanafunzi wanakimbia, ila tu Yoane na Petro, lakini huyu Petro alimukaa Kristu mara tatu. Ndani ya makusanyo ya Wakuhani walimuhukumu Kristu na kisha walimuchekelea.

Hii Siku ya Ine asubuyi inafanyika Liturgia Kimungu kwa ukumbusho ya Karamu Kubwa, pahali Yesu Kristu aliwapatia kwa Wanafunzi na watu wote ya dunia Fumbo Takatifu ya Mwili na Damu Yake.

**Siku ya Tano ya JUma Takatifu (Siku ya Ine ya magaribi)**

Hii siku tunakumbuka Mateso ya Bwana Yesu, nikusema wakati walimupika na mate, walimupika na kofi, walimuchekelea na ingine mateso. Kabisa tunakumbuka Usulubisho na kifo matata yake. Tena tunakumbuka ukikisho ya ule Munyanganyi aliyekuwa na yeye pa musalaba yake na alimuomba Yesu juu ya kumukumbusha na huyu kwa Ufalme Wake.

Hii ni siku ya unyenyekevu kubwa na sadaka ya Kristu, kwani Kristu wanamuhukumu ya kumufunga na minyororo usiku muzima ya siku ya Ine, mpaka asubuyi ya siku ya Tano. Kisha ile siku ya Tanu, kati ya muchana walimupeleka pa kilima ya Kalvario na katikati ya wanyanganyi wa wili walimusulubisha. Kwa saa ya tatu, kisha kati ya muchana alipaza sauti kusema: "Imekuisha", nikusema anakufa Mwana Kondoo wa Mungu, aliyechukua zambi ya dunia nzima. Kisha walimushusha ku Musalaba na walimuzika mbele ya kuchuka Jua na walimuweka ndani ya kaburi mupya.

Leo tunasoma somo ya Evangelio kumi na mbili ku Waevangelizaji wa ine. Kisha kusoma Evangelio ya tano, tunatosha Mwili ya Yesu Kristu inje ya Altari Takatifu na tunamujugulusha mara tatu kati ya Kanisa na waimbaji wanaimba wimbo moja ya Usulubisho yake. Kisha waaminifu wanaenda ya kuibusu Mwili Yake.

Asubuyi ya siku ya Tanu, ni siku Kubwa tunasoma Ibada ya Saa Makubwa, nikusema Saa ya Kwanza, ya Tatu, ya Sita na ya Tisa.. Kisha somo ya Saa Makubwa, tunaendelea na Ibada ya magaribi, pahali ku mwisho tunasoma Evangelio na ku mwisho yake mpadri anamushusha Mwili ya Kristu ku Musalaba yake na anaipeleka ndani ya sanda moja meupe ndani ya Altari Takatifu. Kisha pa hii fasi, kati ya kanisa tunaweka Meza na kaburi ya Kristu (Epitafios). Pa meza padiri ataweka Nguo Takatifu Epitafios, ile saa Waimbaji wanaimba wimbo ya Apostikha.

Matendo haya haiko paka ukumbusho moja, lakini ni sawa ya kufanyika mbele ya ma macho yetu.. Ni moja Fumbo ya ajabu ile inakuja mbele yetu juu ya kusikia sisi upendo kubwa ya Yesu Kristu juu ya wokovu wetu.

Leo wapadri hawafanye Liturgia Kimungu, kwa sababu Liturgia ilifanyika kwa Kuhani Mkubwa Yesu Kristu pa Musalaba yake. Na Kanisa yetu leo inakumbuka na inaleta mbele ya ma macho yetu hii Liturgia ya Kristu. Hii ni Liturgia ya Sadaka yake kwa wokovu ya watu wote ya dunia.

**Siku ya Sabbato (Siku ya tanbo, magaribi)**

Hii siku ya Sabbato tunakumbuka Maziko ya Mwili ya Kristu na kushuka Nafsi yake ndani ya Hadeze. Kule Kristu, pahali aliingia na Nafsi yake, alishinda Hadeze na aliopoa ma nafsi wale walikuwa kule tangu ile wakati walikuja watu duniani.

Leo, siku ya Sabbato Yesu Kristu anapumuzika, sawa vile na Mungu Baba yake alipumuzika kisha kazi ya kuumba ulimwengu nzima ndani ya ma siku sita. Hii Sabbato ya pumuziko ya Mungu Baba ni alama ya Sabbato ya pumuziko ya Yesu Kristu, ndani ya Kaburi yake. Kisha ma siku tatu iliunganishwa Mwili pamoja na Nafsi Yake na alifufuka Yesu Kristu toka wafu.. Kwa hivi Nafsi ya Bwana Yesu alishinda Hadeze na Mwili alishinda mauti, kwa sababu Mwili na Nafsi yake yalikuwa pamoja.

Magaribi ya hii siku tunaimba Vipande Tatu ya wimbo ya Kaburi ya Kristu. Inaanza Kipande ya Kwanza: Uzima Kaburini...". Kisha Masifu na Doksologia kubwa tunajuguluka pamoja na Kaburi ya Kristu inje pempeni ya Kanisa.

Sabbato asubuyi inafanyika sala ya Magaribi ya Pasaka pamoja na Liturgia Kimungu ya Mt. askofu Basilio. Hii Ibada ikona mufano ya furaha na waaminifu wanaita hii Ibada "Ufufuo ya kwanza". Hii ni Ibada nzuri kabisa, kwa ajili ya Shangilio ya Paska, ile tutashangilia kabisa usiku na kesho. Tazama mwimbo moja ya ajabu: "Leo Hadeze inalia tena inapaza sauti: Ufalme wangu umevunjwa, Mchungaji
mwenye kusulubiwa amefufua Adamu; naondolewa wafungwa wangu,na wale
nilimeza kwa nguvu yangu nimewatapika.Msulubiwa ameacha makaburi
wazi,utawala na mauti unabomoka.Ee Bwana,utukufu kwa Msalaba na kwa Ufufuo
wako". Na tazama na mwimbo ya ushindi: "Fufuka,ee Mungu, hukumu dunia,kwani utariti mataifa yote".

Hapa inaisha Wakati ya Kwarezima. Kutoka Siku ya Pasaka inaanza wakati ingine ile inaitwa Pentikostari.

# MA IBADA YA PENTIKOSTARI

Pentikostari inaitwa Kitabu moja ya Kanisa Orthodokse, ile inaanza kisha Ufufuo ya Bwana Yesu Kristu na inajitimia pamoja na Mineo (Kitabu ya Watakatifu ya kila mwezi). Hii Kitabu ikona wimbo ya Ibada ya Magaribi na ya Asubuyi. Tena Pentikostari inaitawa na hii wakati toka siku ya Pasaka ya Kristu mpaka siku ya Mungu ya Pentikosti, nikusema masiku makumi tano kutoka siku ya Ufufuo ya Kristu. Kisha siku ya Mungu ya Pentikosti tunafata Juma ya Roho Mtakatifu mpaka siku ya Mungu ya Watakatifu wote.

Pasaka na Pentikosti ya taifa ya Kiebrania ilikuwa mufano ya Pasaka ya Wakristu na alama ya Pentikosti ya Kanisa ya Kristu.

Pasaka ya dini ya kiebrania (Pasaka maana yake mapito) ilikuwa ukumbusho ya kutoka taifa ya kiebrania toka Misri na mateso pale yao na kwa kurudia mu inchi ya Palestini.

Pasaka ya wakristiani ni siku ya kutoka ku inchi ya lufu na ya mateso ya shetani na ukombozi ya mateso ya uzima ya zambi.

Pentikosti ya dini ya Kiebrania ni ukumbusho ya kukamata Nabi Musa Mawe pahali yaliandikwa sheria toka Mungu pa Mulima Sinaya. Hii tendo ilifanyika ma siku makumi tano (50) kisha ya kuondoka taifa ya Kiebrania toka Misri..

Pentikosti ya Kanisa ya Kristu ni ile siku ya Kushuka Roho Mtakatifu na kuangaza akili ya Wanafunzi wa Kristu, ma siku makumi tano (50) kisha Ufufuo ya Kristu.

Siku Kuu ya kupande Yesu Kristu mbinguni ilifanyika ma siku makumi ine (40) kisha Ufufuo wake. Ile wakati ya ma asiku (40) hatusalimiane sisi: Yabo ao asubuyi vema, usiku vema, lakini tunasalimiana paka: Kristu alifufuka, Kweli alifufuka.

Hii wakati ya Pentikosti, katika Kanuni 20 ya Makusanyo Ikumeniki ya kwanza na Kanuni 90 ya Makusanyo ya Sita na Kanuni 15 ya Mtak. Petro, askofu ya Aleksandria na Kanuni 91 ya Mt. Basilio hatusali ya kupika magoti, kwa sababu tunaishi ndnai ya wakati ya ufufuo ya Kristu. kama tunasali ya kupika magoti hii inaonyesha ya kama tuko tena ndani ya hali ya kutubu. Tunasali ya kusimama ya kuonyesha ya kama tuko watu na sisi ya ufufuo ya nafsi yetu. Uzima ya zambi iliisha na sasa na sisi tunafurahi ufufuo yetu, kwa sababu alifufuka kwa ajili yetu Bwana wetu Yesu Kristu.

**Juu ya nini Malaika alitelemusha jiwe ku Kaburi ya Kristu?**

Malaika alitelemusha jiwe ku Kaburi ya Kristu juu ya kusaidia Wanawake Wabebaji manukato (Mirofori) na Wanafunzi ya Kristu juu ya kuingia, wakati walikuja karibu, ndani ya Kaburi na ya kusadiki ya kama alifufuka Kristu. Yesu Kristu alifufuka, bila kutelemuka jiwe ku Kaburi yake. Kama Malaika alikataa kutelemusha jiwe, waaskari wataendelesha kuchunga Kaburi ya Kristu, bila kujua ya kama Huyu alifufuka. Tena na Wanafunji wake hakuna namna ya kusadiki ya kama Mwalimu wao alifufuka, kama jiwe ilikuwa pa kaburi yake.

Ufufuo ya Kristu ilifanyika asubuyi mapema ya siku ya Mungu, lakini hatujue namna gani alifufuka. Hii ni Siri kubwa, sawa Siri kubwa ni namna gani Maria Bikira alipata mimba. Mu kanisa

Orthodokse tunafatula Picha ya ufufuo ya Kristu ile saa Yeye alishuka ndani ya Hadeze ya kuopoa wakubwa wa kabila ya Ebrania na kabisa Adamu na Eva. Wakristiani ya "Kanisa" ya Roma wanafatula Kristu ya kutoka inje ya Kaburi yake ya kukamata na pendera moja, lakini hii picha haiko ya kweli, kwa sababu hakuna mutu moja aliyeona Ufufuo ya Kristu ilifanyika namna gani.

## Siku ya Pasaka Takatifu

Siku ya Sabbato (Posho) ni siku ya mwisho ya wakati ya Triodi. Siku ya Pasaka Takatifu ni "siku kusanyiko Takatifu siku ya kwanza ya juma siku ya ufalme na utawala, Karamu ya makaramu na siku Kuu ya siku Kuu na katika hii siku tunabarikia Kristu kwa milele". Hii siku ni mwanzo ya wakati ya Pentikostari. Matayarisho ya Siku Kuu ni ma Ibada yote ya Triodi, Ya Juma Takatifu na kabisa Ibada ya Sabbato Kubwa.

Ibada ya Pasaka, sala ya asubuyi na Liturgia yanafanyika usiku ya siku ya Sabbato ku siku ya Mungu. Kanuni ya Ufufuo ya sala ya asubuyi iliandikwa ku Mt. Yoane Damaskinos. Hii Kanuni ya Ufufuo ni muzuri sana, kupita ya ma Kanuni ingine ya mwaka muzima. Kisha mpadri anasoma Fundisho ya Mt. Yoane Krisostomo.

Tangu leo hatusema ku mwanzo ya kila Ibada: Mungu Mutakatifu...lakini tunaanza kusema mara tatu: Kristu alifufuka katika wafu...". Tena pa fasi ya hii sala ya mwisho: kwa maombezi ya Watakatifu Wapadri...". tunasema: "Kristu alifufuka katika wafu...". . Vile tunasema mpaka siku moja mbele ya Kupanda Yesu Kristu mbinguni. Tena hatuseme hii sala: Mfalme wa mbinguni, Wewe Mfariji. Roho ya ukweli, uliye pahali popote, na kuvijaza vitu vyote, Wewe hazina ya mambo mema, tena Mpaji wa uhai. Njoo kukaa kwetu na kutusafisha kila doa, hata kuziokoa roho zetu, Mwema We. ..." mpaka ile siku ya Pentikosti. Tena hatuseme: " Njooni tumwinamie na tumsujudu Mungu Mfalme wetu. Njooni tumwinamie na tumsujudu Kristu yeye Mungu Mfalme wetu. Njooni tumwinamie na tumsujudu yeye Kristu, aliye Mfalme na Mungu wetu"mpaka Sindikizo ya Ibada ya Pasaka. Tena mu Juma Mupya, Juma ya kwanza kisha Pasaka, hatusoma Apodipno Kidogo ao sala ya Kati ya usiku, ao Saa ya tisa. Pa fasi yao tunasoma Ibada ya Pasaka. (tafuta ndani ya Saa Kubwa, paje ).

### Sala ya Magaribi ya siku ya Pasaka

Magaribi ya hii siku ya Pasaka Waaminifu wanakuja kanisani, pahali watasoma Sala ya Magaribi. Kisha wimbo ya Apostika watasoma wapadri, tena na waaminifu, kama wanajua, Evangelio ya ma lunga ya mbalimbali. Hii ni desturi ya zamani na tunataka kuonyesha ya kama kuhubiri ya Kristu inasabaha pa fasi yote ya dunia.

### Juma Mupya

Hii Juma inaanza kutoka siku ya Pasaka mpaka mu Posho magaribi mbele ya Siku ya Bwana ya Mt. Thomas inaitwa Mupya na iko sawa siku moja. Inaitwa Mupya, kwa sababu Wakatikumeni walibatizwa Muposho Mkubwa na walikuwa waaminifu wapya. Kila siku ya hii Juma tunasoma paka Ibada ya ufufuo ya siku ya Pasaka. Tena waaminifu, wenye walichunga mafungo ya chakula hii wakati ya Kwarezima muzima, wanaweza kupewa kila siku Mwili na Damu ya Kristu, bila kifungo. Nikusema tunaweza kula na mayayi na maziwa na nyama, lakini magaribi chakula hapana ya nguvu na siku ingine asubuyi tunaweza kukomunyika.

### Siku ya Tano ya Juma ya Mupya

Hii siku tunashangilia Ukumbusho ya Ubatizo ya Kanisa kubwa ya Mzazi-Mungu, ile ni mujini Konstantinopoli tangu karne ya tano.

Kisha ya kuanguka muji hii kubwa pa mikono ya Waturki ku mwaka 1453, huu kanisa ilianguka na wamuslamani walikamata mawe na walijenga mosque yao. Ilibaki paka kule karibu kanisa moja kidogo na huu ilibomowa mu karne 19. Ku mwaka 1833 Wakristiani ya Konstantinopoli walijenga Kanisa mkubwa kwa utukufu ya Mzazi Mungu. Hii siku tunashangilia Hii chemchem ya miujiza, ile ni chini ya hii Kanisa ya Mzazi-Mungu.

**Siku ya Mungu ya Mtume Thomas.**

Siku ya Mungu ya mbili inaitwaa ya Mtume Thomas, kwa sababu hii siku tunashangilia onekano ya Bwana Yesu Kristu katikati ya Mitume, pahali alikuwa na Mtume Thomas. Kristu aliingia ya kufunga milango na ma dirisha yote. Aliwasalimia kusema mbele yao: "Amani kwa wote". Kisha alimuita Thomas, alimuonyesha mikono na mbavu yake juu ya kusadiki. Thomas alisadiki na alisema: "Bwana wangu na Mungu wangu".

**Siku ya Tatu ya Wanawake Wabebaji manukato (Mirofori).**

Hii siku tunakumbuka hawa wanawake wabebaji manukato, wenye pamoja na Wanafunzi wa siri Yosefu na Nikodimo walienda kwa mkubwa Pilato na waliomba Mwili ya Yesu Kristu. Tena hawa wanawake, asubuyi mapema siku ya Mungu, walienda Kaburini, japo ilikuwa kundi ya wa askari na walichunga Kaburi yake, kw akupakaa Mwili ya Mwlaimu mwao. Bila kuogopa na bila kuwaza namna gani watatelemusha jiwe ku Kaburi ya Kristu. Ile saa alisimama kati yao Bwana Yesu aliyefufuka na kisha hawa wanawake walienda kutangaza kwa Wanafunzi Wake ya kama Kristu alifufuka na watakutana kwa mukini Galilaya. Mifano yao yanatuonyesha ya kama walimupendsa mwalimu yao na bila kuogopa walienda usiku Kaburini ya Kristu.

**Siku ya Ine ya mwenye kupoza.**

Hii Siku ya Mungu Kanisa yetu inashangilia muujiza ya kuponyeshwa ule mwenye kupooza kwa uwezo ya Yesu Kristu. Hii muujiza ilifanyika pa kisima moja, ile iliitwa Kisima ya Kondoo, kwa sababu kule walisafisha watu matumbo ya ma kondoo wenye walichinja juu ya kutoa sandaka Hekaluni ya Solomono. Paka mara moja kila mwaka Malaika wa Mungu alikujaka na alitenga maji ya kisima na ule mutu aliyeweza kuingia ku mwanzo ndani ya maji aliponyeshwa. Huyu mwenye kupooza, aliyekuwa kule miaka 38, alivumilia bila kupata mutu moja ya kumusaidia. Huyu mugonjwa alimuchagua Kristu kati ya wagonjwa weingine na alimuuliza: "Unataka kuwa mwenye afya? Na ule alimujibu: "Ee Bwana, misina na mtu niweke ndani ya kisima, ile saa maji inajitenga. Alimuchagua huyu mtu Kristu, kwa sababu alivumilia kule miaka mengi, bila kupotesha kitumaini yake, bila kuwa na tamaa ao chuki kwa wagonjwa weingine, wenye kila mwaka moja moja waliponyeshwa. Kristu alimutunza na alimwambia hapana kufanya zambi ingine, juu hapana kupata mateso kupita mengi.

**Siku ya Tatu, kati ya Pentikosti**

Kisha hii muujiza aliifanya Kristu kwa huyu mwenye kupooza, wakubwa ya ebrania walitaka kumubaba Kristu, kwa sababu alitumika hii siku ya Sabbato. Kila Sabbato ni siku bila kazi mu dini ya Kiebrania. Kristu aliondoka na alikuja mu njimbo ya Galilaya. Alirudia mu Yerusalema ile siku ya shangilio kati ya Pentikosti. Hii Siku Kuu ni ukumbusho ya Fundisho Takatifu Yake naya Kizazi ya asili kimungu yake. Ndani ya hii Ibada tunapata ukumbusho ya miujiza Yake, kwa sababu haya yanatuonyesha asili kimungu chake.

**Siku ya Tano ya mwanamuke mwenye Samaria**

Kisima ya Yakobo, pahali Yesu Kristu aliikaa kati ya muchana siku moja juu ya kupumuzika kwa ajili ya muchoko yake pa njia, ilikuwa karibu ya muji Sikemu, ile ni karibu ya kilima Garizini. Ku mwaka 1887, mbele ya kuzaliwa kwa Kristu patriarchi ya Israeli Yakobo, wakati alirudia ku inchi Iraki (Mesopotamia), alinunua shamba moja kule na alifungula kisima. Hii kisima mpaka wakati ya Yesu Kristu iliitwa Kisima ya Yakobo.

Karibu ya hii Kisima alimuongojea Yesu Kristu huyu mwanamuke toka muji Samaria na alimuomba amupatie maji. Na hii namna alitaka kumukokota karibu yake, kwani shetani aliisha kumukokota mu uzima ya zambi. Wakati alisikia maneno yake ya ajabu juu ya uzima yake ya zamani, alishituka na alisadiki Kwake. Kisha alibatizwa na aliitwa Fotini. Alihubiri dini ya Kristu mu inchi Italia na alikufa kwa mateso mengi mujini Roma ile wakati alikuwa mufalme ya Roma Neroni, pamoja na wa dada ine yake na watoto wa wili yake. Haya ni matunda ya ajabu ya imani ya Kristu!

Makumbusho ya mt. Shahidi mkubwa Fotini pamoja na wadada na watoto yake Kanisa yetu inawashangilia mu tarehe 26 ya mwezi ya Februarie. Lakini tunawashangila na leo juu ya kukumbuka ya kama na sisi anatuongojea Kristu pa kisima moja juu ya kutukuta na kutupatia fundisho yake ya wokovu...

**Siku ya Sita ya Kipofu**

Siku ya Sabbato moja alitoka Kristu ku Hekalu ya Solomono na pa njia alimukuta huyu kipofu aliyekuwa kipofu toka tumbo ya mama yake. Alipakaa ma macho yake na potopoto ya bulongo na alimutuma ya kunawa kisimani ya Siloamu. Hapana kwa sababu hii maji ya kisima iliweza ya kumutunza, lakini aliotaka Kristu kupima imani yake. Basi, ule kipofu alisadiki kwa maneno ya Kristu na aliende kule. Alinawa na alirudia hapana kipofu, lakini na nuru pa macho yake. Kisha tunaangalia namna gani huyu mtu alijibu mbele ya wakubwa ya Wayuda namna gani Kristu alimutunza. Alipata hatari ya kumufukuza, lakini huyu alichagua ya kumufukuza na hapana ya kunyamasha hii muujiza ya Kristu.

Hii Evangelio ya leo inatupatia mufano nzuri ya huyu aliyekuwa kipofu, kwa sababu hasiogope kusema mbele ya wakubwa ya dini ya Ebrania ya kama Yesu Kristu alimutunza, japo ilikuwa mambo ya kumufukuza. Tena tunaangalia udanganyifu ya wakubwa ya Yudea, wenye, japo walijua ya kama nuru inatokea toka Kristu, lakini walikataa kumufuata.

**Siku ya Tatu ya Juma ya saba**
**(Sindikizo ya Pasaka)**

Hii Ibada ni pamoja na Ibada ile tulifanya kwa Siku Kuu ya Pasaka. Hii siku tunasikia na tunasalimia wa ndugu wetu na Kristu alifufuka mara ya mwisho.

Hii siku wapadri wengine wanafanya hii Ibada usiku nzima juu ya kuishi mara ya mbili hii furaha waliishi na ile siku ya Ufufuo ya Kristu, mbele ya ma siku makumi ine (40).

**Siku ya Ine ya Juma ya Saba**
**Siku Kuu ya Kupanda Kristu mbinguni**

Wakati ya ma siku makumi ine (40) Yesu Kristu alikuja na alionekana katikati ya Wanafunzi wake na alizungumuza, alikula na alikunywa na hawa. Hii siku ya makumi ine alikuja na aliwapatia hamuri Yake ya mwisho. Nikusema aliwaambia juu ya kuhubiri na kufundisha ma inchi yote ya dunia, kisha ya kuchukua Roho Mtakatifu ndani ya muji Yerusalema. Kisha aliwatosha wote pamoja mulimani ya mzeituni.

Kule mbele ya ma macho yao na ya Mzazi Mwake Bikira Maria, aliwabariki na alipanda mbinguni pamoja na mwili yake. Aliikaa pa wingo moja. Mara moja walikuja wa malaika wa wili na mavazi meupe na waliwaambia: "Ee wanaume wa Galilaya, juu ya nini mulisimama na munaangalia mbinguni? Huyu Yesu anayepanda sasa mbinguni, vile vile atarudia...(Matendo ya Mitume 1,11). Na wanafunzi kisha walirudia mujini Yerusalema na furaha kubwa. Wapadri weingine wanasema ya kama hii Siku Kuu ni kupita kubwa mbele ya ma Siku Kuu ingine, kwa sababu Kristu alimaliza kusudi ya uji yake hapa duniani, nikusema Yesu Kristu alipandisha asili kimutu juu mbinguni, kwani Yeye alipanda pamoja na mwili Yake.

Na sisi tunafurahi, kwa sababu, japo Kristu alipanda mbinguni, lakini atabakia karibu yetu kwa milele mpaka mwisho ya dunia, pamoja na Roho Mtakatifu, anayetupatia ma zawadi ya mbalimbali.

**Siku ya Mungu ya Saba ya Wapadri Watakatifu**

Hii Siku ya Mungu ya saba Kanisa yetu inashangilia 318 Wapadri wabebaji-Mungu, wenye walisanyika Makutano kubwa ya Kwanza ya Ulimwengu ku mwaka 325 mujini Nikea, ile alikamata mpango ya kuisanyika Mtakatifu Konstantino, mufalme mukristu wa kwanza ya utawala ya Konstantinopoli. Sababu ya hii makusanyo ilikuwa fundisho ya uwongo ya mpadri Arios toka Kanisa ya Aleksandria, aliyehubiri mbaya ya kama Mwana wa Mungu Yesu Kristu sieko Mungu, lakini ni kiumbe, bila kuwa pamoja na Mungu Baba yake mbele ye wakati wote. Japo makusanyo alimuhukumu na alimutosha ya kanisa ya Kristu, lakini huyu Arios aliendelesha

kusambaa hii fundisho ya uwongo. Kwa hivi Hawa Wapadri 318 walisanyikwa na walifundisha ya kama Yesu Kristu ni Mungu, Mwana wa Mungu toka Munga Baba wa kweli. Tena waliandika mafundisho saba ya Symvolo ya Imani. (Mafundisho ingine tano waliandika Wapadri ya Makusanyo Kubwa ya Mbili ku mwaka 381, kisha kuzaliwa kwa Kristu.

**Sabbato mbele ya Siku Kuu ya Pentikosti**

(Sabbato ya kukumbuka ma nafsi ya Wafu wote).

Hii Posho ni ya mbili ya mwaka muzima. Sabbato ya kwanza ya kukumbuka Wafu ni mbele ya siku ya Mungu ya Apokreo. Leo tunakumbuka ma nafsi ya Wafu, kwa sababu kesho tutaomba nuru ya Roho Mtakatifu. Huyu Roho Mtakatifu, tunaomba juu ya kupumuzisha na ma nafsi yao.

Haipaswe kusali juu ya wafu paka ma siku haya ya mbili. Saidio ya kiroho kwao paka sisi wenye muzima tunaweza kuwatumia. Kwa sala na saidio ya wamaskini tunasali Mungu apumuzishe ma nafsi yao, katika sauti ya Agano Jipya: "Maombi yako na sadaka zako zimefika juu kama ukumbusho mbele ya Mungu" (Matendo ya Mitume 10,4 na 10, 31).

**Siku ya Mungu ya Pentikosti**

Hawa waliyokuwa ile saa Yesu Kristu alipanda mbinguni wote walikuwa watu 120 (11 Mitume, 70 Mitume weingine, wanafunji wao, Wanawake Wabebaji manukato, Mzazi-Mungu Maria, wa dada na wa ndugu ya Kristu) walirudia nyumbani moja ya muji Yerusalema an waliongojea kuwatumia Kristu zawadi ya Roho Mutakatifu. Hii Tendo ya ajabu ilitimizwa ma siku 10 kisha ya Kupanda Yesu Kristu mbinguni na ma siku 50 kisha Ufufuo wake.

Roho Mutakatifu, ile siku, na saa asubui ya tisa alishuka sawa pepo nguvu na aliikaa sawa alama ya ndimi ya moto pa vichwa ya Mitume. Hawa wote waliangaziwa na walijaa na ma zawadi ya Roho Mtakatifu. Kwa ajili ya makelele ile ilifanyika kwa kushuka Roho Mtakatifu, hawa mataifa wenye walikuwa ndani ya Yerusalema, walikuja karibu ya ile nyumba ya kuangalia jambo gani ilikuwa. Walikuwa mataifa kumi na saba (Matendo ya Mitume 2. 9,10). Mtume Petro alisimama mbele yao na aliwafundisha jambo gani ya ajabu ilifanyika katikati yao. Hawa watu ya mataifa ya mbalimbali walifurahi na ile siku walisadiki na walibatizwa watu 3000. Hawa walikuwa Wakristiani wa kwanza ya Kanisa ya Kristu.

Mitume wa Kristu mara moja walifanyika wenye akili na hekima. Walianza kufundisha watu ndani ya ulimwengu nzima.

Hii Siku Kuu ya Pentikosti ni siku ya kuzaliwa Kanisa ya Kristu ndani ya dunia nzima. Pentikosti ni uzima ya Kanisa ya Kristu, ni uzima bila kusimama ya kuingia Roho Mtakatifu ndani ya uzima yetu.

Huyu Roho Mtakatifu anaangaza leo hawa watu wenye wanataka kuchunga ma hamuri ya Kristu na wanaongojea akuje na nyumbani ya roho yao Kristu juu ya kuwapatia neema Yake.

Kisha Liturgia ya hii Siku ya Mungu tunafanya Sala ya Magaribi juu ya kusikia somo ya ma sala tatu mazuri sana ile anasoma padri mbele ya Utatu Mutakatifu. Ma sala haya ni sala ya kumutukuza Mungu, kumushukuru na kumuomba atusaidie na alete pumuziko ya wa ndugu wetu, wenye walikufa. Tena tunamuomba abakie katikati yetu kwa milele, neema ya Roho Mtakatifu.

**Siku ya kwanza ya Juma ya mnane**
**(Siku Kuu ya Roho Mtakatifu)**

Hii siku ya kwanza ya hii juma inayekuja, tunashangilia Roho Mtakatifu, Mwenyezi Mungu, Muletaji uzima na Mtakatifu kamili na mwenye kuwa asili umoja pamoja na Baba na Yesu Kristu.

Huyu Roho Mtakatifu, katika malako ya Kristu anabaki ya kuendelea ndani ya kanisa yake na anaongoza watu njiani ya ukweli. Anachunga, analinzi na anaongoza kanisa ya Kristu katikati ya ma karne yote. Kwa hivi Kanisa ya Kristu haitaharabika, lakini itabaki kwa milele mpaka mwisho ya hii dunia.

Hii Juma tunakula ma siku zote, bila kuchunga chakula siku ya tatu na siku ya tano.

**Siku ya Mungu ya mnane**
**Ukumbusho ya Watakatifu wote**

Siku Kuu kubwa ya mwisho ile wakati ya Pentikostari ni Siku ya Mnane kwa jina ya Watakatifu wote. Tunawasifu hawa Watakatifu hii siku ya Mungu juu ya kuonyesha matunda ya kiroho ya Mitume, wenye walichukua neema ya Roho Mtakatifu, juma moja mbele ya siku ya Pentikosti na kwa ajili ya mahubiri yao, walizaliwa na walitakaswa hawa Watakatifu. Juu ya mifupa ya Mashahidi na Watakatifu ilisabitishwa na ilisimama sawa usingi Kanisa ya Kristu na kwa damu yao Kanisa ilimwangwa na iliongezeka.

Kwa sababu Watakatifu ni wingi na hesabu yao inaongezeka ya kuendelea, tunasifu kwa hii Shangilio ukubusho yao yote, nikusema ukumbusho ya Wenye Haki, Wanabii, Mitume, Mashahidi, Wasimamizi ya Imani, Wachungaji ya waaminifu, Walimu, wanaume na wanawake, wenye kufamia na wasiyo kufamia, tangu wakati ya Adamu mpaka ma siku haya yetu. Tena pamoja na wao tunasifu na majeshi ya Malaika na kabisa Mzazi-Mungu, Bikira Maria, Mama ya Bwana wetu Yesu Kristu.

Watakatifu ni hawa watu wenye wanaishi pa inchi yetu mafundisho matakatifu. Kwa hivi uzima ya Watakatifu inatuonyesha ya kama Kanisa ya Kristu haiko paka fundisho ya bure, lakini ni Fundisho na matunda yake. Matunda yao ni uzima takatifu ya Watakatifu. Kwa mafundisho ya uzima yao tunapata namna gani mtu moja ataweza kufanyika mtakatifu kwa saidio ya ma Fumbo, Neema ya Mungu na ma fazila mtakatifu. Kama tunasoma Vitabu na uzima ya Watakatifu tunapata njia ya nuru, utakaso na wokovu. Tena tunaweza kujua namna gani tutafukuza nguvu ya zambi, ya zoezo mbaya, nguvu ya shetani na nguvu ya lufu ku uzima yetu. Tena mifano ya Watakatifu wanatuonyesha namna gani mtu moja anatakaswa, japo zamani alikuwa munyanganyi, muzinifu, mulevi, mwana mupotevu. Tena tunaweza kusema ya kama kila Mutakatifu ni Yesu Kristu kwa milele kwa ajili ya ma fazila na neema kimungu yake.

## MA IBADA YA USIKU NA MUCHANA

Ibada inaitwa kundi moja ya ma sala ya mbalimbali, maombi na wimbo, yenye sisi tunafanya kwa saa fulani ya usiku na muchana kwa utukufu ya Mungu na utakaso ya waaminifu.

Tunda ya kusoma ma Ibada ni hii: Waaminifu wanakutana ya kuendelea na Mungu, wanafurahi kwa hii ushirika na wanamushukuru Mungu kwa ajili ya ma zawadi na baraka yake ao kwa mateso, yenye yanakuja mu uzima yake kwa ajili ya wokovu yake.

Ndani ya kila Ibada inafanyika mwendo moja ya Mungu katika Utatu Mutakatifu ku taifa Yake na mara moja inafanyika na mwendo moja ya taifa ya wakristu ku Utatu Mutakatifu. Hii kazi ya kushuka na kupanda Mungu na waaminifu inafanyika katika uhuru na upendo kwa ajili ya ufufuo ya Musalaba ya Kristu. sawa vile anatwambia na Mtume Paulo: "Furahini siku zote; ombeni pasipo kuacha. Katika maneno yote mushukuru; maana maneno haya ni mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristu Yesu" (barua ya Kwanza ya Thesal.5,16-18).

Mafananisho ya ma Ibada ni Kumuabudu Mungu na kuishi katika uzima ya kiroho. Bila matendo haya juu ya kumuabudu Mungu na kuishi katika sheria ya Mungu, hakuna namna mtu moja ya kutakaswa.

Ma Ibada yenye tunafanya kila siku na usabitisho, bila kubadilisha saa yao ni:

Sala ya Magaribi, Apodipno Kidogo (sala kisha kula magaribi), sala Kati ya usiku, sala ya asubuyi na Saa ya Kwanza, ya tatu, ya Sita na ya Tisa.

Ma ibada, yenye tunaweza kufanya, bila usabitisho yao, ile saa tunataka ni haya: Sala ya kubariki maji takatifu (ao sala Kubwa ya maji ya baraka na sala kidogo ya maji ya baraka), Ibada ya Ubatizo ya Kanisa moja, Ibada ya kiliyo, Sala ya Mzazi-Mungu na ingine. Ubatizo, paka pa pepo, anaweza kufanya, kama ni mambo ya hatari, hata shemasi moja, hata mwaminifu, kama atanyanyua huyu mtoto mara tatu pa pepo na atasema: Anabatizwa mutumishi wa Mungu (Jina lake) kwa Jina ya Baba na ya Mwana na ya Roho Mtakatifu.

Ibada ya kwanza ni Sala ya Magaribi. Nikusema kila magaribi ya siku moja tunasoma hii Sala pamoja na wimbo ya ule Mutakatifu shangilio yake ni kesho. katikati ya kila Ibada ni Mungu ya Utatu Mutakatifu, kabisa ni Mwana wa Mungu na Mwokozi ya dunia....

## Sala ya Magaribi

Tukona sala ya Magaribi mbili:

1. Sala ya Magaribi Kidogo nii ile sala tunafanya kila magaribi, bila mpadri kutoka inje pamoja na chetezo. Kama Mtakatifu moja, sawa mt. Antonio, ao Mt. Georgio weko na Ibada mbili ya Sala ya Magaribi, hii inatuonyesha ya kama Sala Kidogo ya Magaribi tunafanya hile saa ya magaribi na Sala Kubwa ya Magaribi tutafanya kama tunaanza sala ya kukesha (agripnia).

2. Sala Kubwa ya magaribi ni ile sala tunafanya kila mu Posho ao siku moja mbele ya Shangilio ya Watakatifu Wakubwa. Mpadri ao wapadri wingi wanafanya Kutoka inje na chetezo. Waimbaji ao wapadri wanaimba "Mwangaza upole (ilaron), kisha wasomaji wanasoma somo ya Agano la Kale ku Kitabu ya Mineo na shemasi atasema Ektenia kubwa (mustari moja na maombi).

Kama mpadri atasema: "Haimidiwe Mungu wetu daima..." msomaji anasoma: "Njioni...(Mara tatu) na kisha Zaburi 103 (104) "Bariki Bwana, ee nafsi yangu...". kwa hii Zaburi tunamuonyesha Mungu ya kama tunasimama kila kazi ya hii siku juu ya kumukubusha Mungu na kw akumutukuza kwa ajili Yeye alifanya yoyote vitu katika hekima Yake. Kama tunataka kufanya Ibada ya Kukesha (agripnia) msomaji anasimama pa fasi: "Kitu unachowapa wanakiokokota; kwa sababu kisha waimbaji wataanza kuimba Aniksantaria: Mwanzo yao ni mistari ya hii Zaburi 104, hivi: "Unafunguwa mukono wako, wanashibishwa na mema...".

Kisha shemasi atasoma Ektenia kubwa ao (irinika). Ni maombi mengi mbele ya Mungu kwa jina ya waaminifu na yanaanza na hii ombi: Ku amani tumwombe Bwana". Kama tunataka sisi Mungu asikie maombi letu tunapaswa kuwa na amani ndani ya roho yetu. Amani tunaipata kama tunajiungana na namna nzuri pamoja na Kristu. Kwa maombi haya tunaomba ku Mungu atupatie muda nzuri, saidio ya wa ndugu wagonjwa, kwa wenye wanasafiri, ukombozi ku kila taabu na huzuni ya roho yao. Tena tunaomba amani ndani ya ulimwengu muzima, usabitisho ya Kanisa ya Kristu na unganisho ya waaminifu wote kwa imani moja, Takatifu na Apostoliki. Waaminifu katika kinywa ya waimbaji wanajibu: "Bwana hurumia".

Kisha waimbaji wanaimba ma shairi ku zaburi 141, 142, 130 na 117 toka kitabu ya Zaburi. Nikusema wanaanza kuimba hivi: "Bwana, nimekuita, unisikilize, Unisikilize, ee Bwana. Bwana nimekuita, unisikilize; usikie sauti ya kusihi kwangu. Wakati ninapokuita, unisikilize, ee Bwana. Na mwimbaji ya mbili ataanza kuimba hii mustari: "Maombi yangu ya elekezwe, kama uvumba mbele yako. Kunyanyua kwa mikono yangu, kama zabihu ya mangaribi, unisikilize, ee Bwana". Kisha wataendelesha mistari ya zaburi ingine.

Mbele ya kusoma mistari yote ya zaburi haya, tunasimama juu ya kuimba wimbo ya Siku ya kesho. Kama kesho ni siku ya Mungu, tunaimba wimbo kumi, nikusema wimbo sita ya Ufufuo ya Kristu na wimbo inne ya huyu Mtakatifu ya kesho. Kama hakuna siku ya Posho, tunaimba kila siku wimbo sita, nikusema tatu ku Kitabu ya Paraklitiki na tatu ku Kitabu ya Mineon. Kisha waimbaji wanaimba mwimbo inayeitwa Doksastiko, kwani tunaanza na mwimbo moja ya kumutukuza Utatu Mutakatifu. Ni hii: "Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mutakaitfu". Hii mwimbo inatukuza uzima ya ma fazila ya huyu Mtakatifu ya kesho. Kisha wanaimba waimbaji: "sasa na siku zote, hata milele..." kisha wanaimba mwimbo moja kwa sifa na utukufu ya Mzazi-Mungu.

Kisha mpadri moja ao wote, kama ni wingi, wanafanya Kuingia Kati ya kanisa pamoja na chetezo. Wanasimama katikati na mpadri ao shemasi moja anasema: "Hekima, Simameni na hawa ao waimbaji ao wote pamoja wanaimba hii mwimbo: "Mwangaza upole (ilaron)...Hii mwimbo ni ndani ya Kanisa yetu tangu karne ya tatu. Na zamani waaminifu walisanyikwa hii saa ya magaribi juu ya kumushukuru na kumutukuza Mungu.

Kisha waimbaji wanaimba Prokimenon, nikusema shairi ya zaburi. Kila siku inaikaa na Prokimenon yake. Pempeni ya Prokimenon haya ya kila siku, tukona na Prokimenon ya ma Ibada makubwa ya Magaribi kwa sifa ya Bwana Yesu Kristu, sawa: Ni nani Mungu mkubwa, kama Mungu wetu...". Tena Prokimenon makubwa ya mbili tuko na ile wakati ya Kwarezima.

Kisha shemasi atasoma Ombi Kubwa. Ni mustari moja na maombi ya mambo na watu wingi, sawa juu ya askofu wetu, juu ya majeshi ya watawa, juu ya afaya na wokovu ya wenye muzima, juu ya wafu na taifa ya waaminifu wanajibu kusema: "Bwana hurumia (mara tatu).

Kisha wasomaji wanasoma hii sala: "Ee Bwana, utujalie mangaribi hii kutulinda na zambi...". Zamani waliimba waaminifu wote hii sala. Kisha shemasi anasoma kundi ya maombi ingine, yanaitwa "Plirotika". Tunaomba toka Mungu atupatie Mulinzi malaika ya nafsi yetu, vitu vyote vizuri juu ya saidio ya ma nafsi zetu, amani duniani, kitubio na jibu nzuri mbele ya Kiti ya uhukumu ya Kristu. Kisha mpadri anabariki taifa kusema "amani kwa wote",, kisha anasoma sala, ile saa taifa wanainamisha vichwa vyao mbele ya Mungu kuomba huruma na wokovu na ulinzi hii usiku itayekuja. Kisha waimbaji wanaimba wimbo, yenye yanaitwa Apostikha. Kisha mpadri ao mkubwa ya Kanisa atasema hii sala alisema na mt. Symeoni, wakati alimupokelea Yesu Kristu sawa mtoto mudogo ndani ya kanisa ya Solomono. Nikusema "Sasa Bwana, umuache mutumishi wako...".Kisha msomaji atasoma Trisagion, nikusema: Mungu Mutakatifu..."ma waimbaji wataimba wimbo ya Watakatifu, wenye wanaitwa Apolitikia. Kisha mpadri anasali ya kuomba saidio ku Mzazi-Mungu, Majeshi ya Malaika, majeshi ya Watakaitfu wote na maombi kwa jina ya huyu Mutakatifu ya hii siku.

## APODIPNO KIDOGO

### (Sala kisha chakula ya magaribi)

Kila mtu, kisha muchoko ku kazi ya mbali mbali, usiku anasikia matakio ya kupumuzika. Musingisi ni mufano ya lufu. Mbele ya kulala, hasijue kama atalamuka, kwani anajitoa pa mikono ya Mungu. Kwa hivi kila, mtu anasikia ulazimisho ya kusali mbele ya kulala, juu Mungu amulinze na amuchunge kwa kila ndoto ao jaribu ingine ya shetani kati ya usiku. Kanisa inakuja na inatupatia hapana dawa ya kupata amani mwilini, lakini inatupatia Ibada ya Apodipnon. Imani na sala katika sauti ya watu wakubwa ya masomo, ni dawa ya kiroho kuliko mazuri.

Ibada ya Apodipnon (maana yake sala kisha chakula ya magaribi) inafanyika kisha kula magaribi. Ku mwanzo tunamushukuru Mungu kwani alitupatia hii siku iliyepita na amani, bila mambo mengi. Kisha tunasikia ulazimisho ya kuomba hurumia sisi katikati yetu, juu hapana kulala na chuki ao huzuni ya roho mbele ya mtu fulani mwingine. Kisha tunaomba Mungu atupatie musingishi nzuri na kutulinda kwa kila majaribu ya usiku

Ibada ya Apodipnon ni mbili: Moja ni Kidogo, na tunaisoma kila magaribi na Apodipnon Kubwa, ile tunaisoma mu wakati ya Kwarezima, kutoka siku ya Kwanza mpaka siku ya Tano ya kila Juma ya Kwarezima. Hii sala mbele ya kulala inatufurahi katika kiroho, kwani anakuja Mungu katikati yetu sawa baba na Muumba yetu na anatubariki na antulinzi kwa kila majaribu. Kwa mufano hii sala mbele ya Yesu Kristu: "Na utupe, ee Rabi, saa hii tukienda kulala, mapumziko ya mwili, na ya roho tena utulindie na ule usingizi wa giza ya zambi, na ya kila ubaya ungine wa giza, na wa usiku. Zuia mashawishi kuturukia, zimisha mishale ya yule mwovu, yaliyo na moto, yanatupwa kwetu kwa hila. Punguza vitu vibaya vya mwili wetu, ukiangaza kila nia yetu ya nchini na kidunia. Tena kizi yetu, ee Mungu akili ya kukesha, mafikira sawa moyo wangalifu, usingizi wa kisahala, safi na bila mwogofyo wa kishetani. Hata kutuamusha wakati wa kusali tuwe wahodari mu amri zako, na kuyakamata makumbusho ya hukumu yako. Tena utujalie usiku kucha tuwe na sifa yako, ili tulisifu, tulihimidi, tulitukuze jina lako linaloheshimiwa kamili, na kulipaza sana, jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina", ni ombi moja muzuri sana juu ya kutulinda Yesu Kristu kwa musingisi yetu.

## MESONIKTIKO

### (Sala kati ya usiku)

Ni sala moja na inasomwa mbele ya sala ya asubuyi. Zamani waliisoma na wapadri ndani ya ma kanisa yao, lakini leo wanasoma paka watawa ndani ya monasteri yao.

Kila siku ya Mungu tunasoma Ingine sala ya Mesoniktiko. Tunasoma Kanuni moja ya utukufu ya Utatu Mutakatifu na kisha tunaimba wimbo ine. Tazama moja: "Inastahili kweli kukuimbia Utatu kamili kimungu uliye bila mwanzo; Baba Muumba wa vyote. Mwana wasipo mwanzo aliyezaliwa bila Baba, toka kwa Baba mbele ya milele, na Roho Mutakatifu aliyetoka kwa Baba mbele ya wakati".

Mbele ya kusoma Mesoniktiko, tunasoma sala ingine inayeitwa sala ya mwanzo. Ni ndani ya Kitabu Saa Kubwa. Kwa sababu hii sala ni kifupi, wanaweza waaminifu, mbele ya kuondoka ku kazi yao, ya kuisoma.

## ORTHROS

**(Sala ya asubuyi)**

Hii sala ni kupita urefu na utajiri kwa wimbo ya mbalimbali. Ni sala ya utukufu na ushukudu ya Mungu, kwa sababu alistahilisha watoto Wake ya kupitisha hii usiku na sasa wanaweza kuangalia mara ingine nuru ya mushana, mufano ya nuru ya kiroho ile inatokea kwa Yesu Kristu. Tena hi sala ni ombi ya kubariki Mungu matendo ya mikono yetu hii siku. Tena tunatukuza makumbusho ya Watakatifu ya hii siku.

Mpadri anasema: "Ahimidiwe Mungu wetu..." na msomaji anasoma Trisagio. Kisha wimbo tatu mbele ya ma zaburi sita (Eksapsalmos). Kundi ya ma zaburi sita anasoma mkubwa ya Kanisa. Yanatuonyesha kusali sisi kwa utukufu ya Mungu kwa kuomba huruma na wokovu yetu.

Tunasikia kundi hii ya zaburi sita, bila kutembea ao kutengwa, katika woga na unyamasha, bila kufanya alama ya musalaba ao kupiga magoti, kwa sababu hii somo ya Eksapsalmos inatuonyesha wakati ya uhukumu ya dunia toka Bwana wetu Yesu Kristu. Kwa hivi tunapaswa sisi kusimama sawa vile tutasimama ile siku ya uhukumu wetu mbele ya Kiti ya Mungu.

Kisha somo ya Eksapsalmos waimbaji wanaimba shahiri ya zaburi 118: "Bwana ndiwe Mungu, naye amefunuliwa kwetu, abarikiwe yeye ajaye kwa jina la Bwana". Wakati ya Kwarezima hatuimbe hii mwimbo, lakini mara inne Aliluya pamoja na ma shahiri yake.

Kisha msomaji anasoma Kathisma ya Zaburi. Kathisma ni kundi ya zaburi 3-4-5-6. Kisha msomaji mwingine anasoma kathisma ya mbili. Kitabu ya Zaburi iko na zaburi yote 150 na kila Juma watawa wanasoma hii Kitabu ya ma zaburi yote mara moja.

Kisha waimbaji wanaimba Mahimidi ya ufufuo ya kila siku ya Mungu. Kama ni siku ya Posho wanaimba mahimidi ya Wafu. Mbele ya kila mwimbo wanaimba hii shahiri: "Ee Bwana, umehimidiwa U, unifundishe zilizo haki zako".Kisha mahimidi waimbaji wanaimba Kathisma ya Mineon na kisha, kama ni ukumbusho ya Mtakatifu moja mkubwa, wanaimba Polyeleos. Ni wimbo ya ma zaburi 135 na 136. Kisha Polyeleos wanaimba wimbo ingine inayeitwa Eklogi, nikusema ni shahiri ya mbalimbali toka kitabu ya Zaburi.

Mwimbo ya Ypakoi tunaisoma mbele ya kuimba Anavathmi kila siku ya Mungu asubuyi. Kisha waimbaji wanaimba Anavathmi. Ni wimbo yenye aliandika Mtakatifu Theodoros wa Studitis. Kisha zamani walisoma Wimbo Tisa ya Agano la Kale, na moja wimbo toka Agano Jipya, lakini sasa tunasoma wimbo ya Watakatifu ya kila siku ingine Kanuni. Kisha mwimbo ya sita tunasoma Kontakion na Ikos ya Mutakatifu ya hii siku. Kisha Katavasies ya hii wakati na mpadri kisha atasoma Evangelio ya asubuyi. Kama ni siku ya Mungu atasoma Evangelio Eothinon. Kama ni siku ya Mutakatifu moja mkubwa atasoma ingine katika desturi ya Kanisa. Kisha msomaji atasoma: "Tukiona ufufuo wa Kristu, tumsujudu Yesu Bwana Mtakatifu aliye peke yake bila zambi. Tunausujudu msalaba wako...", Zaburi 50 (51). Wakati waimbaji wanaimba ma shahiri yote ya zaburi 50 (51) Mpadri anatoka inje ya kuchunga pa mikono yake Evangelio na anasimama kati ya Kanisa. Na waaminifu wanakuja ya kubusu Evangelio. Kisha wanaimba wimbo tatu na mpadri atasema hii sala: "Ee Mungu uwaokoe watu wako ukaubarikie urizi wako...". Kisha tunafika kwa mwimbo Tisa ya Mzazi-Mungu. Nikusema mpadri anasema mbele ya Picha ya Mzazi-Mungu: "Mzazi Mungu na Mama wa Nuru, tukimheshimu kwa nyimbo, na kumtukuza. Kisha waimbaji wanaimba hivi: Inamutukuza Bwana nafsi yangu na roho yangu imeshangilia katika Mungu Mwokozi wangu. " Uliye wa thamani kuwashinda Wakeruvi, uliye na utukufu kuwapita bila kiasi Waserafi, uliye ukimzaa Mungu Neno, umebaki bila kukuharibu, uliye Mzazi-Mungu kweli tunakutukuza wewe". Vile wataendelsha ya kuimba mara sita pamoja na ma shahiri. Kisha waimbaji wataimba mwimbo ya Tisa ya Katavasies na kisha mpadri atasema Synapti Kidogo.

Kisha waimbaji wanaimba Eksapostilaria, (nikusema tunaomba Mungu atutumie nuru yake) Tunaimba wimbo haya ao toka Mineon, ao toka Paraklitiki kila siku ya Mungu ao toka Saa Kubwa. Wakati ya Kwarezima tunaimba wimbo ingine, yenye yanaitwa Fotagogika (maana yao ni pamoja, nikusema tunaomba Mungu ya kujaa akili na uzima yetu kwa nuru ya kiroho Yake).

Kisha tunaimba wimbo ya Masifu. Masifu ni shahiri ta ma zaburi 148, 149, na 150. Kisha tunaimba Doksologia kubwa. Kisha hii Doksologia tunaimba mwimbo moja: hii "Leo wokovu ulifanyika duniani, tumwimbie mwenye kufufuka toka kaburi na mukubwa wa uzima wetu. Kwa sababu kwa lufu alibomoa mauti na alitupatia ushindi na rehema kubwa. Kisha mpadri ataanz aLiturgia Kimungu.

Kama hakuna Doksologia kubwa, tunasoma Doksologia Kidogo na kisha tunaimba Apostikha. Kisha mpadri anasema kundi moja ya maombi, Kuaga.

## MA IBADA YA SAA MAKUBWA

Ma Ibada ya Saa makubwa ni wa Ine. Ibada ya Saa ya Kwanza ya Tatu, ya Sita na ya Tisa. KIla Ibada inaikaa na ma zaburi tatu, kisha wimbo, Trisayo na wimbo ingine na ku mwisho ombi moja mbele ya Mungu. Ma Saa ya Kwanza tunasoma ndani ya Monasteri, kisha Ibada ya Asubuyi. Ma Saa ya Tatu na ya Sita tunasoma kisha wakati kidogo pamoja na Ibada ya Mzazi-Mungu na Ibada ya Saa ya Tisa tunaisoma mbele ya Ibada ya Magaribi. IBada ya Saa ya Kwanza ilifanyikwa tangu zamani ku saa ya kwanza asubuyi ya kila siku kusudi hii saa asubuyi inakuja nuru ya jua, ile ni mufano ya nuru ya Kristu, sawa Huyu Kristu ni nuru wa kweli.

Ibada ya Tatu inasomwa ku saa Tisa ya asubuyi, ku mwanzo ya kazi ya kila mtu na inatukumbusha kushuka Roho Mutakatifu hii saa ya asubuyi.

-Ibada ya Sita inasomwa ku saa ya kumi na mbili (12) kati ya muchana juu ya kutukubusha tendo ya Usulubisho ya Bwana Yesu Kristu.

Na Ibada ya Tisa inasomwa mu saa ya tatu, kisha kati ya muchana juu ya kutukubusha lufu ya Bwana Yesu Kristu pa Musalaba yake.

Ma Ibada Makubwa tunasoma mara tatu kila Mwaka. Tukona ma Ibada ya kusoma kwa Siku ya Tano Mkubwa, mbele ya Ufufuo ya Kristu, kisha tunasoma Ibada ingine ya Saa ya siku Kuu ya Ubatizo ya Kristu, mu tarehe 6 ya mwezi ya Yanuarie na Ibada ya ma Saa mbele ya Siku Kuu ya Kuzaliwa Yesu Kristu. Katikati ya ma Saa haya tunasoma somo ya Unabii, kisha Matendo ya Mitume (Apostolos) na Evangelio. Ile wakati waimbaji wanaimba wimbo ya kila Saa, mpadri anafukiza na chetezo kidogo (bila kengele) waaminifu ndani ya kanisa.

### NAMNA GANI TUNAINGIA NDANI YA KANISA

Kama tunakamata mpango ya kuingia ndani ya kanisa kusali, tunapaswa tangu mwanzo ya kusadiki ya kama tunaingia ndani ya fasi moja takatifu, fasi ya kusali, pahali ni na Mungu bila kuonekana, mwenye ni Mufalme ya wafalme. Tena tunapaswa kujua ya kama kila mara tunaingia kanisani, tunaongeza utakaso na baraka kimungu ku Mungu. Kwa hii jambo, tunapaswa kuingia na unyamasha. Mwendo yetu itafanyika na woga ya Mungu, bila makelele na vitengo ya bure. Tunapaswa kuonyesha kwa mufano yetu yote ya kama tunaingia ndani juu ya kuchukua baraka kimungu na Neema Takatifu.

**1. Tunawaka mushumaa**

Kama tunaingia ndani, tunafanya alama ya Musalaba ya kuinamisha kichwa yetu kusema: "Unifanye njia yako wazi mbele ya uso wangu kwa maana hapana uaminifu kinywani mwao" (Zaburi 5,8). Kama tunataka kunyoloka ya kununua mishumaa moja ao mbili. Tunawaka mushumaa moja kwa sifa na Jina ya Kristu, ingine kwa Jina ya Mzazi mwake Mama Maria na ya Watakatifu Wake na ingine juu ya wokovu ya ma nafsi ya wa ndugu wetu, wenye waliisha kufa na wenye muzima. Sau tunawaka mushumaa moja kwa jina ya hawa watakatifu na watu wote. Wakati wanawaka mushumaa zetu tunasoma sala moja ndani ya akili yetu: "Ee Kristu wangu, weye ni Nuru ya dunia. Unisaidie juu na uzima yangu kuwa sawa mushumaa juu ya kulekea kwa upendo mbele ya mukaribifu yangu na tena ninataka uzima yangu kuwa chini ya nuru ya Bwana Mungu wangu".

**2. Busu ya ma Picha ya Watakatifu**

Kisha tunanyoloka pa ile fasi ni ma Picha ya Watakatifu mbele yetu, pa fasi yao. Tunapika magoti ao mara moja ao mara tatu na tunafanya pamoja na alama ya musalaba na kisha tunabusu ma Picha ao Mifupa ya Watakatifu. Mara moja tunasema ndani ya akili yetu hii sala: "Bwana Yesu

Kristu, unihurumie ao Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu Maria, uniokoe ao Mutakatifu (fulani, jina lake) utuombee kwa sisi wote ao sala ingine ile anataka huyu mwaminifu. Kisha tunatembea pempeni, bila kuuzi waaminifu weingine wenye wanaingia ndani.

**3. Mavazi yetu.**

Hatuingie ndani ya kanisa na mavazi yoyote. Tunaingia na mavazi mabaya hii inaonyesha ya kama hatuingie na heshima, wala na sifa, lakini na uzarau mbele ya Mungu na ya Watakatifu.

Ni kweli ya kama Mungu hana na lazima ya mavazi yetu mazuri, kwani eko na mafaha ya hali ya roho yetu, lakini sisi tunalazimishwa kusimama mbele ya Mungu na ndani ya kanisa katika heshima. Nikusema tunaweza kuingia ndani ya kanisa na kapitula kifupi? Tunaweza kuingia ndani ya nyumba ya mufalme ya inchi yetu na kapitula mufupi ao nyumbani ya mkubwa ya wa askari?

Tena na wanawake, hapana wote, wanaingina kanisani ya kuvaa pantalone, mupila, bila mikono ao manguo ingine mabaya na wanakuja ya kuchukua na Komonyo Takatifu. Lakini Kanisa, sawa vile inatuwaambia na Biblia Takatifu haibariki hii mavazi. Sasa juu ya nini hawa wanawake wanaendelea kuvaa hivi na namna mbaya? Wanataka Mungu ya kubadilisha sheria Yake? Juu ya nini hawa wanawake wanataka kuleta kikuao mbele ya watu weingine? Wekona mavazi mengi nyumbani yao. Kama, wanataka watashona na mavazi mbili juu ya kuingia kanisani ya Mungu! Inalazimishwa, kwani hivi watachukua ma baraka minene!

Tena waaminifu inapaswa kuangalia na vilato vyao. Haipaswe kuvaa vilato yenye yanaleta makelele, kwa sababu watu weingine wanapindula vichwa vyao kuangalia nani aliingia ndani. Lakini hivi tunaharabisha sala ya waaminifu.

Kama mtu moja anataka kuingia kanisani, inapaswa kutayarishwa katika mwili na kiroho yake. Faida kubwa tunakamata kama tunaangalia kabisa matayarisho ya kiroho yetu. Yesu Kristu anataka sisi kumupenda katika roho na nafasi na akili yetu. Lakini kama mama moja, mbele ya kuingia kanisani, anasimama saa nyingi mbele ya rikalasi juu ya kutayarisha uso na manguo yake, atasema nini mbele ya Kristu, wakati atakuja kanisani? Hii matayarisho yake ni nzuri juu ya kukomunyika?

Ao, mwanamuke mwingine, asubuyi mapema anaanza kuweka ragi nyekundu pa midomo ya kinywa chake ao ragi ingine pa fasi ingine ya mwili yake. Huyu inapaswa kujua ya kama Yesu Kristu hakuna namna ya kumubariki, kwani hasipende hii matayarisho ya mwili Yesu Kristu, kupita ya matayarisho ya kiroho. Namna gani atakomunyika na midomo yake ya kuweka ragi nyekundu nyingi? Ao aliweka pa ma macho yake ragi meushi? Inapaswa huyu mama kujua ya kama kwa hii matendo yake hasijue anatafuta nini na anataka nini. Tena kwa hii ragi pa midomo yake, anachafuka makalasi, ni mbele ya Picha ya Watakatifu.

**Fasi gani tunapaswa kusimama.**

Bila kutembea na kelele na bila kusalimia waaminifu weingine tunaenda kukamata fasi yetu ndani ya kanisa. Kama tukona tambia katika sheria ya Mungu, hatutafute fasi ku mbele juu ya kutusifu watu weingine ao wapadri. Kama tunaingia na wasomaji wanasoma Eksapsalmos (kundi ya ma zaburi sita) ku mwanzo ya Ibada ya asubuyi, hatutembee. Tena, kama padiri anasoma Evangelio, hatutembee, lakini tunasimama mpaka itaisha somo ya Evangelio. Ile wakati padiri anatoka inje ya kukamata pa mikono yake na Vitu Vitakatifu, hatupike magoti, kwa sababu bado kutakaswa haya Vitu Vitakatifu. Tunapika magoti kama tunafanya Liturgia Proigismeni (Vitu Vitakatifu yalitakaswa tangu siku ya Mungu ya zamani). Kama padiri anasimama mbele ya mulango bora na anasema: "Kwa woga wa Mungu, na imani, na mapendo, gongeeni", haipaswe waaminifu ya kuikaa chini, kwani Kristu ni mbele ya macho yetu.

Kama ni kivukutu, hatuondoke inje na mara ingine tunarudia na mara ingine tunatoka inje. Hii zoezo inauzi watu weingine. Ndani ya kanisa hatuimbe pamoja na waimbaji kwa sababu tunafanya makelele na waaminifu weingine hawaweze kusali.

Kama tunataka kubusu ma Picha ya Watakatifu, wenye ni pa Ikonostasi, tunaweza kubusu kisha mwisho ya Liturgia, ao ku mwanzo yake. Ku mwanzo tunabusu Picha ya Yesu Kristu, kwani tunamuabudu sawa Mumba na Mwokozi wetu. Kisha tunabusu Picha ya Mzazi mwake na

Watakatifu, sawa Picha ya Yoane Mubatizaji na ma Picha ingine. Tunakataa kubusu ma Picha ile saa Ibada inaendelea.

**Kuondoka inje ya Kanisa**

Kama tunaenda kusali kanisani tutaondoka ku mwisho ya Liturgia, halafu ku mbele tutabeba antidoro ku mukono ya padiri na tutabusu mukono yake. Hatuondoke mbele ya hii sala anasema padiri: "Kwa maombezi ya Watakatifu wapadri wetu..." kwa sababu tunafanana na mufano ya Yudas, aliyeondoka ku meza ya Mwalimu na wanafunji wote. Inakatazwa kusalimiana sisi ndani ya kanisa, mbele ya mwisho ya Ibada ya Liturgia. Kanisa ni nyumba ya Mungu japo itaisha Ibada ya Liturgia.

Kama kisha tunataka kumukuta padiri, tunamusalimia kusema kwake: "bariki ee padiri na tunabusu mukono yake". Kama tutabusu padiri pa njia, tunamusalimia hivi" Bariki ee padri", na tunabusu mukono yake na huyu atatujibu: "Mungu akubariki, mtoto wangu".

**Kuingia ndani ya Altari takatifu.**

Inakatazwa katika hamuri ya Kanuni 69 ya Makutano Ikumeniki (ya ulimwengu) ya Sita juu ya kuingia wanawake ndani ya Altari Takatifu. Hata wanaume inakatazwa kuingia, kama hawakuwa na kazi fulani. Inajiruhusu kuingia wanawake ao watawa wanawake, kama weko na kazi ya kusafisha fasi hii katika baraka ya askofu.

Altari Takatifu ni fasi ya Vitu Vitakatifu na wanaweza kuingia paka wapadri juu ya kutoa sandaka mbele ya Mungu na ma Ibada ingine. Hii hamuri waliheshimiwa na wafalme na walikataa kuingia ndani.

Hawa watoto ao watumishi ya Kanisa inapaswa kuingia ndani ya Altari Takatifu inapaswa kujua ya kama wataingia:

-katika heshima na woga ya Mungu

-ya kutembea ndani katika heshima na hapana na haraka.

-Watamusaidia mpadri bila kuzungumuza ao kucheka katikati yao ao pamoja na padiri, kwani ni zambi mnene.

- Inapaswa kuwaza ya kama Mungu ni karibu yao, anawaangalia na sawa Mwana Kondoo ni pa Sahani Takatifu.

Ni zambi mnene kuingia ndani ya Altari bila woga ya Mungu, kwa sababu Mungu ni karibu yetu pa Meza takatifu ndani ya Artoforio na ndani ya Sahani Takatifu. Kama kwa mufano anasimama karibu yetu mufalme moja, sisi tukona ruhusa ya kuikaa ao kuzungumuza katikati yetu?

Mpadri inapaswa kufundisha hawa watoto wenye wanaingia ndani ya Altari, kwa sababu hawajue kitu. Fundisho padiri atafanya na kwa watu wakubwa kwa sababu na hawa hawajue kitu.

## WAKATI GANI TUNAPASWA KUSIMAMA NDANI YA KANISA

Namna gani tutasimama ndani ya Kanisa, haiko kazi katika mapenzi wetu, lakini inatokea ku mapokeo takatifu ya Kanisa. Kwa mufano shemasi, ile siku ya upandirisho yake juu ya kuwa shemasi, mbele ya Meza atapika paka na rigoti moja, lakini padri atapika na magoti yake ya mbili. Ile wakati ya Kwarezima na ile siku ya Kupandisha Musalaba ya Kristu mapokeo Takatifu ya Kanisa inatuelejea tutapika magoti mara ngapi. Ile siku ya Magaribi, kisha Siku Kuu ya Pentikosti, Ibada inatuelejea wakati gani tunapaswa kupiga magoti.

Ni zoezo ndani ya kanisa waaminifu wote kusali ya kusimama, kwa sababu hii usimamisho yao inaonyesha uhuru yao. Hawa weko watu wahuru na hapana watumwa ya kuikaa chini. Hawa waaminifu ni wazee ao wagonjwa wanaweza kuikaa, lakini watasimama kama Ibada ya Liturgia ao Ibada ingine ilifika pa fasi moja takatifu kabisa.

Kwa hivi, wakati gani tunapaswa kusali ya kusimama na wakati gani tunaweza kuikaa ya kupumuzika kidogo?

**Mu Ibada ya Magaribi:**

1.Wakati padiri ataanza kusema: Mwimidiwa Mungu wetu daima, sasa na siku zote, hata milele na milele", mpaka mwisho ya Zaburi 104 tunasali ya kusimama. Kisha padiri anasoma kundi ya maombi (Sinapti kubwa) tunaweza kuikaa.

2. Tangu mwimbo: "Bwana nimekuita..."mpaka mwisho ya kufukiza na chetezo mpadri inakatazwa kuikaa. Ile saa mpadri inatufukiza na chetezo sisi waaminifu hatufanye alama ya musalaba, lakini tuinamisha kidogo kichwa chetu ku mbele kama shukrani mbele ya Mungu.

3. Wakati mpadri ni tayari ya kutoka inje afanye Kuingia pamoja na chetezo, sisi tunapaswa kusimama tangu ile dakika waimbaji wanaanza kuimba mwimbo pamoja na "utukufu kwa Baba...".

4. Wakati msomaji ao padiri anasoma hii sala: " Ee Bwana, utujalie mangaribi hii kutulinda na zambi,...″. sisi tunasimama.

5.Ile saa mpadri anasoma kundi ya maombi na anatoka inje kusema: "Amani kwa wote", sisi tunapaswa kusimama. Kisha atasema: "Vichwa vyetu tuinamisha kwa Bwana", sisi tunaendelea kusimama na vichwa vyetu tuinamisha kidogo ku mbele.

6. Tena tunasimama tangu ile saa mpadri atasema: "Sasa Bwana, umuache mutumishi wako..." mpaka mwisho ya hii sala ya Magaribi.

Tangazo: Kama waaminifu wanasikia ombi ya Mzazi-Mungu, ni nzuri ya kusimama kwa kuonyesha heshima yao mbele ya Mzazi-Mungu.

Kama waaminifu wanaweza kusimama ndani ya Kanisa, bila kuikaa, haiko kosa yao. Ni mufano nzuri, kwa sababu wanakombana juu ya kuangalia na kusikia nzuri maombi na ma sala yote.

**Mu Ibada ya Asubuyi.**

1. Tangu mwanzo ya hii Ibada tunasimama, kwani mpadri anaanza kusema: Muhimidiwe Mungu wetu...". Hivi tutaendelesha kusimama mpaka mwisho ya Eksapsalmos.

2. Tunasimama kama waimbaji wataanza kuimba: "Bwana ndiwe Mungu naye..."mpaka ku mwisho ya kuimba Apolitikia yote.

3. Ile saa wasomaji wanasoma Kontakion, Ikos na Synaksari ya Watakatifu tunapaswa kusimama.

4. Ile wakati waimbaji wanaanza kuimba wimbo ya Mzazi-Mungu: "Uliye wa thamani kwa shinda wa Kheruvi..." Hii saa tunashuka chini ya biti vyetu ao tunasimama.

5. Kila mara mpadri anasoma sala ya Mzazi-Mungu sisi tunasimama na tunafanya alama ya Musalaba wetu.

6. Kama tunasikia ya kama waimbaji wanaimba Doksologia Kubwa tunasimama mpaka mwisho ya hii Doksologia.

**Mu Ibada ya Liturgia Takatifu.**

1. Wakati mpadri anaanza Liturgia na anasema" Haimidiwe ufalme wa Baba..." tunapaswa kuwa ya kusimama.

2. Wakati waimbaji wanaimba Antifonon ya Kwanza ya Mbili na ya tatu tunakuwa ya kusimama.

3. Ile saa mpadri anafanya Kuingia na Evangelio, tunasimama.

4. Wakati waimbaji wanaimba Trisayo: Mungu Mutakatifu...".

5. Ile saa mpadri anasoma Evangelio. Waaminifu wanaweza kuikaa ile saa msomaji anasoma Apostolos (Matendo ya Mitume).

6. Ile saa waimbaji wanaimba Mwimbo ya Kheruvikon na mpadri anafukiza na chetezo ma Picha ya Watakatifu ya Ikonostasi.

7. Ile saa mpadri anafanya Kuingia Kubwa pamoja na Vitu Vitakatifu waaminifu wanashuka chini ya kiti yao na wanainamisha vichwa vyao.

8. Ile saa mpadri anasema Kundi ya maombi mengi (Plirotika) na anasimama inje ya kutubariki, sisi tunapaswa kusimama.

9. Ile saa wasomaji wanasoma Symvolo (Fundisho) ya Imani. Kisha mpadri anasema: "Tusimame vizuri! Tusimame na woga! Tusikilize kwa kutolea sadaka takatifu kwa amani" sisi tutasimama mpaka mwisho ya Liturgia, kwa sababu tangu hii dakika inaanza Fumbo Takatifu ya Komonyo.

10. Ile saa tunasoma sala ya Bwana: " Baba yetu uliye mbinguni..." mpaka ile saa mpadri anasema: "Tusikilize, Vitu Vitakatifu kwa watu watakatifu".

11. Kutoka hii sauti ya mpadri: "Kwa woga wa Mungu, na imani, na mapendo, gongeeni″, mpaka mwisho tunasimama.

## WAKATI GANI, NAMNA GANI NA KWA NINI TUNAFANYA ALAMA YA MUSALABA

1. Tunafanya alama ya musalaba pa kifuo (kilari) yetu ku mwanzo ya kila Ibada.

2. Kama tunasikia jina ya Utatu Mutakatifu, ao jina ya Uso moja ya Utatu Mutakatifu. Nikusema, ile saa tunasikia: Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu...

3. Kama tunasikia jina ya Mzazi-Mungu Bikira Maria.

4. Kama tunasikia ma jina ya Watakatifu, wenye tanashanglia hii siku.

5. Wakati waimbaji wanaimba wimbo ya Mzazi-Mungu: "Uliye wa thamani kwashinda wakheruvi..".

6. Ile saa mpadri anapita mbele yetu kuchunga na Evangelio juu ya kufanya Kuingia Kidogo na Kubwa pamoja na Vitu Vitakatifu.

7. Kama waimbaji wanaimba Trisayo: "Mungu Mutakatifu, Mweza Mutakatifu...".

8. Kama tunasikia hii: "Njooni tumwinamie na tumsujudu Mungu Mfalme wetu. Njooni tumwinamie na tumsujudu Kristu yeye Mungu Mfalme wetu. Njooni tumwinamie na tumsujudu yeye Kristu, aliye Mfalme na Mungu wetu".tunafanya mara tatu alama ya Musalaba.

9. Ile saa mpadri anasema hii ombi: "Sasa Rabi, umuache, mutumishi wako..."

10. Kama ni mwisho ya ma Ibada ya Magaribi, ya Asubuyi na Liturgia Kimungu.

11. Kila mara, kama anataka mwaaminifu katika mapenzi yake.

12. Mbele ya kukomunyika.

13. Ile saa tunabusu ma Picha ao Mifupa ya Watakatifu.

14.Ila saa tunawaka mushumaa yetu.

15. Ile saa tunaingia ndani ya Kanisa ao wakati tunaondoka inje.

## WAKATI GANI HATUFANYE ALAMA YA MUSALABA

Katika sheria na mapokeo ya Kanisa yetu, sawa vile ilikuwa tangu zamani, hatufanye musalaba yetu, hivi:

1.Ile saa mpadri anatufukiza na chetezo, hatufanye alama ya musalaba. Ku mwanzo anafukiza ma Picha ya Watakatifu, kisha anatufukiza na sisi, kwani na sisi tuko ma Picha wa Mungu! Hii dakika, kama tunaikaa, tunapaswa kusimama.

2. Ile saa, ku mwanzo ya Ibada ya Asubuyi, wasomaji wanasoma Kundi ya zaburi Sita (Eksapsalmos). Musalaba yetu tunaweza kuifanya ku mwanzo ao ku mwisho ya hii Eksapsalmos, lakini hapana katikati ya ma zaburi. Katikati ya ma zaburi tunasema: "Utukufu kwa baba..." hapa hatufanye alama ya musalaba pa kifuo (kilari) yetu. Hii wakati tunasoma Eksapsalmos inatuonyesha wakati ya uhukumu ya dunia nzima ku mwisho ya dunia na tunasima ya kusikia na woga na angalisho.

3. Wakati tunabusu mukono ya mpadri yetu. Ni kosa, kama waaminifu mbele ya kubusu mukono ya mpadri ao askofu, wanafanya na musalaba yao. Musalaba tunafanya kama tunabusu ma Picha ya Watakatifu na hapana, wakati tunabusu mukono ya padiri yetu. Kama tunakuta mpadri moja, tunamusalimia hivi: "Bariki ee mpadri ao baraka yako ee Rabi ao Mweshimiwa, ao mpadri mkubwa. Kisha tunainamisha kidogo kichwa chetu na tunamubusu mukono na tunaendelesha zungumuzo naye. Kama tunaondoka tunamusalimia hivi: "Baraka yako, ee mpadri, ao unibariki ee mpadri".

4. Kama tunachukua Antidoro (kipande ya mukate ku mwisho ya Liturgia), tunabusu mukono ya padiri yetu.

## WAKATI GANI TUNAFANYA ALAMA YA MUSALABA INJE YA MA KANISA YA KRISTU

1. Mbele ya kisha ya kula (ndani ya nyumba, inje ya duka ya kula, pa njia ao pa fasi ya bahari ao ya pori).

2. Kama asubuyi tunaondoka inje ya nyumba yetu.

3. Kama tunaanza ao tunaisha kazi yetu moja.

4. Kama tunataka kufungula duka ao nyumba yetu, tunafanya alama ya musalaba pa kafuri ao pa funguo.

5. Kama tunapita inje ya ma kanisa Orthodokse ya Kristu na ya Watakatifu.

6. Kama inje, pempeni yetu inapita kundi ya kiliyo na maiti ya mufu moja, sisi tunasimama na heshima, tunafanya alama ya musalaba na tunaongojea juu ya kupita mustari ya watu.

7. Kama inapita karibu yetu Epitafios ao kujuguluka pamoja na Mifupa ao ma Picha ya Watakatifu.

8. Kama mpadri moja anatembea inje na anapeleka kwa wagonjwa Komonyo Takatifu sisi tunachofa pempeni, tunafanya musalaba yetu na tunaongojea katika heshima juu ya kupitisha mpadri na Komonyo Takatifu.

9. Kama tunapata jambo moja ya hatari ao tulipata hatari moja, tunafanya musalaba yetu pamoja na sala: "Bwana Yesu Kristu, Mwana wa Mungu, unihurumie".

10. Kama tunaenda ya kusafiri, ao kama tulifika pa fasi ile tulipenda ao kama tutarudia ku safari yetu tunamushukuru Mungu na tunafanya alama ya Musalaba.

11. Kama yanakuja ndani ya roho na akili yetu mawazo mabaya ya zambi ya uzini na usharati tunafanya alama ya musalaba na tunaomba saidio toka Mungu.

12. Mbele ya kila kavumu ya furaha ao ya sikitiko tunafanya musalaba yetu juu ya kumushukuru Mungu.

Kanisa yetu iko na heshima kubwa mbele ya Musalaba ya Kristu na inaitimia pa fasi yote ya matendo na ma Ibada yake. Kwa hivi tunaona musalaba ndani ya Vitabu ya Kanisa, ndani ya vimbambashi (ukuta) ya kanisa, katikati ya ma Picha ya Watakatifu, pa Vitu Vitakatifu (Kimombe na Sahani Kitakatifu na ingine).

Vile na sisi mu uzima yetu kila siku, asubuyi, kati ya muchana na magaribi tunaanza na musalaba na tunaisha na musalaba, kwani hivi tunasadiki ya kama tutapata ma baraka mnene ya uzima yetu.

Baraka itakuja kubwa kama sisi tunafanya alama ya Musalaba katika unyenyekvu na hapana katika majivuno. Katika roho usafi na hapana ku roho ya tamaa.

Tena tunapaswa kufanya musalaba wetu na namna nzuri na bila kosa, hapana na haraka, hapana na haya, hapana ya kutenga mukono yetu pa pepo, hapana sawa tunacheza na baragumu na kinubi. Haipaswe kufanya ma alama ya musalaba mengi juu ya kuonyesha ya kama tuko waaminifu wazuri. Tena hatufanye alama juu ya kupata utukufu toka watu ya dunia, kwa sababu anatuwambia Kristu: "Kila mutu anayenikiri mbele ya watu, nitamukiri vilevile mbele ya Baba yangu aliye mbinguni. Lakini kila mutu anayenikana mbele ya watu, nitamukana vilevile mbele ya Baba yangu aliye mbinguni".

5. Alama ya Musalaba inafuchika ndani yake matendo ya wokovu yote, yenye yalitokea kwa upendo kubwa ya Mungu wetu juu ya wokovu ya kila mtu. Kwa hivi ni alama ya wokovu, alama ya uzima ya milele, alama ya utakaso. Kwa hivi na sisi tunapaswa kuitimia mara mengi katika heshima na woga ya Mungu.

## JUU YA NINI TUNAFANYA ALAMA YA MUSALABA

Kila mara, wakati tunafanya musalaba wetu, tunafanya kwa sababu yenye yafwatayo:

1. Kwa sifa na kuabudu ya Utatu Mutakatifu juu ya kutufunika sisi Neema ya Roho Mtakatifu.

2. Kwa sifa ya Mzazi-Mungu na

3. Kwa sifa ya Watakatifu wetu juu ya kuomba saidio na maombi yao.

4. Kwa sifa ya hii tendo inafanyika hii dakika. Kwa mufano kama inapita Evangelio, ao yanajuguluka Mifupa ao Epitafios ya Kristu...

5. Wakati tukona ulazimisho moja na tunaomba juu Mungu atutumie saidio yake.

6. Wakati kila mara tunaomba baraka ya Mungu mu uzima ao jamaa ao wa ndugu wetu.

7. Juu ya kufukuza majaribu na mitengo ya shetani.

8. Juu ya kuonyesha katika unyenyekevu mufano yetu ya kama tuko Wakristiani, ile saa waaminifu weingine wanaogopa kufanya mbele ya watu weingine alama ya musalaba yao.

9. Kwa kumushukuru Mungu kwa ajili ya mafazili na ma saidio yake yote.

## NAMNA GANI TUNAFANYA ALAMA YA MUSALABA

Ku mwanzo tunaungana vidole yetu tatu ya mukono ya kuhume na hivi tunaonyesha ya kama tunasadiki kwa Mungu moja katika ma Nyuso Tatu: Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Ma Nyuso Mtakatifu Haya weko na asili moja, nguvu moja na bila kugawanywa. Vidolo vingine vya wili

tunaungana pamoja chini juu ya kuonyesha ya kama tunasadiki kwa asili wa wili ya Kristu, nikusema Yesu Kristu, wakati alikuja duniani aliishi na asili kimutu na kimungu. Kwa hii namna ya alama ya Musalaba tunaonyesha Ukikiri wetu ya Imani Orthodokse. Hii Imani yetu ni usingi ya fundisho Ukweli ya Kanisa Ortodokse.

Mukono hii ya kuhume tunaileta pa sula yetu, pahali ni akili yetu juu ya kuonyesha hivi ya kama tunamupenda Mungu katika akili yetu yote na tena tunamuonyesha ya kama tunamutoa Kwake mawazo yetu yote.

Kisha mukono yetu tunaiweka pa tumbo yetu. Hivi tunaonyesha ya kama tunatoa kwa Bwana matakio yetu na mahasa yetu yoyote.

Kisha tunaleta mukono yetu pa ribeka yetu ya kuhume na kisha ya kushoto juu ya kuonyesha hivi ya kama tunamutoa Kwake nguvu na kila tendo yetu pa Mikono Yake.

Ufafanusho ingine kabisa nzuri tunapata toka Mtakatifu Kosmas wa Etolos. Huyu alisema hivi kwa fundisho yake:

"Wakristiani wangu, munisikie, namna gani tunapaswa kufanya alama ya musalaba yetu na ni nani maana yake. Evangelio Takatifu inatwaambia ya kama Utatu Mutakatifu na Mungu Moja anatukuzwa mbinguni kupita nyingi ya Malaika wote. Na weye unapaswa kufanya nini? Unganisha vidole yako tatu ya mukono ya kuhume na, kwa sababu hauweze kupanda mbinguni juu ya kumusujudu Mungu, unaweka mukono yako pa sula yako, kwa sababu kichwa chako ni sawa muviringo na inaonekana sawa mbingu na unasema pamoja na kinywa chako: "Sawa vile ninyi Malaika munamutukuza Utatu Mutakatifu mbinguni, vile vile na mimi, sawa mutumwa musiyestahili ninatukuza na ninasujudu Utatu Mutakatifu. Na sawa vidolo yako haya ni tatu na pamoja vile na Mungu ni Moja katika ma Nyuso Tatu: Baba , Mwana na Roho Mtakatifu.

Kisha unashuka mukono yako ku kichwa chako na unaiweka tumboni mwako na unasema: "Ee Bwana wangu, ninakusujudu na ninakuabudu, kwa sababu ulikubali kufika duniani ndani ya tumbo ya Mzazi Mwako kwa ajili ya zambi zetu. Kisha unaweka mukono yako pa ribeka ya kuhume na unasema: "Ee Mungu wangu, unihurumie na uniweka pa fasi ya kuhume pamoja na hawa wenye haki. Na kisha unaweka mukono yako pa fasi ya kushoto na unasema: "Ee Bwana wangu, ninakuomba usiniweke pa fasi ya kushoto pamoja na hawa wenye zambi. Kisha unaangalia chini na unasema: Ee Mungu wangu, ninakusujudu na ninakuabudu, kwa sababu, sawa vile uliwekwa kaburini, hivi na mimi nitawekwa. Na, wakati unasimama, unaonyesha Ufufuo Wake na unasema: "Ee Bwana wangu, ninakusujudu na ninakuabudu, kwani ulifufuka toka wafu kwa kutupatia uzima ya milele". Hii ni maana yote ya Musalaba ya Kanisa Orthodokse.

## NAMNA GANI TUNAFANYA NDANI YA KANISA PA MA IBADA YA MBALIMBALI

**1. Ile saa mpadri anatufukiza na chetazo.**

Mpadri anafukiza Altari Takatifu, ma Picha ya Watakatifu na waaminifu wote ndani ya ibada ya Magaribi, ile wakati wimbaji wanaimba: "Bwana nimekuita..." na kama anafanya ibada ya Asubuyi anafukiza, ile saa waimbaji wanaimba: "Uliye wa thamani...". Tena mpadri anafukiza na chetezo, ile saa waimbaji wanaimba Doksologia kubwa, mbele ya mwanzo ya Liturgia, ile saa ya kusoma Matendo ya Mitume (Apostolos) na ile saa wanaimba mwimbo ya Kheruvikon.

Mukristu moja mbele ya mpadri anayemufukiza na chetezo hasifanye musalaba yake, lakini anainamisha kichwa chakje sawa shukrani mbele ya mpadri, kwa sababu anastahiliwa kumusifu mpadri, sawa alisifu ma Picha ya Watakatifu kwa kuwafukiza na ubani.

**2. Ile saa mpadri anatuwambia ya kuinamisha kichwa chetu.**

Mpadri anasema: "Vichwa vyetu kuinamisha kwa Bwana". Hii sauti mpadri anasema mara moja ndani ya sala ya Magaribi, mara moja ndani ya sala ya asubuyi, mara moja ndani ya Liturgia, kisha somo ya sala: "Baba yetu uliye mbinguni..."

Mpadri kisha hii hamuri ya kuinamisha wakristu vichwa vyao, kisha anasoma na sala moja. Hii tendo ya waaminifu inaonyesha ya kama wanamufamia Mungu sawa Rabi na Baba wao na sasa sawa watumwa wenyenyekevu wanamuomba kuwahurumia kwa kila ulazimisho yao. Hivi taifa ya

waaminifu wanaonyesha ya kama wanasikia mpadri anasema nini na anafanya nini ndani ya Kanisa, bila kuonekana makelele ao kuwa uvivu na uzaifu kati ya wakristu.

**3. Ile saa mpadri anatubariki.**

Mpadri kila wakati anatubariki kusema: "Amani kwa wote", ao: "Neema ya Bwana wetu Yesu Kristu...".

Baraka ni katika neno ya mpadri kitoleo ya neema ya Mungu mu uzima ya wakristu. Mpadri anasema hii neno mara mengi kati ya ma Ibada yote. Huyu anayechukua hii baraka anapata hali ya ajabu kimungu ndnai ya uzima yake. Abrahamu alikuwa mtu mutajiri kupita ya watu weingine ile wakati yake, kwa sababu alikuwa mtu mubarikiwa toka Mungu

Basi, ile saa mpadri anatubariki, Waaminifu wanasimama na haraka, wanainamisha vichwa vyao, wanamushukuru Mpadri kwa hii zawadi yeye anawapatia kwa kuwabariki. Kama hawafanye hivi, inaonekana ndani ya kanisa moja uvivu na mpadri anawabariki, lakini Wakristu wanaikaa na uvivu na bila angalisho.

## MATOLEO NA KITOLEO YA MUKATE

Matoleo yote yenye yanajitoa juu ya kumaliza mpadri Fumbo ya Komonyo Takatifu, sawa mukate, vinyo, mafuta, mishumaa na ubani yanaitwa matoleo ao zawadi.

Waaminifu wanafanya mukate moja sawa muvirigo, inayeitwa Prosforo na hii inaonyesha ya kama Mungu hana na mwanzo na mwisho na wanaitoa Kanisani juu mpadri afanye Fumbo ya Komonyo Takatifu. Kanisa Orthodokse inafanya Prosforo ya kutimia na levire kwa sababu na Yesu Kristu mu Karamu Kubwa alitimia mukate na lavire. Lakini Kanisa ya papa ya Roma wanafanya mukate sawa muvirigo kidogo bila levire.

Hii mukate inayeitwa Prosforo ikona juu yake alama ya Musalaba ya kristu na ma sauti: IS KR. NI KA, nikusema Yesu Kristu anashindi (ni Mushindi). Pempeni ya hii Alama ni Alama ya majeshi Tisa ya Malaika yote na pa fasi ya kushoto ni alama ya Mzazi-Mungu.

Vinyo pamoja na ngano na mafuta ni ma zawadi ya Mungu yenye anawapatia kwa watu. Kisha ya kuitimia Kristu vinyo mu Karamu Kubwa, kisha ilibarikiwa, ilitakaswa na inajitimia ndani ya Kanisa ya Kristu mpaka hapa sasa.

Vinyo mpadri anatimia juu ya Fumbo ya Komonyo. Anaiunganisha pamoja na maji. Vinyo inapaswa kuwa nyekundu juu ya kufanana na Damu ya Kristu. Hii unganisho inatukubusha Damu na Maji ile ilitokea toka Mbavu ya Bwana Yesu Kristu wakati alisulubiwa. Unganisho inaonyesha Damu ya kivukutu ya Mwili ya Kristu na imani ya kivukutu ile inapaswa kuwa na waaminifu, wakati wanataka kukamata Komonyo Takatifu.

Mukate na mafuta na vinyo tunatimia, ile wakati mpadri anafanya Ibada ya kubariki mikate Tano (Artoklasia).

Ku Fumbo ya Ndoa mpadri anatimia vinyo kwa ukubusho ya Komonyo Takatifu na ya kutuonyesha ya kama hawa vijana wa wili watavumilia pamoja kila mateso na machungu ya uzima yao, sawa na vinyo inaikaa kidogo utamu na kidogo uchungu. Hivi ni na uzima yao unganisho katika mafuraha na machungu ya uzima yao.

Kama askofu moja anafanya Ubatizo ya Kanisa moja mupya anatimia vinyo.

Kama tunatosha mifupa ya wafu tunayasafisha na vinyo.

### Kama ni mwanzo ya Kwarezima kubwa (mbele ya Pasaka)

Kwa kuingia Mwaaminifu moja ndani ya wakati ya Kwarezima ya Pasaka inapaswa kuongezeka matendo yake ya kiroho. Nikusema atakombana ya kuangalia matendo haya:

1.Ataongeza sala yake nyumbani mwake, asubuyi na magaribi.

2. Atajaribu juu ya kufata ma Ibada yote ya hii wakati ya Kwarezima. Nikusema kila asubuyi atafata Ibada ya Kati ya usiku, sala ya asubuyi, ma Saa ya Kwanza na sala ya Magaribi. Kila siku ya Kwanza, ya Mbili, ya Tatu, ya Ine, na ya Tano atafata magaribi sala ya Apodipno Kubwa. Kila siku ya Tano atafata Ibada ya Akathisti ya mzaziMungu. Muposho inafanyika Liturgia juu ya pumuziko ya wafu. Magaribi Sala ya Magaribi na siku ya Mungu Liturgia kimungu ya Mtakatifu Bazile. Kisha Evangelio ya asubuyi tunaimba wimbo ya sikitiko ya roho yetu kwa ajili ya zambi zetu. Ni haya:

"Unifungulie milango ya toba, ee Bwana...", " Uniongoze njia ni ya wokovu, ee Mzazi-Mungu...", na "Nikikumbuka wingi wa matendo yangu mabaya mimi mwenye zambi...". Hii siku ya Mungu magaribi tunaimba Ibada ya Magaribi ya Kutubu.

3. Kizila. Kila mwaminifu, katika nguvu yake ataangalia kufunga na chakula lakini kabisa atafanya kifungo ya zoezo mabaya na zambi mbaya. Paka vile atapata endeleo ya kiroho. Kuliko nzuri ni waaminifu kumuuliza mpadri ya roho yao ya kila tendo ya uzima ya kiroho.

4. Waaminifu hii wakati inapaswa kusoma Vitabu ya Mungu na kabisa Mandiko Takatifu.

5. Huruma. Nikusema, katika fundisho ya Biblia, kila mwaminifu inapaswa kuleta kanisani juu ya malazimisho na mateso ya maskini 1/10 ya mushahara yao ya kila mwezi. Kama kwa mufano wanachukua kila mwezi 1000 franga, watafanya wema ao wataleta makuta kanisani pa mikono ya wapadri ma franga 100.

6. Hurumia. Kila mwaminifu hii wakati haipaswe kuwa na mabishano na machukizo na watu weingine. Inapaswa kuhurumia wa ndugu wake. Hata, kama wandugu weingine wanamuchukia, huyu atapata namna na wakati juu ya kuonyesha upendo na hurumia yake mbele yao.

7. Toba. Nikusema kila Mukristu inapaswa kusikia zambi zake, kukata mapenzi ya majivuno yake na kisha atatafuta mpadri ya roho juu ya kusema zambi zake. Kila magumu yake haipaswe yeye kutafuta namna ya kuimaliza, lakini inapaswa kuuliza mpadri ya roho yake. Vile atatimiza kila tendo yake katika mapenzi ya Mungu. Mbele ya kila mambo, sikitiko ao ulizo yake inapaswa kumukuta mpadri ya roho yake. Atamuuliza na atachukua jibu na baraka yake ya kila kazi yake.

Kabisa Mwaminifu moja ma siku haya ya Kwarezima haipaswe kuangalia namna gani atafanya mikate ao chakula mazuri, lakini atafanya nguvu juu ya kuishi katika uzima ya kiroho. Atawaza matendo makubwa ya kila siku, ya kila siku ya Mungu na katika akili yake atakuja karibu ya matendo haya ya Bwana Yesu Kristu. Watu ya hii dunia wanataka kusikia siku Kuu ya kuzaliwa Kristu paka, kama watakula nyama mengi, kama watakunywa vinywaji mengi na kama watacheza na watafurahi katika kimwili. Lakini Waaminifu wa kweli wanafanya nguvu ya kuishi kila siku matendo makubwa katika neema ya Mungu na wanafurahi na hivi wanachukua neema ya Mungu na ulinzi ya warafiki Yake, nikusema ya Watakatifu Wake.

## FUNDISHO JUU YA WAFU

Kama tunaishi ndani ya giza ya zambi na ma zoezo mabaya yetu hatusikie ya kama ni uzima ingine, uzima ya milele. Kama tutaanza kukombana kwa kutosha katika Fumbo ya Maungamo na Neema ya Roho Mtakatifu zambi zetu tunaondoka inje toka hii kifungo ya ngiza ya zambi na tunaanza kuangalia nuru kimungu ya Kristu. Kwa hii Nuru ya Mungu tunaanza kusikia uzima ya milele.

Juu ya kusikia sisi ya kama ni uzima ya milele, tutawaza hivi. Tunalaria ya kupumuzika pa kitanda yetu. Kwa musingisi yetu tunaona ma ndoto ya furaha ao ya sikitiko. Mwili yetu ni pa kitanda bila kujitenga, lakini nafsi yetu hailale, kwani inaona, inasikilika. Nikusema kila mutu, hata kama analala, anaangalia ya kama eko na na uzima ingine, bila mwili yake!

Vile karibu inaonekana na mbele ya lufu. Pale tutaona na tutasikia paka na masikio na ma macho ingine. Ni macho na masiko ya nafsi yetu. Mwili yetu italala pa kaburi yetu, lakini nafsi yetu itaishi kwa milele!

Hakuna namna kuishi mtu moja, bila kuwaza ya kama ni uzima ya milele na kwa hivi, haipaswe kusema ya kama hasiogope lufu ao hakuna lufu mu uzima yake. katika sauti ya Mtume Paulo: "Na sawasawa watu wanavyowekwa kufa mara moja, na nyuma ya kufa hukumu" (Waebrania 9,27). Ya kama sisi tutakufa, hakuna shaka, japo sisi tunakataa ya kuikumbuka, lakini jambo ya matata ni kisha, nikusema itafwata hukumu. Nikusema tutajibu mbele ya Mungu juu ya matendo yetu yote. Na, kama mtu moja anajua ya kama siku moja inapaswa kupatia jibu ya uzima yake, anaanja kutayarishwa...

Mutu wa akili ni huyu anayepata akili na anajua ya kama ni mwisho ya hii uzima na anakamata mpango juu ya kusimamisha kila zambi na zoezo mbaya yake (Mtakatifu Isaaka wa Syria).

Kanisa yetu inasali juu ya wenye uzima na juu ya wenye waliisha kufa na hivi inaonyesha upendo yake mbele ya watu wote, wale wanayoishi na wale waliisha kufa katika mwili. Ma nafsi ya hawa watu waliisha kufa wanapata faida kubwa kama tunasali na tunakumbuka ma jina yao ndani ya

Liturgia Kimungu. Hata na hawa watu waliisha kufa bila kutubu, wanapata furaha kidogo, ile wakati Kanisa inasali juu ya pumuziko ya ma nafsi yao. (mt.Yoane Krisostomo). Imani ya Kanisa yetu ni ya kama ma sala ya wenye muzima na wema wao yanasaidia ma nafsi ya hawa waliisha kufa (Mt. Yoane Damaskinos). Mt. Yoane Krisostomo anasema ya kama ma nafsi ya wale wa ndugu waliisha kuingia ndani ya gehena, hakuna namna ya kuingia inje kwa ajili ya sala na wema ya wa ndugu wao wenye uzima, lakini wanapata saidio na furaha kubwa pale weko ndani ya gehena yao.

Mu uzima ingie ya milele, hakuna toba, lakini Mungu Mwema anakubali ma sala ya wenye haki na wema wao juu ya pumuziko ya nafsi ya wa ndugu wao.

Kama mtu moja anajaribu katika Maungamo, Takatifu Komonyo, somo ya Vitabu ya kiroho lakini hasikuweze kufika pa fasi moja ya utakaso na alikufa, huyu mtu Mungu Muhukumu wa haki hakuna namna ya kumusahau. Lakini kama mtu moja anaishi bila woga ya Mungu, anafanya zambi zote mpaka mwisho ya uzima yake, hasisadiki hukumu ya dunia nzima, huyu mtu hata Mungu hata wa ndugu wake hakuna namna ya kumusaidia, kwa sababu huyu wa pekee alihukumu nafsi yake kwa milele.

Sisi tunamuomba Mungu juu ya kuweka wa ndugu wetu wenye waliisha kufa pa fasi ya mwangaza, pa fasi ya baridi, pa fasi ya furaha, pahali hakuna uchungu, taabu na ombolezo...lakini hatujue Mungu wetu atafanya nini...Sisi tunasimama mbele ya Mungu sawa wasimamizi ya wafu, wandugu wetu, kwa sababu wafu hawaweze kusaidia maugu na ma nafsi yao. Kama sisi tuko watu watakatifu, sala yetu anaisikia Mungu na anapatia pumuziko kwa huyu ndugu wetu fulani. Kama huyu mufu ni mtu mwenye haki, kwa ajili ya sala yetu, anapata furaha na pumuziko kupita mnene ndani ya paradizo.

Hawa wandugu wetu wenye waliisha kufa tunawakubusha na tunawasaidia kwa sala na huruma.

Mufano kimoja: Muzee mutawa Zakharias alisali juu ya wazazi wake, kisha lufu yao na kabisa juu ya baba yake, kwani huyu alikuwa mu uzima yake mulevi na alitukana watu. Wakati huyu muzee alikuwa baba mkubwa ya monasteri yake, alizungumuza na shetani moja. Alimuuliza:

-Muko na Wakristiani wingi ndani ya gehena?

-Ndivyo, alimujibu shetani. Na baba yako alikuwa kule ndani, lakini weye ulimutosha kwa wema na huruma ile ulipatia kwa wamaskini na nafsi yake ilitoka inje kwa ajili ya saidio yako.

-Na mama yangu eko wapi?

-Na mama yako hahikukuwe kule. Hatukumuona, japo tulimutafuta...

**1. Kwa sala.**

Tunaweza kusaidia wa ndugu wetu wenye kufa hivi:

Kwa sala yetu kila siku, asubuyi na magaribi, sawa vile tunafanya na kwa hawa wa ndugu weko muzima. Tutasali hivi: "Bwana Yesu Kristu, Mwana wa Mungu pumu-zisha mutumishi wako (jina lake). Na hii sala tunaisema mare mengi katika mapenzi wetu. Na Mungu "atatimiza hamu yao wanamwogopa; atasikia kilio chao na kuwaokoa" (Zaburi 145,19). Kabisa Mungu anasikia sala yetu kama inatokea toka midomo masafi na, kama uzima yetu ni katika mapenzi ya Mungu. Hivi Mungu kwa ajili ya Mukristu moja mtakatifu, anasaidia na ndugu wake...

Ndani ya kitabu na uzima ya Mtakatifu Shahidi Thekla tunasoma hii tangazo: Mwanamuke moja mujane (balaka muke) alikuwa na binti moja, jina lake Falkonila, mupagano aliyekufa na aliingia ndani ya gehena! Huyu binti yake Falkonila alikuja kwa mapenzi ya Mungu, kwa ndoto ya mama mwake na alimwambia: "Ee Mama wangu, penda huyu mugeni Thekla na umuchunge kwako sawa mimi, kwa sababu huyu ni mutumishi wa Mungu na anaweza kusali juu Mungu niweke mimi pa fasi ya hawa wenye haki". Na kweli, kwa ajili ya sala ya Mt. Thekla, huyu binti Falkonila alienda toka gehena ndani ya Paradizo!! (Tafuta uzima ya Mt. Thekla ya mwezi ya 24 ya Septemba).

Mtakatifu Serafim toka muji ya Sarofi ya Rusia anatuelejea: "Walikufa wa dada wa wili, wenye walikuwa zamani na wa mama wakubwa ya monasteri yao. Bwana Yesu alinitangaza ya kama ma nafsi yao, wakati walipita katikati ya majeshi ya ma shetani, walipata magumu mengi. Nilisali na mimi ma siku na ma usiku tatu na nilimuomba Mzazi-Mungu juu ya wokovu wao. Ku mwisho wema ya Bwana Yesu, kwa ajili ya maombi ya Mzazi Mwake, iliwasaidia. Walipita ma nafsi yao majeshi ya mashetani na walichukua maondoleo ya zambi zao. Uwaza! Japo Mungu aliweza kuwaokoa huyu wa pekee, lakini alimutangazo hii jambo yao kwa Mt. Serafim juu ya kupata tangazo na watu weingine

na kusali Mt. Serafim siku na ma usiku tatu! Sasa uwaza mara ngapi na sisi tunapaswa kusali na kuishi uzima safi juu ya kusikia na Mungu sala yetu!

**2. Kwa Prosforo.**

Mwaminifu moja, tangu sala ya Magaribi ya siku ya Sita (Muposho) atapeleka mukate Prosforo kanisani juu padri kesho atatosha Mwili ya Kristu afanye Liturgia Kimungu. Ile wakati padiri anafanya Matayarisho (Proskomidi) ya Liturgia Kimungu anakumbuka na ma jina ya wafu na wenye muzima. Hii ukubusho inaleta saidio na faida kubwa kwa hawa watu padri anawakumbuka. Tazama mufano moja:

Jemadari moja mkubwa ku mwaka 1984 alianza kufata kuliko nzuri Kanisa ya Kristu, wakati alisoma hii fundisho. Kila mu Posho alipeleka Kanisani mukate (prosforo) moja juu ya pumuziko ya baba yake, aliyeisha kufa. Kisha wakati kidogo alikuja baba yake kwa musingishi ya mama yake na alimwambia: "Ananifurahisha nyingi huyu bwana A...kwa sababu ananitumia hii zawadi (prosforo). Alimwambia hii sauti ya baba yake huyu mama kwa mtoto mwake na yeye aliende kuuliza mpadri ya roho yake. Huyu mpadri alimujibu: "Hii Prosforo (mukate), mtoto wangu, unaileta kanisani. Katika namna ya kiroho inapanda mbinguni, ile wakati mimi ninakumbuka jina lake kama ninatayarisha Proskomidi. Hii Prosforo inafurahisha na inapumuzisha nafsi ya baba yako".

3. Kama tunafanya Koliva. Koliva ni bego ya ngano ao kapombo ya mikate, yenye tunapeleka kanisani juu ya kupumuzisha Mungu ma nafsi ya wa ndugu wetu. Makumbusho ya wafu tunafanya kila mu Posho asubuyi. Saidio juu ya nafsi ya wafu ni mnene, sawa inaonekana hii jambo mu uzima ya mpadri aliyeisha kufa jina lake Dimitrios Gagastathis. Tazama inaandikwa nini mu kitabu yake: "Ku mwaka 1946 waliniambia ya kama ndani ya bonde moja, karibu ya mukini Liopraso, ni mifupa ya wafu wa ine, wenye waliwaua na mashashi wa adui ya Kristu ku mwaka 1944. Nilikamata mpango juu ya kuyapeleka ndani ya ile fasi ni na mifupa ya Wafu weingine, karibu ya kanisa yetu. Wakati tulifika pa hile fasi yalikuwa mifupa yao, tulisikia malalamiko na maombolezo yao, sawa walifanya ile siku ya mateso na kifo yao. Kundi ya wa ndugu wangu, wenye walikuja karibu yangu, walianza kuogopa. Niliwashauria kuwa na ukimya na niliwaambia: "Mwangalieni dini yetu ni kabisa muzima ya ajabu". Tangu ile dakika nilianza kusali na kusema: "Mungu Mutakatifu...", malalamiko yao yalisimama. Waliongojea kusikia ma sala ya hurumia ya zambi zao!!! Kila sala ya pumuziko na usamehe yao ni ya kweli. Ni ulazimisho ya kufanyikwa mu Kanisa yetu! Watakatifu wetu wenye waliingisha hii mafundisho mu Kanisa yetu walikuwa ya kweli wenye akili na watakatifu"!

Ni kweli kusema ya kama Kanisa yetu inasali juu ya waaminifu wake, wenye wakati waliishi, walikuwa na unganisho katika kiroho pamoja naye. Nikusema, Kanisa yetu haifanye sala kwa wapagano ao kwa wakosefu ya imani ao kwa wale walisimamisha uzima yao kwa mapenzi yao.

Makumbusho ya wafu hatufanye ma siku Kuu ya Bwana Yesu Kristu, ma Siku Kuu ya Mzazi Mwake na kutoka mu Posho ya Lazaro mpaka siku ya Mungu (ya Mtume Thomas), nikusema juma moja kisha juma ya Ufufuo ya Kristu.

4. Kama tunakumbuka ma jina yao ndani ya Liturgia makumi ine (40). Nikusema tunafanya Liturgia Kimungu kila siku ya ma siku (40) na tunakumbuka ma jina ya wa ndugu wetu, wenye waliisha kufa. Kundi ya ma Liturgia makumi ine inasaidia nafsi ya wa ndugu wafu wetu.

5. Kama tunafanya Liturgia, pahali na sisi wenye muzima tunatayarishwa na tunakomunyika. Mara moja na wafu, wa ndugu wetu, wanakomunyika katika namna ya kiroho, ile anajua Yesu Kristu. Kwa hivi makumbusho kisha ma siku tatu, ma siku Tisa, ma siku Makumi ine, kisha mwezi tatu, kisha miezi sita na kisha mwaka moja, ao kisha miaka tatu tunapaswa kuifanya ndani ya Liturgia Kimungu.

**Saidio kwa wema na huruma.**

Wema ni saidio ile tunatoa sisi kwa watu wamaskini, makuta ao vitu vya uzima yao. Kufwatana na Mandiko Takatifu, Kanisa ya Kristu katika Watakatifu Wpadri wetu, alitengeneza hii saidio hivi: Kila Mukristu inapaswa kupatia kwa Mungu, nikusema kwa watu wamaskini,watoto yatima, kwa Utume ya Kanisa, kwa saidio ya mateso ya watu weingine makuta 1/10 toka mushahara yake. Mtakatifu Yoane Krisostomo anatueleja hivi: "Twende ya kutoa na sisi wema na matoleo ya saidio kwa pumuziko ya wale waliisha kuondoka. Hivi tutawasaidia ya kupata fasi kupita nzuri mu uzima ya milele". Tena alisema: "Weka kwa uriti yako, hapana paka watoto wako, lakini na Rabi Yesu Kristu.

Andika na Jina Lake juu watoto wako watafanya makubusho na wema juu ya pumuziko yako. Usisahau kusaidia wa maskini".

Tena na Mtakatifu Grigorio wa Dialogos anaandika hivi: "Musizanie ya kama vitu haya mtu moja anatoa katika imani kwa Mungu hailete mu nyuma yake malipo nyingi! Anapata saidio na ule mutu anatoa hii wema na ule mtu aliisha kufa na anaongojea saidio ya wale wa ndugu weko ndani ya uzima. Mufano moja: Ule mutu anayemimiya na marasi mtu mwingine, ku mwanzo atapakaliwa huyu wa pekee na kisha atamupakaa na mutu mwingine ndugu yake. Na vile, huyu anayekwenda na haraka juu ya kusaidia wokovu ya ndugu yake, ku mwanzo anasaidia maungu yake na kisha anasaidia na ndugu yake. Mungu si eko musiye na uhaki, kwani hasiogope tendo moja inayefanyika kwa saidio ya ndugu mwingine.

Nguvu ya sala, ya kifungu ya kula na kabisa nguvu ya huruma inaonekana safi kwa hii mufano inafwata:

Mama moja aliyekuwa na uso muzuri sana alibaki mujane tangu kipimo ujana yake pamoja na mtoto moja mudogo. Juu ya maisha yake alichagua uzima ya raisi, bila muchoko nyingi, alifata uzima ya zambi ya kimwili na alipata hivi mali na makuta mengi. Wakati mtoto mwake alikomea, alikufa mama yake na mali yake ilibaki pa mikono ya mtoto mwake. Wakati huyu kijana alisikia bure ya hii uzima na faida ya bure ya utajiri ya mama yake, kwani na mama yake alikufa bila kubeba kitu pamoja naye, alibadilisha mali yake kwa wamaskini, kwa kanisa ya Kristu, ma shamba yake pa mikono ya wamaskini juu ya pumuziko ya ma nafsi ya wazazi wake na kabisa juu ya mama yake na alienda jangwani kusali pamoja na watawa weingine. Pamoja ilizaliwa ndani yake na hii ulizo: Mungu alikubali huruma na wema yake na alisikia na ma sala yake ao hapana? Alianza kuuliza na watawa juu ya kupata jibu.

Alienda mujini Yerusalema juu ya kupata jibu. Patriarchi alimutumia kwa watawa ya jangwa ya fasi Thivaida. Kisha na wale walimutumia kupita ndani ya jangwa. Kisha mwendo yake ya ma siku makumi tatu (30) alisimama mbele ya pango moja pahali alitoka inje mutawa moja muzee, mtakatifu. Alimuelejea ulizo na jambo yake na ule Muzee alimujibu na unyenyekevu nyingi:

-Mtoto wangu, hii tendo uliyeniomba ni kubwa sana. Lakini kwa muchoko uliyefanya kuja mpaka hapa, tutaomba pamoja mbele ya Mungu juu ya kupata jibu ya ulizo yako na kupata ujulisho ilikwenda wapi nafsi ya mama yako.

Alitoka huyu mumoja inje na bakora yake alifanya muviringo moja chini ya inchi na aliniambia:

-Hapa ndani ya hii muviringo utasimama weye ma siku saba na usiku. Usitakule hata kitu kimoja, wala utaikaa na utaomba Mungu na machozi. Hii kazi umoja nitafanya na mimi ndani ya pango-chumba yangu na Bwana Mungu Mwema atafanya mapenzi yake.

Wakati ilifika usiku ya saba, akili yangu ilipanda mbinguni na niliona mu fasi ya kushoto kiziwa moja mnene ya kujaza machafu, matope ya uchafu na arufu mbaya. Ndani ya hii kiziwa niliona vichwa, mikono na miguu na waliyepanda na walishuka, sawa vile inafanya maji, wakati inapikwa. Wakati hii uchafu ya kiziwa inapikwa na ilipanda na ilishusha, mara moja niliona na mama yangu, mwenye alinifamia na alianza kuniita na malalamiko:

-Mtoto wangu, mtoto mupendwa wangu, unisaidie na uniokoe. Na, wakati alisema hii sauti yake, hii matope ya uchafu ilimuzibiliya mara moja. Mara ya mbili ilimupandisha matope ya uchafu mpaka kilari (kifuo) yake na huyu mama yangu alipata saa kuniomba mara ingine: «Mtoto mupendwa wangu, unisaidie! . . . na hii matope uchafu ilimupandisha mara ya tatu na huyu aliniambia: «Uniwema mtoto wangu, usiniache ndani ya hii uchafu na mateso ya gehena ya milele».

Ile saa mimi, kwani nilikuwa na umivu mingi juu ya mateso ya mama yangu, nilifungua mkono yangu na nilimukamata na ku nywele yake. Wakati huyu alikwenda kujilobeka mara ingine, nililobeka na mimi mukono yangu ndani ya uchafu na nguvu mingi nilimutosha inje ya ile kiziwa. Ile saa niliona ma fasi ya kuume yangu sahani moja mnene, pahali ilikuwa maji safi. Nilimunawisha ndani na nilimuweka kusimama katikati ya vijana wenye kuvaa manguo meupe, na wenye walisimama pempeni yangu.

Mama yangu alishukuru na machozi mengi Bwana Mutukufu na alibusu na heshima wale wa malaika wenye mwangaza. Tena alishukuru na mimi. Asubui, wakati ilikuja mchana, alikuja mutawa wa jangwa na aliniuliza:

-Ee ndugu, hii usiku uliona ono moja kwa sala yako?
-Padri mtakatifu, niliona ono moja ya ajabu kabisa na misitaweze kuisahau mu uzima yangu yote.

Nilimwambia yoyote matendo ile niliona. Ile saa yule alinikikiri ya kama aliona na huyu hii ono umoja na alimushukuru Mungu na Mwokozi wetu na machozi mengi kwa ajili ya wema nyingi Yake, kwani aliacha kutoka nafsi moja toka gehena mu Paradizo. Mukono yangu, lakini, ile niliweka ndani na ile kiziwa juu ya kukokota mama yangu, ilichunga hii harufu mbaya na nilimuuliza mpadri:

-Mpadri mweshimiwa, ninakuomba nguvu, fanya sala kwa Mungu juu ya kufukuza hii harufu kibaya inatokea ku mukono yangu. Na yule aliniambia:
-Usisikitike juu ya hii mambo, mtoto wangu. Vile Mungu alipenda imbakie hii alama bila kutoka juu ya kusadiki na wenye wanakataa Mungu, wavivu na wazaifu watu, kwani hawa wanashaka ya kama ni mateso ya gehena na bintu mazuri mu paradizo.

-Iko vile, mpadri mweshimiwa, lakini misiweze kuvumilia hii harufu kibaya, wala watu wenye wananikaribia hawaweze kuvumilia. Ile saa huyu mpadri mtakatifu alikata kipande moja ya nguo meushi yake, alifunga mukono yangu na aliniambia ya kama itambakia vile mpaka mwisho ya uzima yangu.

Ee ndugu, kwa sababu ulichoka kukuja mpaka hapa, nitaomba kwa Mungu juu ya kusaidiaya kurudia nzuri. Na, wakati alisema hivi, ilipuliza pepo nguvu na mawingu moja ilifika karibu yake na alimwambia:

Kwa jina ya Bwana wetu Yesu Kristu, kamata huyu ndugu na utamupeleka mu makao yake na kule atatangaza kwa watu wengine tendo ya ajabu ya Mungu na rehema yake kubwa.

Wakati aliisha hii sauti yake huyu mpadri, mawingu moja ilinichukua, ilininyanyua pa pepo na, sawa vile ilipeleka Mitume mu shamba ya Getesimani juu ya Kiliyio ya Mzazi-Mungu, vile alileta na mimi inje ya nyumba yangu, iliyekuwa karibu ya Konstantinopoli.

Hii, askofu Mtakatifu, ilikuwa historia ya mukono yangu na sababu gani nilimufunga na hii nguo ya mpadri yule ya jangwa.

## Juu ya nini Kanisa yetu inafanya makumbusho kisha ma siku Tatu, Tisa na makumi inne?

Siku moja Mtakatifu Mutawa Makarios alitembea mu jangwa. Malaika wa Mungu alikuja akimufwata nyuma yake, akamwambia: «Himidi, Padri Mtakatifu.»

Padri Makarios aliwaza ya kama ule mutu anaweza kuwa Mutawa wa jangwa, akimujibu : «Mungu akusamehe, mutoto yangu.»

Walitembea pamoja na Padri Makarios aliona uso ya ule kijana Mutawa, ilikuwa mzuri sana kupita, alishangaa na alimuuliza:
« Mutoto yangu, ninapokuona ninashangaa juu ya nini uso wako ni wa ajabu na inangaa sana? Sijaona hata mara moja uso ya watu wengine sawa hii yako. Naapa kwa Mungu wa mbinguni nataka uniambie kweli.»

Basi Malaika alipita magoti mbele ya Padri Makarios na akamwambia :
«Himidi, ewe Padri, Mimi sawa unaniona, niko Malaika wa Mungu na nilikuja ku kufundisha ile Mafumbo (Mystere) haujui na unapenda kufunza. Padri naye akapiga na magoti mbele ya Malaika na akamwambia :
Ewe Bwana, nakushukuru, kwa sababu ulinitumia Muongozi wa kunifundisha Mafundisho yote yale mimi sijue na yale Mafumbo ninatamainia kusikia.

Malaika akamujibu mara ingine: «unaniambia mimi unataka kufunza nini ?
-Padri alimujibu:
Ewe Malaika, uniambie juu ya nini mu Kanisa yetu tunafanya makumbusho ya wafu kisha ma siku Tatu, Tisa na makumi inne?
Malaika alimujibu hivi :

Sikia ewe, Padri Mtakatifu. Ile siku ya tatu kisha lufu ya mutu mmoja. Kanisa Orthodoksi inafanya makumbusho, kwani, sawa tulisema, ile roho haijaenda bado kwa Bwana Yesu.

Kanisa inafanya sala na inamuombe Mungu apokee na Mapendo mingi ile roho itafika ile siku ya tatu kubusu mukono kwa kupokea baraka yake.

Kisha kubusu Malaika Watapeleka ile nafsi (roho) ku dunia, ku ile fasi aliishi, kule wataanza kumuonyesha mafasi yake alitembea, na zambi zake alitenda. Nikusema watamuonyesha hivi: «Hapa, ee Nafsi (roho) uliiba vitu fulani, kule ulizini, hapa ulihukumu mutu fulani, hapa ulisema uwongo kule ulilewa, hapa ulifanya makelele, kule ulifanya machukizo» na zingine zambi.

Kisha Malaika wataanza kumukumbusha yale matendo yake mema. Kwa mufano: «Hapa ulisaidia, kule ulifunga, hapa ulitubu, kule ulisharikia Liturgia ulifanya sala kwa Mzazi-Mungu. Sala ya usiku muzima,» na ingine. Kwa hivi hii matezamio wataifanya mupaka siku ya tisa. Ile siku ya tisa watarudi mara ingine mu mbinguni juu roho kubusu Bwana Yesu Kristu mara ya pili ..

Hapa waaminifu ya kanisa watafanya sala ya makumbusho juu Mungu apokee na huruma na macho yake ya Mapendo ya ile roho. Ndio vile iko mandiko ya Kanisa yetu ya kama ile waka ya makumbusho inaleta faida ku roho. Tena inasaidia Matendo ya huruma na kufanya Ibada Takatifu (Litrugia).

Kisha kubusu mara ya pili Malaika wataleta mara ingine ile roho ku ile fasi ya Paradiso. Kule wataionyesha kutazama Paradizo, iliyo fasi ya huruma ya Mungu, fasi ya Abrahamu, tena fasi ya watu wenye haki. Na wakati itaona ile furaha pasipo kusema, itafurahi itasihiina itaomba kwa Malaika ikae mule pamoja na watu wenye haki.

Kisha Malaika Watapeleka ile nafsi (roho) ku Gehena? Kule nafsi itaona namna wanateswa wale watu wenye zambi. Malaika wataionyesha hivi: «Tazama, hii ni muto ya moto, huyu ni kidudu wasipo kulala, hii ni giza ya inja na ya ndani, kule kunakaa wale watu wenye kusoga memo yao juu ya mateso mengi. Hivi polepole nafsi (roho) itaona mateso yote ya wenye zambi.

Padri wangu, alivyosema Malaika, hakuna mateso ya nguvu kupita mateso ingine sawa ile mateso ya musharati (kahaba ) na ya mnyanganyi. Kabisa- kabisa mateso itakuwa mingi kwa ule mutawa, mwanaume ao mwanamuke alizini, na ile mateso wataipata. Padri na bibi yake, kama walizini pasipo kutubu.

Kama itaisha hii safari, nafsi (roho) Malaika Wataipeleka nafsi (roho) mara ingine siku ya makumi ine (40 jours) mu mbinguni kubusu Bwana Yesu Kristu mara ya tatu. Basi waaminifu wanafanya sala ya makumbusho juu ya kumuomba Mungu akumbuke katika mapendo na huruma yake ile nafsi. Ile siku ya makumi ine iko siku ya hukumu, siku ya mwisho. Nikusema tangu ile siku nafsi (roho) itaenda ku ile fasi anataka Mungu Mpenda wanadamu kadiri ya matendo yake mtu alitenda mu dunia. Ni hivi ile nafsi (roho) itakaa mu fasi yake ya milele. Ni kule itabakia mupaka ile siku ya ufufuo wa mwili wake wakati atakapokuja mara ya pili Bwana Yesu Kristu. Kisha Ufufuo wa mwili wetu, nafsi (roho) itaungana na mwili na watasikia ao furaha, kama weko mu Paradizo, ao sakitiko na mateso mingi, kama wataenda mu Gehena.

Halafu, Mtakatifu Makarios, alilia na alitosha machozi mengi na akasema : Ole kwa ile siku alizaliwa ule mutu !.

Malaika alimujibu: Ndivyo, Padri mtukufu, hii mambo ni kweli paka kwa wote watu walitenda zambi, pasipo kutubu. Lakini kwa ule mutu mwenye haki sisi inapaswa kusema hivi : «Heri ile siku na saa, ule mutu alizaliwa».

Padri aliuliza Malaika mara ingine.

Ninakuomba kunionyesha tena na hii kitu: ule mutu mwenye zambi atakufa na ataenda mu gehena atakuwa na furaha ao mateso yake haitaisha?

Malaika alijibu hivi :

Hapana, ewe Padri Mtakatifu, hata ufalme wa wenye haki uko na mwisho, hata gehena ya wenye zambi iko na mwisho. Mufano, kama mutu mmoja atabeba mu bahari fungu ya mchanga mara moja katika miaka elfu (1000) kuipeleka fasi ingine itafika wakati moja atatamainia kubeba mchanga yote. Lakini wakati ya gehena na ya watu wenye zambi haitaisha hata kidogo. Vivyo hivyo na wakati ya Paradizo na ya wale watu wataingiamo haitaisha hata mara moja.

Padri aliuliza Malaika mara ingine- Ninakuomba uniambia na hii kitu, ewe Malaika wa Mungu: Watakatifu wake na huruma mingi kwa watu wote, juu ya kujua kama kile anaweza kuwa na Mapendo ya kumuomba msaada wao katika maisha yake?

Malaika alimujibu hivi;

Watakatifu wote wanawapenda watu wote na wanataka kuwasaidia. Lakini ninyi watu muko wabaya, watakatifu wanasikitika kwa ajili ya zambi zenu. Na wanasirika kwa sababu ninyi Munakataa

kuwapigia «Aksanti», Kuwashukuru. Na Malaika Watakatifu weko na huruma mingi kwa watu wote, kwa sababu na wao waliona yale matendo ya ajabu alitenda Mungu juu ya wokovu wa wanadamu. Tena Malkia Mzazi- Mungu Mama Maria anasaidia sana kizazi ya Wanadamu.

Ilipaswa, Padri Mtakatifu, kila mutu kuchunga kinywani mwake jina la Mama Maria kwa kumuomba na kumutukuza. Lakini shetani alimudanganya na aliharibisha akili yake juu ya kusahau Jina na mapendo yake.

Leo, kama anaishi duniani, anaishi juu ya mapendo na sala ya Mama Maria kwa Mungu. Kwa sababu watu walizarau Mungu na Watakatifu Wetu.

Padri Makarios aliuliza Malaika mara ingine : Uniambie, Malaika Mtakatifu, katikati ya zambi zote ni zambi gani iliyo kubwa zaidi ?

Malaika alimujibu : Kila zambi, ewe Padri Msifiwa, inatenganisha mutu kwa Mungu. Lakini chuki na matusi ni yulu ya zambi zote. Kwa sababu paka hii mbili zinaweza kuangusha mutu chini ya Hadeze.

Na tena Padri alimuuliza: Zambi gani Mungu anachukia kupita zambi zingine?

Malaika alimujibu: Majivuno. Ni paka hii zambi iliharibu dunia nzima. Kwa ajili ya hii Adamu aliyeumbwa wa kwanza alipoteza Paradizo. Kwa ajili hii Mkubwa wa kundi la Malaika wa Kwanza, alipoteza baraka na neema ya Mungu na kisha aligeuzwa akawa Malaika wa shetani. Kwa ajili ya hii Mufarisayo alipoteza uwezo wake kwa Mungu. Kama mutu atanguka kwa hii zambi ni nguvu sna kutubu na kuamuka.

Mara ingine Padri alimuuliza : Watu gani wanateswa. Mu gehena kuliko wengine ?

Malaika alimujibu hivi : Ninakuonyesha ni musharati na mwenye kuchambulana. Lakini nakuambia tena ya kama katika gehena ni fasi moja ya matata na yasipo rehema ya Mungu. Maana yake ni fasi yasipo kuonekana. Kule wanalipizwa na mateso mengi wale Mapadri, watawa wanaume na wanawake walizini pasipo kutubu mbele ya kufa kwao.

Ile kundi ya kwanza ya Malaika ilianguka ndio sasa kundi ya mashetani. Mapadri na Watawa waliishi hapa duniani muzuri wataokolewa na sifa yao itakuwa kubwa sana.

Halafu, Watawa Wabaya na wenye kuvunja amri Mungu atawatuma bila sifa, ku fasi, ya malipizi. Tena, kama Mapadri sababu ya uzaifu wao, wanaacha kufanya sala yao ya kila siku (asubui, manparibi, usiku) ao Liturgia ya siku ya Mungu na ya Watakatifu wetu nao pia watalipizwa sana kwa Mungu. Lakini nitasema nini juu ya Mapadri walevi? Ole wao kwa sababu malipizi ya ngubu kabisa inawaongojea.

Basi Padri Makarios aliuliza tena Malaika:

Nakuomba unionyeshe hii mambo: Wale watu wanazarau siku ya Mungu watakuwa na faida na furaha hata kidogo kule mbinguni ?

Malaika alimujibu hivi: Ole wao, ewe Padri mukubwa, kwa sababu malipizi ya nguvu inawaongojea. Ule mutu anazarau ile siku ya Mungu, anazarau Bwana Yesu Kristu na Yesu atamuzarau kwa sababu siku ya yenga ni siku ya Bwana Yesu.

Ule mutu anasifu siku ya yenga, anasifu Bwana Yesu Kristu. Ule mutu makumbusho ya Watakatifu na anashangilia siku za Makumbusho yao, Watakatifu watamusaidi, kwa sababu weko na uwezo kubwa kwa Mungu na wakimuomba kila kitu, Bwana Yesu atawapatia. Lakini watu walifukuza woga wa Mungu rohoni mwao, na sasa hawana Mungu rafiki yao, ao Mtakatifu fulani akili yao na roho yao vitawatawaliwa paka kwa vitu vya bure vya hii uzima, pasipo kuwaza ya kama vitu hivi vitatoweka na vitapotea.

Sikia. Muzuri, Padri muheshimiwa, kila mutu akiwa Padri, ao Mutawa ao Laiki akikataa kusifu na kwenda ku Misa kila siku ya Mungu hataona uso wa Mungu, na hatapata matumaini ya wokovu wake.

Na sasa, Padri mtukufu, kama unataka kuniuliza kitu ingine, uniulize, kwa sababu sasa ni wakati kutoka mbinguni kwa Bwana Mungu wangu kwa kumutukuza.

Basi, Padri Makarios alilia, na alisema: Ole kwa sisi «Tazama, huyu mutumishi muzuri wa Mungu ni Malaika wasipo Mwili na zambi, na anajiharikisha kwenda kumutukuza Bwana Yesu Kristu. Lakini sisi watu wenye zambi na wa bure hatuna na hii baraka ya kumutukuza Mungu lakini tunazarau wokovu wetu.

Na tena alimuuliza ule Malaika wa Mungu:

Ninakuomba uniambie, sala gani Watawa wa waaminifu wetu wanapaswa kufanye? Ule Malaika alijibu hivi: Kama mutu mmoja ni mwenye elimu, nikusema mutu wa akili ni vizuri kusoma zaburi ya Daudi. Kama hana mutu wa elimu, anaweza kusema hivi : «Bwana Yesu Kristu, Mwana wa Mungu, unihurumie mimi mwenye zambi». Hii sala iko nguvu kabisa na teketeke kabisa, kwa hii maneno, watu wa akili mingi waliacha vitu vyote vya dunia wakaishi na uzima takatifu walitumika hii sala.

Hii sala watu wote wanaweza kuisema hata watu wa bure wasipo akili mingi kila mutu mwenye kutaka kuokolewa, ataweka kinywani mwake na mu akili yake hii sala pahali popote, mchana na usiku, njiani, kama anaikaa ao anatembea, ao anatumika, na hii sala iko na nguvu kusaidia ule mutu anataka kuokolewa.

- Na tena Padri mukubwa alimuuliza Malaika: Kwa sababu, ewe Malaika wa Mungu, ulifika kunifundisha mimi mwenye zambi nakuombe unioyeshe na hii kitu : Kama mutu mmoja eko mwenye zambi na atafundisha mutu mwingine kwa kuacha njia ya zambi na kufwata njia ya wokovu, yeye atapata malipo fulani ya roho yake ao hapana ?

Malaika alimujibu hivi: Ule mutu atafundisha mutu mwingine na kumutosha mu njia ya zambi kwa kumwonyesha njia ya Mungu, huyu aliokoa nafsi (roho) yake na nafsi ya ndugu yake mu gehena. Lakini ule mutu alishauria ndugu yake kufwata njia mubaya, atamuharibu ule ndugu yake, na nafsi yake ataitoa mikononi mwa shetani. Halafu, hakuna zambi ingine kubwa zaidi kuliko hii anatenda mutu ya kuondoa ndugu yake mu njia ya Mungu na kumupeleka mu njia ya shetani. Na hakuna kazi ingine kubwa zaidi, sana ile anafanya mutu kwa kumushauria ndugu yake kwa kufwata uzima wa roho, uzima wa Mungu ….

Kisha kusema hii maneno ule Malaika aliinamisha kichwa chake kwa Padri, akamwambia

Unihimidi, Padri Mtakatifu na unisamehe.

Basi Padri Makarios alipiga magoti yake chini, alimubusu Malaika na alimwambia:

«Wende na amani ku Utatu Mtakatifu na uniombee.

Wakati Malaika aliondoka na alipanda mbinguni, Mtakatifu Makarios alimushukuru Mungu, alienda nyumbani mwake, na kule alionyesha mazungumuzo yote kwa rafiki yake mmoja Mutawa mwingine aliyeishi pamoja naye, hivi vyote viwili vilitukuza na kuhimidi Mungu wa mwisho, Utukufu kwa Mungu.

**Matoleo- koliva**

Zawadi ingine sisi tunatoa kwa rafiki moja yetu ao jerani na zawadi ingine kwa mtu mkubwa, ya serkali ya inchi yetu. Basi, na zawadi yetu mbele ya Mungu inapaswa kuwa katika utukufu ya Mungu. Tena hali ya roho yetu inapaswa kuwa nzuri juu ya kupokelea Mungu zawadi wetu.

Mulimaji Kaina, mtoto ya Adamu, alitoa sandaka mbele ya Mungu toka kazi ya muchoko yake, lakini sandaka yake aliitoa bila heshima, upendo nja woga mbele ya Mungu. Na sandaka yake Mungu alikataa kuipokelea, tena na sala yake!

Lakini muchungaji Abeli alitoa sandaka yake na unyenyekevu, imani, saaw vile anasema Mtume Paulo (kwa Ebrania 11,4), nikusema alimutoa kwa Mungu kila zawadi alikuwa nayo katika upendo na heshima. Kwa hivi na Mungu alikubali sala yake na alimubariki.

Na sisi leo tunapaswa kufata mufano ya Abeli na hapana mufano ya ndugu yake Kaina. Kila zawadi yetu mbele ya Mungu, sawa mukate, mafuta, mishumaa na ingine inapaswa kuwa ya muzuri na katika upendo na heshima.

**Lufu katika mateso**

Mateso kwa ajili ya malari yoyote ao mafukuzo kwa watu wambaya sisi tunapaswa kuyapokelea na uvumilia sawa vile tunavumilia magumu yetu kama tunasikia maumivu ya mwili yetu.

Sisi wote tunajua mifano ya watu watakatifu, wenye waliteswa mbele ya lufu yao. Vile waliteswa na Mitume, mashahidi ya kanisa yetu, lakini na watakatifu wa sasa.

Mifano yao yanatupatia fundisho moja nzuri sana. yanatufundisha ya kama:

1. Haipaswe kusikitika ao tafuta jibu mbele ya kila mambo yetu, kama tunajua ya kama watu wetu wenye wanasadiki, lakini ku mwisho ya uzima yao wanateswa na wanavumilia, mbele ya kufa.

2. Kama na watu wenye haki wanateswa, mbele ya lufu yao, hii inafanyika juu ya kusafishwa toka ma alama hata kidogo ya ma zambi na ma zoezo yao na hivi watachukua taji ya milele. Kama na Mwana Wake wa Pekee aliteswa mbele ya kufa pa Musalaba Yake, tutasema nini sisi, kama hata na watu watakatifu wanateswa juu ya kusafishwa ma nafsi yao kwa machufu hata kidogo?

3. Mateso na magumu yote yanaonyeshwa ndani ya hii uzima ao yataponyeshw mu uzima ingine ya kama ni ma zawadi ya Mungu.

Kwa hivi lufu ya Mukristu moja katika materso haiko kitu kimoja kimbaya na sisi haipaswe kuogopa. Paka tunapaswa kumuomba kwa Mungu amupatie kwa huyu Mukristu uvumilia juu ya kunyanyua musalaba ya mateso yake bila kupotesha kitumaini yake mbele ye Mungu. Tunateswa miezi kidogo lakini kisha Mungu anatuingisha kwa Ufalme wa Mbingu wake na anatupatia vitu vitakatifu ya milele. Tena mateso haya na majaribu sisi tunapata ni katika kipimo yetu na hapana juu pia ya kipimo yetu. "Lakini Mungu ni waminifu, hasiyewaacha ninyi kujaribiwa, kuliko munavyoweza; lakini pamoja na lile jaribu atafanya njia ya kukimbia, ili muweze kuvumilia" (barua ya kwanza ya Wakorinto 10,13).

Ni kazi kimbaya kama mtu moja atakufa katika mateso ao bila mateso lakini ndani ya zambi zake, nikusema bila kutubu, bila Maungamo na bila Takatifu Komonyo.

**Lufu isiyona haki ya watu wenye haki**

Lufu isiyo na haki ni kifo ya Abeli. Kaina alimuua ndugu yake, hapana kwani alimuuzi, lakini kwa sababu Abeli alimusifu Mungu na sandaka muzuri na Mungu alimupokelea sala yake. Kaina alisirika, alimuchukia ndugu yake na ku mwisho alimuua.

Mungu alitaka kwa hii uwaji ya kumusifu kuliko nyingi Abeli na alimufanyishia taji ya utukufu yake kabisa kubwa na kujaa na mwangaza.

Iko namna Mukristu moja kuondoka ya hii uzima mara moja. Lakini kanisa inasali juu waaminifu wake hapana kuondoka katika lufu na haraka. Mpadri mkubwa Porfyrios, mtakatifu wa sasa anasema juu ya nini Mungu anaweza kubariki Mukristu moja akufe mara moja:

1. Kama mtu ni mtakatifu, nikusema anaishi uzima moja takatifu na anataka Mungu kwa sababu Yeye anajua ya kumuchukua karibu Yake juu ya kuendelesha kuishi naYe kwa milele.

2.Wakati mtu eko na matendo mazuri hapana mengi, lakini Mungu anaona ya kama huyu ataanguka kisha ma zambi ingine na atapotesha Paradizo. Kwa hivi Mungu anabariki akufe huyu mwaaminifu juu yeye kwa sala ya wa ndugu wake ataontoka ku gehena na atapata uzima ya milele Paradizoni.

3.Kama mtu moja asipende kutubu na hana na mafaa ya wokovu yake. Lufu yake ni sawa tunda ya matendo mabaya yake na Mungu anamuacha kwa sababu anajua ya kama yeye hasipende kutubu. Lakini sisi hatujue mambno gani inafanyika kwa ma nafsi ya watu hile wakati ya mwisho ya uzima yao.

## NAMNA GANI TUNATAYARISHWA KWA KUKOMUNYIKA

Sisi tuko watu wenye zambi na hatuweze kukaribia ya kupewa Mwili na Damu ya Kristu bila kutayarisha roho yetu. Kisha Ubatizo, ile tulibeba na kipimo yetu kidogo, Bwana Yesu Kristu alitupatia na Fumbo ingine kubwa. Ni Fumbo ya Maungamo na Kutubu. Kwa hii Fumbo tunapata mara ingine mapatano na Bwana wetu na hivi tunaweza kukamata Mwili na Damu Yake.

Kama tunaenda kuungama bila kutubu hii mufano yetu inaonyesha ya kama tunataka kuomba maomdoleo ya zambi, bila kusikia zambi zetu. Lakini Maungamo bila kutubu inatupatia Takatifu Komonyo moto ya nafsi yetu na hapana moto ya zambi zetu. Kama tunaenda kuungama ku mwanzo kunapaswa kuomba ponyesho ya zambi na ma zoezo mabaya yetu. Kila zambi inaacha ndani yetu alama yake pa nafsi na mwili yetu. Kama tunatubu ya kweli, tunasikia na haraka matunda ya kiroho ndani ya uzima yetu.

Mbele ya kukomunyika tunaweza kufanya hii matayarisho:

1. Matayarisho ya uzima yetu, kwa sababu tuko waaminifu wa Kristu.

2.Matayarisho siku moja mbele ya kukomunyika.

3. Matayarisho asubuyi mapema, mbele ya kwenda Kanisani ya kukomunyika.

**1. Matayarisho ya uzima yetu, kwa sababu tuko waaminifu wa Kristu.**

Bwana wetu Yesu Kristu alitueleja: "Kweli, kweli ninawaambia ninyi, kama hamukuli mwili wa Mwana wa watu, na kunywa damu yake, hamuna uzima ndani yenu. Yeye anayekula mwili wangu na kunywa damu yangu, ana uzima wa milele" (Yoane 6,53-54). Tena mu Liturgia ya Mt. Yoane Krisostomo tunasoma hii sala, mbele ya Komonyo Takatifu: "Kwako tunakutolea uzima yetu yote na kitumaini, ee Rabi Mupenda wanadamu...", lakini ndani ya Liturgia ya Mtakatifu Bazile Mkubwa tunasoma: Ee Mungu wetu, utufundisha utakaso kumaliza katika woga wako....kwa kuunganwa pamoja na Mwili takatifu na Damu ya Kristu wako...na hivi tutafanyika makao ya Roho yako Takatifu".

Sawa tuliandika juu pia, inapaswa kuwa kweli uzima ya Mukristu matayarisho moja juu ya kuchukua Komonyo Takatifu na geuzo moja ya kiroho juu ya kuwa makao ya Roho Mtakatifu. Tnagu komonyo ya kwanza mpaka Komonyo ya mbili inapaswa Mukristu moja kuishi na matakio kubwa na kuongojea hii baraka kubwa. Nikusema tunapaswsa kuangalia na kuogopa kila tendo mbaya na kila zambi kwa sababu keso keshokutu tutachukua mara ingine Komonyo Takatifu! tena kila siku tunasoma ma sala ya Komonyo Takatifu na tunachunga ndani yetu matakio ya Komonyo ya Mungu. tena tunawaza ya kama tutafanya na kila kazi ya kimwili yetu sawa vile anataka na anabariki Kristu, kwani Huyu ni pamoja na sisi kila siku.

kama tunachafuka nguo ya Ubatizo yetu na zambi moja fulani, tutatubu, tutaungama tutaomba hurumia ku hawa watu tuliwapatia sikitiko na hivi tunarudishia kwetu Neema ya Roho Mtakatifu. Kwa hivi na Mtume Paulo anatuelejea ya kama kila siktu tunapaswa kutazama roho yetu, matendo mabaya gani tulifanya na namna gani tunapaswa sasa kutenda juu ya kutubu na kutosha kila kosa na uchunga ya uzima yetu. Vile anasema: "Lakini mutu ajihukumu mwenyewe na kisha apate kula mukate na kunywa kikombe" (Kwa Wakorinto 11,28). Tena pa fasi ingie anaandika: "Kila mwenye kula mukate huu na kunywa kikombe cha Bwana, isivyostahili atakuwa amejipatia kosa juu ya mwili na damu ya Bwana" (kwa Wakorinto 11,27). Kama tunataka kupokelea wa rafiki wetu nyumbani mwetu, kwa sababu tuko na shangilio moja, kwa mufano siku ya kuzaliwa yetu, tunatayarisha nyumbani yetu mbele ya ma siku mengi. Lakini, kama sasa tunataka kumupokelea Mufalme ya Mbingu Bwana Yesu Kristu, haipaswe kutayarisha roho yetu?

Mukristu moja leo anasikia ya kama inapaswa kuchukua mara mengi Mwili na Damu ya Kristu, lakini anakataa kutayarisha roho yake ya kuungama na namna ukweli. Anakataa kufamia nzuri hali ya roho yake na kwa hivi anabaki bila ponyesho ya roho yake. Lakini Yesu Kristu anatuelejea: "Nanyi mutajua kweli, na kweli itawaweka ninyi huru" (Yoane 8,32).

Kwa hivi kama tunataka kufamia nzuri maugu yetu na ma kosa yetu yote, kutazama ma zambi zetu zote na kusikia ya kama makosa yetu ni kupita mengi ya ma fazila yetu, tunapaswa kufanya na haraka hivi:

1.Mbele ya kuungama kwa mpadri moja ya roho, tunapaswa kuwaza yoyote zambi na ma kosa yetu.

2. Hii kazi ya kutafuta kila kosa na zambi zetu ndani ya roho yetu tunapaswa kutoa wakati uhuru.

3.Mbele ya kuungama ni nzuri ya kusoma na kitabu moja juu ya kutusaidia tutaangalia nini na tutaungama namna gani.

**Matayarisho juu ya kwenda kwa Fumbo**

Watu weingine wanatubu na wanakana kuungama kwa Mpadri moja ya roho. Weingine wanaungama bila kutubu kweli. Lakini tunalazimishwa yote wa wili. Kama hatufanye hivi tunachekelea Fumbo ya Maungamo.

Maana ya neno kutubu ni ya kama ninasema ma zambi zangu na ninaomba huruma ya Mungu na tunzo ya nafsi yangu. Tena maana yake ni ya kama ninakamata mpango kugeuza akili, mawazo, namna ya tabia yangu na ninakamata mpango kuishi katika mapenzi ya Mungu.

Tunda ya toba ni ya kusikilika hali ya ma kosa ya roho yangu. Na hii hali ya makosa yangu ninaiweka mbele ya Kristu. Kama nitasikia hali ya zambi zangu, na nitaisema mbele ya mpadri, roho yangu inajaa na unyenyekevu na utii mbele ya sheria ya Mungu. Paka hivi niko stahili mbele ya Kristu na nitaweza kuchukua Komonyo Takatifu Yake.

Hii badilisho inataka upendo nyingi na baraka kubwa kutoka ya Mungu. kwa hivi na mim i ninaungama mare mengi na ninapewa Komonyo ya Kristu mara mengi juu ya kupata hapana paka maondoleo ya zambi, lakini saidio ya kiroho juu ya kuniongoza Roho Mutakatifu katika shauria ya Mpadri ya roho mu uzima ya utakaso.

Namna gani nitaangalia hali ya roho yangu juu ya kufanya maungamo moja nzuri:

**1. Zambi yangu mbele ya Mungu.**

Hamuri ya kwanza mbele ya Mungu ni hii: Upende Bwana Mungu wako kwa moyo wako yote na kwa roho yako yote na akilizako zote na kwa nguvu zako zote" (Marko 12.30) mimi ninaikanyanga mara mengi. Ninatazama ya kama misimupende Mungu kabisa na ninapenda kabisa maungu yangu na kila kitu ni yangu...

Zambi ya mbili kubwa ni hii: Misisadiki ya kama Mungu eko Baba wangu na anaangalia kila mambo ya uzima yangu. Lakini Yesu Kristu anasema: "Ninyi tafuteni kwanza ufalme wake na haki yake; na vitu hivi vyote viyaongezwa kwenu" (Matayo 6,33). Kwa mufano watu wanakataa kukomesha watoto wao na wanasema hatuna na namna ya maisha yetu...Ao wanakataa kuvumilia kila mateso ya uzima yao ao wanaikaa na shaka juu ya upendo ya Kristu mu uzima yao. Watu weko na kitumaini kupita nyingi mbele ya mkubwa moja ya Serkali, kwa maugu na nguvu yao, kwa mali na makuta yao na hapana kwa nguvu na saidio ya Yesu Kristu.

Zambi kubwa ingine ya tatu ni hii: Watu leo wanakana ao wanasahau kumushukuru Kristu juu ya ma baraka yake yote ya uzima yao. Wanakana kuwaza ma zawadi ya Mungu. Wanashukuru wa rafiki wao, wandugu wenye waliwapatia makuta ao vitu vingine, lakini wanakataa kusema shukrani moja mbele ya Yesu Kristu.

**2. Zambi mbele ya wa ndugu wetu.**

Na hapa hamuri ya Kristu: "Upende jirani yako kama wewe mwenyewe" (Marko 12,31) inanipata na mimi mukosefu. Ni kweli ya kama misipende ndugu wangu, sawa vile ninapenda maugu yangu. Ninataka watu weingine ya kunipenda, lakini hii sauti ya Kristu: "Pendeni adui zenu" (Luka 6,27) misiwaze hata kidogo! Ninapenda paka kwa neno, kwa ulimi lakini hapana kwa matendo na roho yangu. Tena ninachunga tamaa ndnai yangu na ninasahau ya kama misipende Mungu wangu ao ninachukia ndugu moja fulani.

Zambi ya mbili mbele ya ndugu wangu ni ya kama misionyesha tabia nzuri mbele yake sawa vile nilipenda na huyu kuonyesha tabia ya mufano yake mbele yangu. (matayo 7,12). Ninataka mtu mwingine ya kunipenda, lakini mimi niko muvivu na misimupende ya kweli. Hivi, ninasahau kutengeneza hali ya moyo yangu na ninatafuta kutengeneza hali ya ndugu wangu ao ninamuhukumu na ninamuchekelea.

Zambi kubwa ya tatu ni hii: Misipenda kuwa musaidizi ya watu weingine yote (Marko 9,35) na hivi ninapotea baraka ya Mungu na kisha misiweze kupata jibu mbele ya kila mambo yangu.

**3. Zambi mbele ya maugu yangu.**

Zambi tatu makubwa mbele ya maugu yangu ni haya:

Ku mwanzo, upendo ya maugu yangu. Ninapenda sana uzima na mwili na maugu yangu. Inanifurahisha kuvaa manguo mazuri kupita ya watu weingine. Kila siku ninaikaa wakati kupita nyingi mbele ya rikalasi na hapana mbele ya Picha ya Yesu Kristu na MzaziMwake Maria! Ninasadiki ya kama mimi niko kupita mkubwa katika akili na zawadi mbele ya watu weingine na ninakataa watu weingine ya kuniambia ma kosa na zambi zangu.

Zambi ya mbili ni hii: Misipende kukamata mpango juu ya kutubu na namna ukweli juu ya zambi zangu. Ninataka kuishi nzuri wakati kidogo pamoja na Yesu Kristu, lakini ma saa na siku zote ingine niko pamoja na shetani, kwa sababu ninakataa kutosha mazoezo mabaya yangu. Ninakataa kuangalia hii sauti ya Kristu: "hakuna mutu anayeweza kutumikia bwana wawili; kwa maana atachukia mumoja na kupenda mwingine" (Matayo 6,24) na ninazani ya kama nitaweza kutumikia pamoja na hawa wakubwa wa wili: Mungu na shetani pamoja.

Zambi ya tatu ni hii: Misipende kusoma kwa ajili ya uvivu yangu, vitabu vya Mungu na ya Kanisa yake. Misijue fundisho ya imani yangu na misiweze kuzungumuza na watu weingine, wakosefu ya imani...Misipende kusoma hata ya kuuliza kujifunza sheria ya imani yangu.

**2.Matayarisho siku moja mbele ya Komonyo Takatifu**

Hii siku muzima inapaswa kuwaza ya kama kesho nitaunganwa pamoja na Kristu Mungu wangu. Kabisa magaribi na usiku ninawaza namna gani nitasafisha nyumba ya roho yangu juu ya kumupokelea Mutembelesaji mkubwa wangu, Yesu Kristu.

Ninafungwa ndani ya nyumba yangu hapana juu ya kupata jibu kama niko stahili ya kukomunyika, lakini juu ya kusadiki ya kama misina stahili na hivi nitaanza kutubu ya kweli.

Ku mwanzo ninaanza kuuliza moyo yangu:

1.Ninauliza maugu yangu ninatoa nini mimi juu ya upendo yangu mbele ya Mungu na sandaka Yake pa Musalaba. Ninasadiki ya kama misina stahili ya upendo yake na inapaswa kubadilisha tabia yangu mbele Yake.

2.Ninasikia ya kama kwa ajili ya zambi zangu, ninaishi mbali ya nyumba ya Baba wangu na ninasikia kwa ajili ya hii jambo huzuni rohoni yangu.

3.Ninakamata mpango juu ya kutengeneza mapatano yangu pamoja na Mungu wangu. Inapaswa kurudia Kwake, kama kweli ninatakia Komonyo Yake kwa uponyesho ya moyo na mwili yangu.

4. Ninajaribu juu ya kusikia ya kama misina stahili akuje Bwana wangu ya kuikaa ndani ya moyo yangu, kwa sababu nyumba ya mwili yangu iliisha kuharabika na Huyu Yesu hasitaweze kupata makao ya kuikaa ndani yangu.

"Kwa hiyo ninakusujudia, na kwa uvuguo ninakulilia; sawasawa uliye-mupokea mupotevu na kahaba aliyekukaribia, pamoja unipokee nami kahaba na mupotevu, ewe mwenye huruma, na moyo wenye sikitiko, ninapokukaribia hapa sasa". (Sala ya Komonyo Takatifu).

5. Ninasikia ku mwisho ya kama sababu kubwa ni upendo katikati yangu na Mungu wnagu, kwani Huyu ku mwanzo alinipenda (barua ya Kwanza ya Yoane 4,19). Kwa hivbi ninakaribia Kikombe Kitakatifu katika woga na upende wa Kristu.

Ninaomba hurumia ku wandugu, wazazi na watu jirani weingine, kama niliwasikitisha ao nilizungumuza mbaya nao.

Ninasoma sala ya Usiku Apodipno Kidogo. Kisha ninasoma sala ya Komonyo tangu usiku, hapana juu ya kusikia ya kama niliisha kuisoma, lakini juu ya kusikia maana yake ya kama misi na stahili kukomunyika, lakini ninamuomba Mungu anistahilishe na kubali toba yangu.

Magaribi ninakula chakula kidogo bila mafuta ao matunda juu ya kulala na tumbo yangu upepeo. Misipende kuzungumuza na mambo ya nyumba ao mambo ingine ya kazi yangu. Nitaacha saa na siku ingine. Misipende kuangalia Televizio wala ma tangazo ya radio ao muchezo. Msiende inje ya kunywa ao ya kucheza, kwa sababu kisha misitaweze kupewa Mwili na Damu ya Kristu. Kama niko na wakati uhuru ninasoma kitabu ingine ao sala moja ao ninasema sala ya Kristu: "Bwana yewsu Kristu Mwana wa Mungu, unihurumie mimi mwenye zambi" na kisha ninaenda kularia ya kupumuzika.

**3. Matayarisho asubuyi mapema**

1.Ninalamuka asubuyi mapema na ninatayarishwa hapana na haraka.

2. Ninaanza kusoma sala ya asubuyi.

3.Ninasoma ma sala ya Mwisho ku Ibada ya sala ya Komonyo.

4. Ninaenda kanisani tangu mwanzo ya ibada ya asubuyi.

5. Ninaangalia na pasopo na angalisho na woga ya Mungu. Mara moja ninasali juu Mungu anistahilisha kw akuchukua Mwili na Damu Yake kwa utakaso ya nafsi na mwili yangu.

6. Wakati mpadri atasema: "Kwa woga wa Mungu, na imani..." ninakaribia na namna upole, bila kutembea bio bila kusahau ninaenda wapi.

7. Ninakamata na mikono yangu yote wa wili kitambaa nyekundu na ninaiweka chini ya ndevu yangu. Ninasema safi jina yangu na ninafungula kinywa changu.

8.Kisha Takatifu Komonyo haipaswe kuzungumuza juu hapana kuanguka Kipande kimoja kitakatifu ya Mwili ya Kristu inje ya kinywa changu.

9. Ninarudia pa fasi ya kiti changu, ninakula Antidoro (kipande ya mukate) na hii itanisaidia ya kusukuma Mwili ya Kristu ndani ya tumbo yangu.

10. Kisha Komonyo Takatifu ninaangalia hapana kuzungumuza ao ya kucheka ao kucheza, kwa sababu nitapotesha furaha ya Neema ya Takatifu Komonyo.

11. Kama nitarudia nyumbani yangu, ninasoma mara moja Shukrani ya Komonyo, na hii furaha na barka niliisha kuchukua toka Komonyo Takatifu inajaa uso na roho yangu...Ninaishi sawa vile anataka Mungu juu ya kutukuzwa Jina lake hapa duniani!

**4. Kifungo ya kula na Komonyo Takatifu**

Kifungo ya kula ni bunduki mbele ya adui na majaribu. Yesu Kristu anasema: "Namna hii haiweze kutoka, isipokuwa kwa kuomba na kwa kufunga" (Marko 9,29). Na Mt. Bazile aliandika: "Kama unataka kuwa moyo yako nguvu, kamata mwili yako na kifungo ya kula.

Kifungo ya kula ni hamuri ya kwanza ndani ya Paradizo. Kila dini inachunga hii hamuri. Ndnai ya dini ya Kristu Kizila (kifungo) ni hamuri ya Mungu na inapaswa waaminifu wote ya kuchunga hii sheria. Hii fazila ya kizila pamoja na saidio ya wamaskini inasaidia mukristu moja kupanda juu pia mu uzima ya kiroho yake. Kifungo ni usingi, musaidizi na muchungaji ya ma fazila yote. Ni mwanzo ya kutembea mtu moja njia ya Kristu, ni mwangaza ya uzima takatifu, ni mama ya sala, ni chemchem ya akili na mwongozi ya matendo mazuri yoyote". (Mt. Isaaka wa Syria).

Kifungo ya kweli haiko paka chakula bila mafuta, lakini ni kifungo ya kusimamisha zambi zetu. Unataka kuchunga kifungo? Onyesha hii fazila katika matendo mazuri yako. Kama utaona mtu moja maskini, umusaidie. Kama utaona adui yako, sikiliza naye. Kama utaangalia rafiki yako ya kuendela nzuri mu uzima yake, hapana kumuxhukia... Usifanye paka kizila katika mwili yako, lakini chunga na macho na masikio na mahasa yako yote" (mt. Yoane Krisostomo). Kifungo mu Kanisa Orthodokse inasaidia juu ya kuua mukristu zambi na ma zoezo mabaya yake na hapana ya kuua mwili yake.

## Desturi ya mafungo ya kula ya mwaka muzima ndani ya Kanisa Ortodokse

1. Kwarezima Kubwa ya Pasaka. Inaanza siku ya Kwanza, Kisha siku ya Mungu ya triodi (jivini) mpaka siku ya Posho, siku moja mbele ya Pasaka. Hii wakati ya Kwarezima tunakula chakula bila mafuta kila siku, ila tu muPosho na siku ya Mungu, pahali tunakula chakula na mafuta. Paka mu Posho Mkubwa, siku moja mbele ya Pasaka hatukula hatukule na mafuta.

2. Kwarezima ya Kuzaliwa kwa Kristu

Inaanza tangu tarehe 15 ya Mwezi ya Novemba mpaka tarehe ya 24 ya mwezi ya Decemba. Hii wakati tunakula chakula na mafuta, ila tu siku ya tatu na siku ya tano, pahali tunakula chakula, bila mafuta. Tena tunakula samaki mpaka mu tarehe 17 ya mwezi ya Decemba, ila tu siku ya Tatu na siku ya Tano. Kifungo ingine nguvu kabvisa ni hii: Waaminifu weingine wanakula samaki paka kila mu Posho na mu Siku ya Bwana, ila tu siku ya tatu na siku ya Tano, na mpaka mu tarehe 12 ya mwezi ya Decemba.

3. Kwarezima ya Mwezi ya Augusti (mwezi ya mnane)

Inaanza tangu mwanzo ya hii mwezi mpaka mu tarehe 14 ya hii mwezi umoja. Tunakula kila siku chakula bila mafuta, ila tu mu Posho na siku ya Bwana, pahali tunakula chakula na mafuta. Samaki tunakula paka kwa Siku Kuu ya Mageuzo Sura ya Bwana wetu Yesu Kristu, mu tarehe ya 6 ya Augusti.

4. Kwarezima ya Mitume Petro na Paulo (29 ya mwezi ya (Sita) Yunie.

Inaanza tangu siku ya Kwanza kisha siku ya Bwana ya Watakatifu wote mpaka mu tarehe 28 ya mwezi ya Sita. Tunakula samaki na chakula ya mafuta siku zote, ila tu siku ya Tatu na siku ya Tano.

5.Mu tarehe 14 ya Mwezi ya Tisa (Septemba). Ni Siku Kuu ya kupandisha Musalaba ya Kristu.Tunakula chakula bila mafuta, ila tu ni sala ya kukesha.

6.Mu tarehe 24 ya mwezi ya Desemba, siku moja mbele ya Kuzaliwa kwa Kristu. Tunakula chakula bila mafuta.

7.Mu tarehe 5 ya Mwezi ya Yanuarie. Chakula bila mafuta.

8. Mu tarehe 29 ya mwezi ya Augusti. Ni Siku Kuu ya kukata Kichwa ya Mt. Yoane Mubatizaji. Chakula bila mafuta.

9. Kila siku ya tatu na siku ya Tano ya mwaka muzima tjnakula chakula bila mafuta. Hii siku ya Tatu juu ya kukumbuka sisi utoaji ya Yudasi, aliyemutoa Bwana Yesu Kristu mikono ya Wakuhani ya Waebrania juu ya kumusulubisba. Na siku ya Tano tunakumbuka Mateso na Usulubisho ya Mungu wetu Yesu Kristu. Kama ma siku hisi tukona shangilio ya Bwana Yesu ao ya Mzazi mwake, tunakula samaki na hapana mayayi na maziwa ya kukamatana.

Kama hatuna na mambo ya malari tunapaswa sisi wote Waaminifu waorthodokse ya kuchunga hii mafungo ya kula. Kama tukona mambo ya afya yetu tutamuuliza mpadri ya roho yetu.

**Kifungo mbele ya Komonyo Takatifu**

Kama waaminifu wanatimiza mafungo yote ya Kanisa yetu ya mwaka muzima, haiko lazima kabisa wafanya na kifungo ingine mbele ya Takatifu Komonyo. Wataweza kuchunga kifungo siku moja mbele ya Komonyo, pahali watakula kula bila mafuta. Kama tunataka kukomunyika siku ya Mungu, mu Posho tunakula asubuyi na kati ya mushana chakula na mafuta, lakini magaribi kitu ingine bila mafuta, kabisa matunda.

Tena, kama weko Waaminifu wenye wanachunga kifungo ya kila siku ya tatu na siku ya Tano ya mwaka muzima, kula paka mukate ya kukauka na maji, hawa wanaweza kula mu Posho hata na nyama na mu siku ya Mungu watakomunyika, lakini nani anakula mukate ya kukauka na maji siku mbili ya mwaka muzima?

## WATAKATIFU YA KANISA ORTHODOKSE

Katika Fundisho ya Kanisa Orthodoksa Watakatifu ni watumishi wa kweli wa Kristu. Ni waaminifu waorthodoksi wenye kwa upendo ukamilifu wao mbele ya Mungu na utii yao mbele ya Sheria Yake walimufurahisha na kwa neema ya Roho Mtakatifu walitakaswa, walitukuzwa kwa Mungu na japo walikufa, wanaishi na wanaomba mbele ya Mungu juu ya sisi wote, wenye muzima na wenye kufa.

Jina Mtakatifu waliikamata ku mwanzo paka hawa waaminifu walikufa kwa mateso mengi juu ya kuchunga imani ya Kristu mbele ye wa adui ya Kanisa Yake. Kisha mafukuzo ku mwaka 312, kisha kuzaliwa kwa Kristu walichukua hii jina na hawa wakristu, wenye waliishi uzima moja takatifu.

Sisi waaminifu tunasifu ukumbusho ya Watakatifu wote, kwa sababu hawa wanapata sifa na utukufu ndani yas Ufalme ya mbingu na wanasimama karibu ya Kiti ya Kristu na wanaomba kwa wokovu wetu. Tunasifu sisi na ma Picha yao. Hii usujudu inaenda kwa Uso yao na hapana kwa vitu vya Picha, nikusema kwa ragi na mbau. Tunawasifu Watakatifu, lakini tunaabudu Mungu wetu Yesu Kristu.

Namna gani tunasifu Watakatifu ya Kanisa yetu?

Tunajenga kanisa kwa Jina yao.

Tunaweka Mifupa yao pa Meza takatifu.

Tunabusu ma Picha yao.

Tunawatukuza na Ibada ya kwa sifa yao.

Tunaandika vitabu na mafundisho yao.

Tunasali mbele ya Mungu na tunawaomba wakuje kwetu kwa kutusaidia kwa maombi yao.

### 1.Sifa ya Mzazi-Mungu

Tunaanza kuhesabu Watakatifu wote ku Mzazi-Mungu. Jina yake ni Maria. Anaitwa na Mzaz-Mungu kwa sababu alizala Yesu Kristu Mungu wetu. Anaitwa na Mtakatifu Kamili (Panayia), kwani Huyu eko na utakaso yoyote ndani ya uzima yake kupita juu pia ya Watakatifu wote.

Anaitwa Bikira daima kwa sababu alipata mimba kwa namna ya ajabu, kwa sababu hasipatikana na mwanaume moja, lakini katika nguvu ya ajabu ya Roho Mtakatifu alizala Yesu Kristu Mungu muzima. Huyu ni Malkia na Mufalme ya mbingu na eko kupita mkubwa ya Watakatifu na ya Malaika. Kwa hivi na sisi tunamutukuza na hii mwimbo: "Yliye wa thamani kuashinda wa Kheruvi, uliye na utukufu kwa pita bila kiasi wa Serafi..." Paka Utatu Mtakatifu ni juu yake. Mzazi-Mungu Maria eko na fasi ya mbili kisha Utatu Mtakatifu ndani ya Kanisa ya Mungu. Mpadri, kama anaanza kufanya Matayarisho ya Proskomidi, atatosha Kipande ya Mzazi-Mungu na kisha atatosha ya Malaika na Watakatifu wote. Tunamushangilia kila mwaka mara Tisa. Nikusema tunamutukuza

Mzazi-Mungu mu tarehe ya 25 ya mwezi ya Tatu (Martie), Habari Njema yake. Mu tarehe 2 ya mwezi ya Saba (Yulie) ya Kuweka Manguo yake ndani ya kanisa yake mujini Konstantinopoli, mu tarehe 15 ya mwezi ya Mnane (Augusti) siku Kuu ya Kulala kwake, mu tarehe 31 ya mwezi ya mnane, ya kuweka Musipi yake ndani ya Kanisa ya muji Konstantinopoli, mu tarehe 8 ya mwezi ya Tisa (Septemba), kuzaliwa kwake, mu tarehe 28 ya mwezi ya Kuma (Oktoba), Mufuniko Takatifu yake, mu tarehe 21 ya mwezi ya kumi na moja Novemba), ukumbusho ya kuingia kwake hekaluni ya Solomono, mu tarehe 9 ya mwezi ya Kumi na mbili (Desemba) ya kupata mimba Mzazi mwake Mtak. Anna, mu tarehe 26 ya hii mwezi Desemba, Makutano ya mzazi-Mungu.

Kila siku ya Tatu ya kila Juma inajitoa kwa ukumbusho ya Mzazi-Mungu.

Mwimbo ya Akathistos ile tunasoma kila siku  na kabisa ile wakati ya Kwarezima ya Pasaka ni kwa sifa yake.

Mwezi ya Augusti inajitoa kwa ukumbusho na sifa ya Mzazi-Mungu.

Ndani ya kila Ibada tunapata na wimbo kwa utukufu yake na yanitwa Theotokion.

Na Mwana wake wa pekee Yesu Kristu anasikia maombi yake na anatusaidia. kw ahivi na sisi tunapiga magoti mbele ya Mama mwake, kwani tunajua ya kama atatusikia na atatusaidia Mwana wake kwa maombi yake.

## 2. Majeshi ya malaika

Majeshi ya Malaika yaliumbwa mbele ya kuumba mtu Muumba Mungu wetu.. Katika sauti ya Mtume Paulo "Hawa wote si roho za kutumikia, waliotumwa kutumikia wale watakaoriti wokovu" (Waebrania 1,14). Ni roho, bila mwili, bila kabila, hawakufe na hawazale moja kwa mwingine. Hesabu yao ni bila kuweza kuhesabu sisi. Majeshi yao ni Tisa:

Wa Malaika - Wakubwa ya malaika - Wa Nguvu

Hawa wa Mwanzo - Mamlaka -  Hawa wa kiti.

Jemadari - wa Kheruvim - Wa Serafim.

Imani ya Kanisa yetu ni hii, ya kamakila mwaminifu, kiila kanisa na muji ni karibu na Malaika moja sawa mulinzi na muchungaji yake.

Kazi ya wa malaika ni ya kumuhimidi na kumutukuza Mungu, bila kusimama na juu ya kumuomba kwa saidio yetu. Mungu anawatumia juu ya kusaidia ao ya kuokoa watu, kama weko na lazima ya saidio yao. Ni watumishi wa Mungu na, kama wanakuja katikati yetu, wanakamata nyuso sawa watu vijana. Vile alionekana Malaika Mkubwa Mikaeli mara mengi ndani ya matendo mengi ya Agano la Kale na Malaika Gabrieli ndani ya matendo mengi ya Agano Jipya.

Kanisa yetu inakataza ya kuabudu sisi majeshi ya Malaika. Tunawasifu sawa vile tunasifu na ma kundi yote ya Watakatifu. Namna gani tunawasifu?

1.Tunawashangilia na Ibada kwa Jina yao.

2.Kila siku ya kwanza ya kila Juma inajitoa kwa ukumbusho ya Malaika yote.

3. Mpadri anatosha kwa Proskomidi Kipande kwa sifa ya malaika yote.

4. Ku mwisho ya Sala ya usiku (Apodipnon Kidogo) tunasoma na sala mbele ya Malaika, sawa mulinzi ya nafsi na mwili yetu, mbele ya kulala.

5. Tunaimba Ibada (Paraklisis) ya Wa Malaika juu ya kutulinzi na kutusaidia.

## 3. Mtakatifu Yoane Mubatizaji na Mutangulizi

Mt. Yoane, katika sauti ya Bwana Yesu Kristu: "Katikati yao wanaozaliwa na wanawake hakuna mukubwa kupita Yoane Mubatizaji" (Matayo 11,11).

1.Huyu alikuwa Nabii kupita mkubwa ya Wanabii weingine ndani ya Biblia.

2.Alikuwa Mutangulizi wa Bwana na alitayarisha wenye uzima na wenye kufa juu ya kumupokelea Yesu Kristu.

3.Aliitwa na Mubatizaji wa Yesu Kristu na taifa ndani ya muto Yordani.

4.Alikuwa Mushahidi, kwa sababu alichinjwa na alimaliza hivi kazi kubwa yake.

5.Kanisa yetu katika wapadri inatosha Kipande ya Proskomidi na inakumbuka jina lake.

7.Kila siku ya Mbili ya kila Juma Kanisa yetu inakumbuka jina lake.

8. Ukumbusho yake inashangiliwa mara sita kila mwaka: Mu tarehe 7 ya Yanuarie (Makutano yake), mu tarehe 24 ya Februarie ukumbusho ya kupata mara ya kwanza na ya mbili Kichwa chake.

Mu tarehe 25 ya mwezi ya Tano, ya kupata kivhwa chake mara ya tatu. Mu tarehe 24 ya mwezi ya Sita, kwa kuzaliwa yake, mu tarehe 29 ya mwezi ya Augusti ya kukata kichwa chake na mu tarehe 23 ya mwezi ya Septemba ya kupata mimba mama yake mt. Elisabeta.

## 4. Mitume wa Kristu

Aliwachungua Bwana Yesu Kristu juu ya kumusaidia mu kazi Yake. Waliangazwa kwa nuru ya Roho Mtakatifu na walikamata ma zawadi yote na hawa weko wasingi ya Kanisa ya Kristu na kwa hivi Kanisa inaitwa Apostoliki (Wa Mitume). Hawa Mitume ni kupita wakubwa ya Watakatifu wote. Ila tu ya kundi hii ya Mitume kumi na mbili (12) Bwana yesu alichagua na Mitume weingine makumi saba (70), wenye walitimiza kazi ya Mitume wakubwa. Kanisa yetu inakumbuka ukumbusho yao mu tarehe ya mbalimbali lakini inashangilia na wote pamoja mu tarehe ya 30 y amwezi ya Sita (Yunie). Ukumbusho ya Mitume makumi saba inashangilia mu tarehe ya 4 ya mqwezi Yanuarie. Kila siku ya Ine ya kila Juma Kanisa yetu inakumbuka ma jina yao na inawashangilia katika wimbo ya mbalimbali. tena inawakumbuka ya kutosha Kipande yao mu Ibada ya Proskomidi.

## 5. Wapadri Apostolike.

Wapadri Apostolike wanaitwa hawa Wapadri walikuwa Wafwasi na Wanafunji wa Mitume. Hawa waliwafata ku mwendo yao, waliangalia na walisikia mafundisho yao. Kila mandiko yao, ile waliandika iko na nguvu na sifa kubwa mu kanisa yetu, kwa sababu yaliandikwa kisha wakati ya Mitume na yanatupatia mapokeo mengi ya zamani. katikati yao tunaweza kukumbusha ma jina yao:

Mtakatifu Klimis, askofu ya muji Roma.

Mtakatifu Ignatio, askofu ya muji Antiokhia.

Mtakatifu Polikarpos, askofu ya muji Smirni ya Azia Kidogo.

Ermaw, aliyeandika kitabu "Muchungaji" na

Papias, aliyeandika kitabi inaitwa: "Mafafanusho ya maneno ya ma siku ya Mungu".

## 6. Isapostoli (Mitume wa Kristu ya wakati ingine)

Maana ya jina Isapostoli ni hii: Katikati ya ma karne ya Kanisa yetu walionekana watu wakubwa, wenye walitumika kazi ya Mungu juu ya kusabaa fundisho na imani ya Kristu ndani ya inchi yao ao pa inchi ingine. Nikusema walitumika sawa Mitume wa Kristu zamani na sifa yao ni umoja na sifa ya Mitume wa Kristu. Hawa wanaitwa Isapostoli (wenye walipata sifa umoja na Mitume wa kristu).

Tunaweza kuandika ma jina yao:

- Mtakatifu mwanamuke Fotini wa Samaria (ukumbusho yake mu 26 ya mwezi ya Februarie na siku ya Mungu ya Tano, kisha Pasaka.
- Mtakatifu mwanamuke Magdalena mubebaji ya manukato (Mirofori), ukumbusho yake ni mu tarehe ya 22 ya mwezi ya Saba (Yulie).
- Wafalme ya Konstantinopoli Konstantino na mama yake Helena. Ukumbusho yao ni mu tarehe 21 ya mwezi ya Tano.
- Mtakatifu Thekla, ukumbusho yake ni mu tarehe ya 24 ya Septemba.
- Mitume ya kabila ya Slavi, jina yao Methodios na Kyrillo, ukumbusho yao mu tarehe ya 11 ya mwezi ya Tano.
- Mtakatifu Kosmas wa Etolos, ukumbusho yake ni mu tarehe ya 24 ya Augusti.
- Mtakatifu mwanamuke Nina ya inchi Georgia.
- Mtakatifu Vladimiros, mufalme ya inchi Rusia.
- Mtakatifu mwanamuke Olga na weingine...

## 7. Wa askofu-Wapadri ya Kanisa.

Wapadri wa kanisa wanaitwa hawa wapadri ya kanisa, kabisa waaskofu, wenye walichanguliwa kwa ajili:

1. Ya utakaso ya uzima yao, kwani walifata mwendo ya Kristu, bila shaka.
2. Walifata Fundisho ya Kanisa Orthodokse na walifafanusha nzuri Mandiko Takatifu.

3.Taifa ya Waaminifu Waorthodokse waliwafamia kwa ajili ya mufano na uzima takatifu yao.

Wingi katikati yao walikuja kwa makutano ya Ulimwengu na walijaribu juu ya kuchunga fundisho ya kweli na walikombanisha mafundisho ya uwongo. Hawa waliandika Fundisho ya kweli ya Kanisa yetu, mpango ya Makutano juu ya Dogme na ma Kanuni ya Watakatifu wote.

## 8. Washahidi.

Hawa Wakristiani, wenye walifukuzwa na waliteswa kwa ajili ya imani ya Kristu na kisha walikufa wanaitwa Washahidi. Kifo yao juu ya kuchunga mpaka mwisho ya uzima yao imani ya Kristu ni ukikiri ya Imani ya Kristu katika mapenzi yao. Kanisa yetu inatuwambia ya kama hii kiro yao kwa kutosha damu yao kwa imani ya Kristu ni Ubatizo ndani ya damu yao. Hii Ubatizo yao ni kupita kubwa ya Ubatizo ndani ya maji, kwa sababu huyu Mushahidi, kisha lufu yake katika mateso anapanda mbinguni, bila kuchafuka mara ingine hii Ubatizo yake.

Katikati ya ma karne tatu tangu ku mwaka 62 kisha kuzaliwa kwa Kristu mpaka masikilizano ya kusimamisha nvita mbele ya Waaminifu ya Kristu ku mwaka 312, walikufa wakristiani 11.000.000 (milione). Weingine walikuwa:

1. Washahidi wakubwa, kwa sababu waliteswa kabisa.

2.Washahidi wapadri, ni hawa walikuwa na wapadri ya Kanisa.

3.washahidi watawa ao Washahidi watawa na wenye bikira (wanaume na wanawake watawa wanaume ao watawa wanawake).

4. Washahidi, wale walikuwa wakristiani bila kuwa na cheo ya upandirisho.

5.Washahidi wanawake bikira, wenye waliishi uzima ubikira. Na

6.Washahidi wapya. Hawa walikuwa vijana na wapadri wenye walikufa na mateso mengi ile wakati ya utumwa ya Waturki mu inchi yetu Uyunani (Grece).

## 9. Wasimamizi ya imani

Wasimamizi ya imani ni hawa wakristiani walikikisha Yesu Kristu, lakini bado kufa, wala wafukuzo wao waliisha kufa, wala ilisimama ufukuzo wao. Kwa hivi hawa walikufa na lufu bila mateso. Kanisa yetu inawashangilia na makumbusho yao, katika sauti ya Yesu Kristu: "Basi kila mutu anayenikikiri mbele ya watu, nitamukiri vilevile mbele ya Baba yangu aliye mbinguni. Lakini kila mutu atayenikana mbele ya watu, nitamukana vilevile mbele ya baba yangu aliye mbinguni" (Matayo 10.32).

## 10. Walinzi ya imani ya Kristu.

Dini Kristianisme, kisha onekano yake ndani ya dunia ilitetemehsa mazoezo, ma dini na ma kabila ya wati ile wakati. Kwa hivi ilikuwa mbele ya Wayudea Kikwazo na mbele ya Wayunani upumbafu" (Barua ya kwanza kwa Wakorinto 1,23).

Wapadri na Wa askofu wenye walininzi ya Dini ya Kristu katika mauhubiri na vitabu vyao mbele ya wafalme wapagano ya Roma na wafukuzo ya Kristu waanaitwa Walinzi. Mu lugha kingiriki Apologites.

Kisha hawa Walinzi ile wakati ya kusabaa dini ya Kristu, walionakena na Walinzi weingine ile wakati ilisabaha dini ya uwongo ya Mohameti ku mwanzo ya karne saba. Walinzi weingine walionekana na sasa, ile wakati dini ya Kristu inafukuzwa na inachekelewa kwa hawa wanamukana Kristu.

Walinzi ile wakati ya mafukuzo ya Wafalme ya Roma walikuwa wingi, Tunaweza kuandika sasa ma jina kidogo yao: Kodratos, Athinagoras na Aristidis toka muji Atena ya Uyunani (Grece), Yustinos Mushahidi na wa akili toka Palestini. Klimis wa muji Aleksandria ya Misri, Origenis toka Msiri na Tertyllianos na Kyprianos toka Afrika.

## 11. Watawa Watakatifu.

Kisha mwisho ya nvita ya wafalme wapagano mbele ya Kanisa ya Kristu, ilisimama uwazo ya kama na uzima katika Kristu ni umoja na lufu ya washahidi. Kwa hivi, waaminifu wingi katika sauti ya Mtume Paulo: "Tokeni katikati yao, mukatengwa nao,..." (barua ya mbili ya Wakorinto 6,17)

walijitoa kwa Kristu na uzima yao yote. Hii ondoko yao ku dunia na nyumba yao ni mateso ya mioyo yao na ni umoja ya kutosha damu yao kwa imani ya Kristu.

Hawa ni watawa, watawa wa jangwa na wenye walikimbilia ndani ya jangwa ao ndani ya pori mbali ya watu, ao hawa waliishi ndani ya monasteri ao ndani ya pango ya milima. Matunda ya hii uzima yao ilikuwa usafishi, mwangaza ya akili yao na ukamilifu yao kwa zawadi ya Roho Mtakatifu. Saidio yao kwa maombi yao, vitabu ile waliandika na miujiza yao yalikuwa usingi kubwa mu uzima ya Wakristiani. tena walijaribu juu ya kusimamisha imani ya dini ya Kristu na walikombanisha wa dui ya Kanisa Yake katikati ya ma karne yote. Tunaweza kuandika na ma jina ya hawa wakubwa kabisa, sawa Mtakatifu Mutawa Antonio wa Misri, Mt. Pakhomios wa Misri. Savvas Mutakaswa, Eftimios, Theodosio mkubwa ya uzima ya watawa ndani ya Monasteri yake, Makarios wa Misri, Athanasios Wamulima Takatifu ya Uyunani (Grece) na weingine wingi.

### 12. Wenye Haki

Hawa wote waliyoishi mbele ya uzalio ya Kristu, kufwatana sheria Takatifu na kwa kitumaini ya kufika duniani Yesu Kristu wanaitwa wenye Haki. hawa ni sawa Wazazi wa kwanza ya dunia nzima na wafwasi wao, Wababu wa Mungu, Wanabii, Wapatriarchi, Wafalme na weingine.

## MITUME WA KRISTU.

Mitume wanaitwa wanafunji kumi na mbili ya Yesu Kristu, wenye waliacha vitu vyote ya dunia na walimufuata Kristu mu zima na kazi yake mpaka ile siku ya Kupanda kwake mbinguni. Kisha kwa kushuka Roho Mtakatifu walifanyika wahubiri na washuhuda ya imani ya Kristu kwa ukombozi ya dunia nzima ku zambi na walisaidia kwa kusambaha Ufalme wa Mungu pa inchi yote. Jina Mitume aliwapatia Huyu Yesu Kristu. "Ulipokuwa muchana akata wanafunzi wake, akawachagua kumi na wamili katikati yao, aliwapa jina la Mitume" (Luka 6,13).

Kwa uchagua ya Mitume mwake Yesu Kristu alisimama ya kuchunga karibu yake mitume kumi na mbili sawa vile na watoto ya Yakobo walikuwa kumi na wawili, hawa walikuwa Wapatriarchi ya ma kabila kumi na mbili ya Israeli. Hivi na hawa Mitume kumi na wawili walifanyika wakubwa ya Israeli mupya, nikusema wakubwa ya wale watu wenye watasadiki na watamufuata Kristu.

Pempeni ya hawa kumi na wawili Kristu alichagua na weingine makumi saba. Hesabu yao ni umoja na wale wapadri wenye aliwachagua Nabii Musa juu ya kumusaidia mu kazi ya kutembesha taifa ya Israeli kufuatana sauti hii mu Agano la Kale.

Katikati ya Mitume kumi na wawili Kristu alichunga karibu yake kabisa Mitume tatu: Petro, Yoane na Yakobo. Hawa walimufuata kwa kila kazi na mwendo Yake. Juu ya nini alichagua hawa wa Tatu? Kwa sababu Petro alimupenda kabisa Kristu, Yoane alimupenda kabisa Yesu na Yakobo alikubali kunywa kilauri ya mateso yake, sawa Mwlaimu yake. Na kweli Yakobo alikufa na haraka, kwani alimuua Herode ku mwaka 44, kisha kuzaliwa kwa Kristu.

Mitume wote walikuwa toka jimbo Galilaya na paka Yudas Mutoaji yake alikuwa toka Yudea. Walikuwa watu wasiyo akili, kwani hawakufate mafundisho ku masomo. Walikuwa wavuvi, watozakodi, lakini walisadiki kwa Mungu na waliongojea kufika Kristu sawa Mwokozi duniani. Kwa sababu walimufuata Kristu, walijua na waliangalia matendo na mafundisho yake yote. Hawa waliendelesha kazi ya Mwalimu wao na walitembelea ku muji moja ku ingine kwa kuhubiri bila kuogopa wakubwa na mateso yoyote. Na sisi tunapaswa kuwafamia na kuwasifu.

Mtume wa kwanza alikuwa Petro. Huyu zamani aliitwa Simoni. Alikuwa na bibi, bila kufata masomo, alikuwa ndugu ya Andrea aliyeitwa ku Kristu ku mwanzo na wa wili walikuwa wana ya Yona toka mukini Bitsaida ya Galilaya.

Huyu Mtume alimwambia kuwa mwenye heri Yesu Kristu na alimuitwa Petro, na juu ya imani yake alikamata mpango juu ya kujenga Kanisa Yake. "Heri wewe, Simoni wa Yona; kwa kuwa mwili na damu...lakini Baba yangu aliye mbinguni. Nami ninakuambia, Wewe ni Petro, na juu ya mwamba huu nitajenga kanisa langu; wala milango ya Hadeze haitalishinda" (Matayo 16,17-18).

Huyu alihubiri ku mwanzo mu Yudea na muji Antiokhia, kisha mu inchi Azia Kidogo na alifika mpaka muji Roma ya Italia. Alikufa ya kusulubiwa ya kutundikwa mwili yake na kichwa

chake chini, sawa vile na yeye aliomba akufe hivi ku mwaka 66-69. Aliandika ma barua ya wili mu Kanisa ya Kristu.

Mtume wa mbili ni Andrea mwenye kuitwa wa Kwanza. Zamani alikuwa mwanafunzi ya Yoane Mutangulizi. Huyu alimukokota na ndugu yake Petro, wakati alimwambia: Kuja tulipata Mwokozi". Huyu ni musingi ya kanisa ya Konstantinopoli. Alihubiri Evangelio ya Kristu pempeni ya Bahari Meushi, kisha mu jimbo ya VIthina ya Azia Kidogo, mujini Vizantio. Kisha alihubiri mu inchi Rumania na aliingia mu Uyunani (Grece) na alifika mpaka muji Patra. Kule alifanya miujiza mengi, na kwa sababu watu wingin walisadiki kwa Kristu, mkubwa ya muji, jina lake Egeatis alimupingilia pa Musalaba lakini ya kuweka chini kichwa chake. Kisha wakati wingi Mwili yake walipeleka mujini Konstantinopoli.

Mtume wa tatu alikuwa Yakobo, ndugu ya Yoane, mutheologo na Mwefangelizaji. Huyu alihubiri ndnai ya jimbo Yudea nzima. Mufalme Herode Agripas, kwa ajili ya nguvu yake na mahubiri bila kuogopa, alimuua ku mwaka 44 na hivi huyu alikuwa Mushahidi wa mbili, kisha Mushahidi wa Kwanza shemasi Stefano, aliyekufa ku mwaka 43, kisha uzalio ya Kristu.

Mtume wa Ine alikuwa Yoane, mutheologo na ndugu ya Yakobi. Huyu alimupenda sana Yesu Kristu, kwani alikuwa kijana kabisa. Huyu anaitwa Mwevangelizaji, Theologo, mwanafunzi ya upendo, Mupendwa wa Kristu, mwenye bikira, mwana wa Nguvu. Alihubiri mu jimbo ya Azia kidogo. Mufalme mupagano moja alimufukuza mu kisanga Patmos, pahali watu wingi wasadiki kwa Kristu. Wakati alirudia mujini Efeso alikufa na amani na kipimo yaker miaka 95. Huyu aliandika Evangelio na jina yake, ma barua tatu na kitabu ya Ufunuo.

Mtume wa tano ni Filippo, toka muji Vitsaida ya Galilaya. Huyu alisema kwa Natanaeli: "Tumeona Yeye aliyeandikiwa na Musa katika torati, na manabii waliandika juu yake, Yesu Mtu wa Nazareti, mwana wa Yosefu" (Yoane 1,45).

Huyu alihubiri Evangelio mu Azia Kidogo, mujini Yerapoli pamoja na Mtume Vartholomeo (Natanaeli) na dada yake Mariamni. Alikufa na materso mengi, kwani walimukimbilia mikono ya chini yake pa kimbao moja mujini Yerapolis.

Mtume wa SIta ni Vartholomeos ao Natanaeli.

Kwa huyu alisema Yesu Kristu, wakati Natanaeli alimukaribia: "Tazama Muisraeli kweli, hana hila ndani yake" (Yoane 1,47). Alihubiri Evangelio ya Kristu mu taifa ya India na aliwapatia Evangelio ya Matayo. Lakini wale watu wasiyoamini walimusulubisha mujini Urvanupoli. Pale alikufa na alitoa nafsi yake mikononi ya Kristu.

Mtume wa saba Thomas.

Huyu anaitwa na Didimos (Mupasa). Kwa huyu alisema Yesu Kristu: "Usiwe usiyeamini, lakini mwenye kuamini" (Yoane 20,27) na huyu alimugusha Kristu na alisema: "Bwana yangu na Mungu wangu" (Yoane 20,28). Alihubiri mu taifa ya Persia na India. Mufalme ya India, kwa sababu Thomas alibatiza mwana wake, alimufunga ndani ya kifungo na ku mwisho alikamata mpago juu ya kumuua. Wa askari wake walimupingilia na mishale yao na walimuua.

Mtume wa mnane ni Matayo Mutozakodi, ndugu ya Yakobo wa Alfeos.

Huyu alimufuata Kristu, lakini mbele aliacha kazi yake. Kisha ile karamu aliifanya kwa Kristu alifanyika Mtume na Mwevangelizaji. Alihubiri mu inchi ya Parthia na Persia, pahali alijenga na ma Kanisa na alifanya miujiza mengi. Ku mwisho walimuua wa adui wa Kristu.

Mtume wa tisa ni Yakobo, mwana ya Alfeos, ndugu mudogo ya Matayo.

Anaitwa Yakobo mudogo ao Levi. Hatujue kabisa fasi gani alihubiri. Lakini wa adui wa Kristu walimukamata na walimutundika pa musalaba na hivi alito anafsi yake pa mikono ya Kristu.

Mtume wa Kumi ni Simoni wa Kana ya Galilaya. Huyu alihubiri mu jimbo ya Mavritania ya Afrika, pahali alikufa pa musalaba sawa Yesu Kristu.

Mtume wa kumi na moja ni Yudas wa Yakobo. Huyu tena anaitwa na Leveos ao Thadeos. Huyu alikuwa ndugu ya Yakobo, ndugu ya Yesu Kristu, nikusema alikuwa mtoto ya Yosefu, mulinzi ya Bikira Mama ya Yesu Kristu. Maana ya jina yake Leveo ni muhodari na Thadeos mu lugha Kiaramaiki maana yake ni Mupole na mtu mwema. Huyu aliandika barua ya Yuda. Alihubiri mu inchi ya Irak (Mesopotamia). Kisha alienda mujini Edesa, pahali aliponyesha mkubwa ya inchi Avgaros. Ku mwisho walimusulubisha pa musalaba na walimuua na mishale.

Mtume wa Kumi wa wili alikuwa Mathias, aliyekamata fasi ya Yudas mutoaji wa Kristu.

Kisha ya kupanda mbinguni Bwana Yesu Kristu, Mitume walichagua wawili, katikati ya Mitume makumi saba na walisali na walichukua Mathias. (Matendo ya Mitume 1,24.26). Huyu alihubiri Evangelio ya Kristu mu inchi Ethiopia. Alivumilia mateso mengi na alitoa nafsi yake mikononi ya Mungu.

Hawa Mitume kumi na mbili na hawa makumi saba pamoja na Wanawake wafwasi wa Yesu walikuwa wote 120 watu (Matendo 1,15). Hawa tunapaswa sisi kujua ya kama hawabatizwe sawa sisi katika maji, kwa sababu walibatizwa ile siku ya Pentikosti katika Roho Mtakatifu.

Mtakatifu Mtume Yoane anasema safi ya kama Yesu Kristu hakubatiza "...Lakini Yesu mwenyewe hakubatiza, lakini wanafunzi wake (Yoane 4,2). Tena na Mt. Yoane Mubatizaji alisema juu ya Bwana Yesu Kristu: "Mimi ninawabatiza ninyi kwa maji, lakini mumoja anakuja, mwenye uhodari kuliko mimi, sistahili kufungua kamba ya viatu vyake" (Luka 3,16). Tena naYesu Kristu alikikiri kusema hivi: "Kwani Yoane alibatiza kwa maji, lakini ninyi mutabatizwa katika roho Mutakatifu nyuma ya siku ni nyingi" (Matendo 1,5). Hii malako ya Bwana ilitimizwa ile siku ya Pentikosti: "Gafula uvumi ukatoka mbingu kama wa upepo unaovuma na nguvu sana, ukajaza nyumba yote walipokuwa wameketi. Na zilionekana kwao ndimi kama za moto, zilizogawanyika zikawakalia kila mumoja wao" (Matendo ya Mitume 2,2-4). Kwa hivi hawakuwa na ubatizo ingine.

## UBATIZO YOTE YA MBALI MBALI

**Ubatizo ya kwanza ilikuwa ya Wayuda.**

Hii haisafisha zambi ya watu, lakini machafu ya mwili watu. Kwa mufano, kama mtu moja aligusha mifupa ya maiti ya mufu moja ao alikaribia kwa wagonjwa ya ukoma, alinawa. Kama mpaka magaribi alikuwa munye uchafu, kisha ya kunawa na maji alikuwa musafi.

**Ubatizo ya mbili ilikuwa ya Yoane Mubatizaji.**

Huu ilikuwa kupita kubwa ya ubatizo ya Wayuda, lakini kupita chini ya Ubatizo yetu. Ilikuwa sawa kilalo katikati ya ma Ubatizo wa wili juu ya kuongoza watu toka Ubatizo ya Wayuda mu Ubatizo ya Kristu. Haikupatia wala Neema ya Roho Mtakatifu, wala maondoleo ya zambi, lakini alisukuma watu juu ya kufanya matendo mazuri na ma kazi ya kutubu (Matayo 3,8). Alitayarisha watu juu ya kubali Ubatizo ya Kristu.

**Ubatizo ya tatu ni ya Roho Mtakatifu.**

Kwa hii Ubatizo walibatizwa Mitume ile siku ya Pentikosti, pahali alishuka Roho Mtakatifu "...Lakini ninyi mutabatizwa katika Roho Mutakatifu nyuma ya siku si nyingi" (Matendo 1,5). Hawa haiko lazima ya kupata Ubatizo ingine.

**Ubatizo ya ine ni ya Bwana wetu Yesu Kristu.**

Huu ni ile alitupatia Bwana wetu. Inafanyika ndani ya maji inasafisha mwili na kwa Roho Mutakatifu inaangaza nafsi na moyo na inatosha zambi yoyote ya kila mutu anayetaka kuchukua hii Ubatizo. Huu ni ubatizo kuliko kubwa ya ma Ubatizo yoyote. Kwa hii Ubatizo walibatiza Mitume na kisha waliendelesha Wafwasi wao. Na mpaka leo inaendelea kumaliza Kanisa yetu huu Ubatizo. Paka huyu anayekamata mpango kubatizwa na hii Ubatizo ataingia ku Ufalme Mbingni katika sauti ya Bwana Yesu Kristu sawa vile alisema kwa mwanafunji wake Nikodimo. (Yoane 3,5).

**Ubatizo ya tano ni lufu kwa imani ya Kristu.**

Hii Ubatizo ni kupita isifiwa na kubwa ya ma Ubatizo yoyote, kwa sababu kisha yake hakuna namna mtu moja ya kupata uchafu na kufanya zambi mara ingine. Mushahidi anaingia ku Ufalme mbinguni kwa milele.

**Ubatizo ya Sita ni ya kutosha machozi ya toba.**

Ni ubatizo ya wale watu wanatubu kweli na wanatosha machozi juu ya zambi zao. Kwa machozi mtu moja anaweza kusafisha moyo na roho yake na atarudi sawa vile alikuwa mbele ya kuanguka mu zambi fulani. Mateso ya kufa mtu moja kwa ajili ya imani ya Kristu inaleta umivu na muchoko, lakini hii mateso ya kutosha machozi inapaswa mtu moja kuichunga mu uzima muzima yake. Nikusema ni kazi ya kuchoka na haiko kazi ya raishi.

**UTUKUFU KWA UTATU MUTAKATIFU**
**MONASTERI YA MT. GRIGORIO**
**KILIMA TAKATIFU 2005**